# CONSTITUTION OF KENYA REVIEW COMMISSION

# (CKRC)

## VERBATIM REPORT OF

## CONSTITUENCY PUBLIC HEARINGS, MALINDI CONSTITUENCY HELD AT KAKONENI CHIEF'S CAMP

ON

**MONDAY 29TH APRIL 2002.**

**CONSTITUENCY PUBLIC HEARINGS, MALINDI CONSTITUENCY**
**HELD AT KAKONENI CHIEF'S CAMP ON MONDAY 20TH APRIL, 2002**

**Present**

1. Com. Riunga Raiji
2. Com. Dr. Abdirizak Arale Nunow

**Secretariat in Attendance**

| | | |
|---|---|---|
| 1. | John Watabin | Programme Officer |
| 2. | Hilda Miranga | Rapportuer |
| 3. | Gladys Osimbo | Verbatim Recorder |
| 4. | Rose Samba | Sign Language Interpreter |

**The meeting was opened at 10.35 a.m with Com. Riunga Raiji in Chair.**

**John Watibini:** Makamishna tuliokuja nao ndio hawa, tuko na Makamishena wawili, watajijulisha kwenu na kikundi ambacho wameandamana nacho, halafu tuanze kwasababu naona saa zimeenda na hii siku ni yenu. Asanteni sana. Kamishna tafadhali tuendelee.

**Com. Riunga Raiji:** Hamjambo wananchi, na kwa niaba ya Tume ya Kurekebisha Katiba nina mkaribisha nyinyi nyote katika kikao cha kutoa maoni hapa Malindi. Mimi tuko na Commissioner Dr. Abdirizak Arale Nunow, jina langu ni Riunga Raiji mimi

ni Commissioner, pamoja nami tuko na tume ya kutoka Nairobi, tuko na Programme Officer Mr. John Watibini, tuko na hawa wengine ambao wanaandika habari ambayo mnatoa, Hildah Miranga, Gladys Osimbo na Rose Samba.

Kwa hivyo labda kama kawaida yetu kabla hatujaanza tutaomba na moja wenu atuongoze kwa maombi.

**Pastor Peter Ponda:** Basi na tuombe, tuna kushukuru Baba wa Bwana wetu yesu Kristo kwa wakati huu mwema ambao Bwana umetupatia, tunakushukuru kwa kutulikunda na kutuamsha vyema na hata Bwana kutuleta pamoja wakati huu, tunakushukuru hata kuwaleta wangeni wetu kuwa pamoja nasi ili Bwana tukapate kushirikiana pamoja juu ya jukumu hili ambalo Bwana ni kubwa la kuweza kuangalia na kuweza kurekebisha Katiba yetu ya Kenya, tunaomba Bwana ukapate kuwa pamoja nasi wakati huu tunapoanza, Bwana ukaanze na sisi na hata Bwana tuendapo mwisho tukapate kushukuru. Ukatuongoze, ukatuzaidie katika kila jambo na hata Bwana kila jambo mahali hapa likatendege kwa ajili ya utukufu wa jina lako. Ni katika jina la yesu aliye Bwana na Mwokozi tumeuomba na kuamini. Amina.

**Com. Riunga Raiji:** Pamoja na Tume ambayo imetoka makao makuu ya Commission, tuko na District Co-ordinator wetu hapa Bwana Jeffa Kingi, ambaye ninafikiri mnajua, nitamuuza labda atujulishe kama kuko na wanachama wa Constiuency Committee hapa ili tuwajue kabla hatujaanza.

**Jeffa Kingi:** Hapa kuna wana kamati, mwanzo kabisa tuna Pastor Peter Ponda, yeye ndiye mwana kamati anayewakilisha eneo hili la Kakoneni., pale tuna Rose Mwatela, yule ni mwanakamati, anatuwakilisha upande wa Gethe na Watamu, na pale tuna msichana anaitwa Ummi Abudi, huyo anatuwakilisha sehemu ya Malindi, wote ni wanakamati wa tume ya Kurekebisha Katiba.

**Com. Riunga Raiji:** Asante sana Jeffa, utaratibu tutafwaata ni kwamba, labda wale walikuja mapema, tunajiandikisha, tutafuata, wale walikuja mbele watapata nafasi na watafuatwa na wale wengine, first come first served. Hapa kila mtu yuko huru kutoa maoni, unaweza kutumia lugha yoyote ambayo unafikiria ndiyo itakuwezesha kutoa maoni sawasawa. Na kama labda kuna mtu ambaye mnamjua ambaye asikii au deaf, tuko na Translator hapa, kwa hivyo mtuambie, tutampatia kila mtu tuseme dakika tano, kama uko na memorandum, hatutaruhusu mtu kusoma memorandum yote kwasababu zingine ni ndefu, tutawapatia dakika tano kutusahihisha tu, kutuambia tu sammary, halafu memorandum zote tutasikusanya, na tutarudi nazo, tutazitumia katika uaandikishaji wa Katiba. Na kama ungetaka kutoa maoni yako binafsi uko huru, tutakupatia muda usiosidi dakika kumi hivi na ukimaliza utajiandikisha ili tuwe na orodha ya wale wote ambao walichangia wakati tulikuwa hapa. Nafikiri kwa hayo machache tunaweza kuanza na Bwana Nathaniel Gandi, karibu, tutakupatia dakika tano utupatie tu highlights ya memorandum.

**Nathaniel Gandi:** Asanteni sana, mimi niko na memorandum ya Cherore Locational Leaders, public views on Constitutional Review. Sasa yangu ni Memorandum, nilipokua nimependekeza kuwa kama ningeenda through yote, hawa wengine wangekuwa na kazi ndogo ile ya kutoa kubwika kitu kidogo kidogo, maanake hawataenda nje ya hii, lakini dakika tano

hasitanitosha. Sijui mnasema aje?

**Com. Riunga Raiji:** Labda kwa sasa tunaona tuko na watu twenty one, si eti tunakataa kwa sababu tunataka kupatia watu wengi nafasi.

**Nathaniel Gandi:** Hawa watu wengi nafasi mtawapatia nafasi mtawapatia….

**Com. Runga Raiji:** Okey we will give him ten, it is okey ?

**Nathaniel Gandi:** These is a whole memorandum, the whole kitabu yote ile ndogo mlionipatia, I am going to prove that one.

**Com. Dr. Abdirizak Arale Nunow:** Wananchi nafikiri ni vizuri tuelewane, hii memorandum imeandikwa itaingiswa kwenye computer neno kwa neno hata moja haitarukwa, kwa hivyo ukisoma yote, nikurudia tu kile kitafanyika, kwa sababu ishaandikwa. Ndivyo tunasema utueleze points, upeane memorandum, itaingiswa kwa computer, neno kwa neno. Hivyo hivyo ndivyo itafanyika akisoma yote paka mwisho. Kwa hivyo mtakuwa mume-save time akitueleza points na apeane memorandum na a-sign register. Kwamba memorandum ya Gireseni amepaana tumeelewana, kwa hivyo akitupatia points aendelee.

**Com. Riunga Raiji**: Nafikiria tunaelewana ni labda ni management of time ndiyo shida.

**Nathaniel Gandi**: Time itaenda sawasa, mwisho ni saa kumi na moja hapa tunaweza kuka only two hours. Kwasababu tukimaliza hii, akuna kitu kingine wataongea, ni ile kupeleka some papers.

**Com. Riunga Raiji**: Okey, okey, tuseme hivi….

**Com. Dr. Abdirizak Ali Nunow:** Mmekubali tunampa time hata ikihisha yeye peke yake ni sawa?

**Wananchi:** Sawa

**Com. Dr. Abdirizak Ali Nunow**: Haya

**Com. Riunga Raiji**: Okey

**Nathaniel Gandi:** Basi hapa tunaanza na Preamble, katika preamble, we need a preamble in our Constitution. Yani tunataka utangulizi, katika utangulizi binadamu anajengwa katika pembe tatu ambazo ni za kiuchumi, kisiasa na kijamii.

Kwa hivyo katika uchumi wa Kenya tunataka uchumi ambao utakuwa sawa kwa wananchi wote na wale wananchi kunatoka ule uchumi, basi wawe watapata manufa zaidi kushida kule sehemu ambako hakutoki uchumi huo.

Katika upande wa Directive Principles of State Policy: Tunataka tuwe na serekali ambayo ni ya demokrasia, ambayo inasingatia transparency and accountability, yaani ule uwazi na uhajibikaji. Pia tunataka serekali iwe itaheshimu mila za kila sehemu na katika Wakiriama na Mjikenda wana mila, kama ambapo wakati wakupeleka, wakati wa arusi au wakati watu wanoana., lazima wapeleke kitu kinaitwa mnazi, kwa hivyo huu lazima uhalalishwe.

Katika Constitution Supremacy: Tunasema tunataka Parliament, katika kubadilisha Katiba, tunataka wananchi wausishwe, sio Katiba ibadilishwe na Bunge peke yake baadaya ya kuwa tumeshaiandika.

Na katika upande wa Citizenship: Mtu ambaye amezaliwa na wazazi ambao wote wanatoka katika nchi hii basi anakuwa automatic citizen na ambaye amezaliwa na mzazi mmoja ambaye anatoka hapa katika nchi pia anakuwa citizen, na rights zake ziwe sitaangaliwa vizuri zote. Na wakati wa kutoa kitambulisho, tunataka wanainchi wote wapewe vitambulisho na wapewe pamoja na passport. Sio Passport iwe ni kitu cha pekee cha watu fulani fulani tu. Na ukitaka passport unamaliza karibu ya miaka kumi. Tunataka passport itolewe pamoja na kitambulisho.

Tukifika katika upande wa Defence: Defence ibaki ile ile ambapo tuna Military, Pre-military, Police, Prisons, sibaki zile zile lakini pia kuwe na Defence Council na Minister of Defence, maanake vitu hivi haviko, vimewekwa kwa President's office pekee yake. Kwa hivyo kuwe na Defence Council ambayo itaangalia vitu hivi, ambao members watakuwa ni Defence Minister, Permanent Secretaries na wale Defence Commanders.

Katika upande wa declaring state of emergency: Basi hi Defence Council ihusishwe sio Resident pekee yake ana declare emergency, na pia Parliament iwesekuushwa katika ku-declare emergency ya nchi.

Katika Upande wa Political Parities: Tunafikia upande wa kuwa tuwe na party mbili tu, kawasababu tukiwa na party nyingi huwa ni za ukabila. Siwe party mbili kama zile za nchi ambazo simeendelea. Na party hizi sitapewa pesa kutoka kwa serikali. Sipewe pesa kutoka kwa public funds, ambapo sitakuwa sikiendesha shughuli zao za siasa. Na pesa hizi basi zitumiwa katika transport, security lakini zisitumewe kuonga wananchi ili wapigiwe kura. Kwa hivyo candidate yoyote atakaye onekana aki-bribe wananchi kwa kuwapatia pesa, basi candidate huyu awe disqualified mara moja kwasababu tunataka tuchague mtu ambaye amependwa na wananchi, atawatengenezea nini sio wauwapatia pesa.

Relations ( relationships) among political parties: Tunataka iwe mzuri between the Government and political parties.

Structure and Systems of the Government: Tunataka teuendelee na hii Parliamentary Government lakini, tuwe na Waziri Mkuu,

Prime Minister. Prime Minister huyu, atatoka katika chama ambacho kimeshinda. Rais au President, atakuwa ni ceremonial tu. Lakini mambo yote yanafaywa na Prime Minister.

Hatutaki unitary Government, maanake unitary Government it had marginalized us, the coastal people for a long time. Tumeachwa kando kwasababu ya Unitary Government. Sisi tunataka serekali ya Majimbo. Serekali hii ya Majimbo itaweza ku-control vitu kama, Natural Resources, Administration, Finances na Security. Kwa hivyo tunahitaji resikali ya majimbo.

Other way of involving power to the lower levels: Yaani power itawafikia namnagani watu wa huko chini. Tunataka tuwe na Governor katika region. Baada ya Prime Minister, tunakuwa na Governor, Govenor anafuatwa na DC, DC anafuatwa na DO, DO atafuatwa na chief na tunataka tuwe na headman, hatutaki assistant chief. Maanake ni kama duplication of work, itawesa kusaidia ku-save pesa nyingi. Tunataka, headman, Chief, DO, DC na Governor, na wote hawa wachaguliwe na wananchi. Na wananchi wawe na power ya kuwaida wakiwa wamekosea, tunaweza kuwafuta. Kwa hivyo basi, hatutaki Chief ambaye atakaa miaka hamsini na mitano na hatutengenezei. Ikiwa tunamuona hatutengenezei baadaya ya miaka mitano, tumuondoe, tuweke mwingine. Kwa hivyo tunataka yule ambaye atatufanyia kazi, hatutaki watu watakaa tu miaka hiyo yote na hatuwezi kufanya chochote.

Katika upande wa Legislature ambayo ni Bunge: Basi Bunge, the Parliament should have powers to make suggestions on appointments, PS, Ambassadors and those who are a appointed, previously hawa walikuwa wakichaguliwa na Rais lakini tunataka wawe wakichaguliwa kwa msaada wa Bunge. Sio Rais tayari asimame asema Ambassador wa pahali fulani ni fulani, kuwe na ushirikiano wa Bunge, ndio watu kama wao wachaguliwe. PS pamoja na Ambassadors. Na hata appointment zile zingine katika Federal Government, Parliament should remain a law making body, the Parliament should have unlimited powers to control its own procedures through standing orders.

Wabunge: Basi should remain part-time, wafanye kazi kwa siku nne, hizi zingine, siku hizi wanfanya kazi kwa siku tatu, nataka wafanye kazi kwa siku tano, kutoka Mondays to Fridays.

Katika upande wa umri wa wabunge: Wanaotaka kupiga kura umri hubaki vilevile wa miaka kumi na minane na wale ambao wanataka kupigania viti vya Bunge, kuwe na age limit ya miaka sabini na mitano, ikipita miaka sabini na mitano huwezi kupigania kiti cha ubunge, upishe vijana, young turks, wako wanaweza kuendelea. Basi hii iwe pamoja na Presidential.

Presidential na Parliamentary elections sifanywe siku moja. Na ile ya ma-councillor, ifanywe nayo siku tofauti. Kwasababu inapofanywa siku moja, utakuta watu wanoenda pale, ni ile hali ya kutaja chama kimoja tu, mtu hata si mzuri, lakini amejiingiza katika wenzake, basi inakuwa ni chogoro chogoro chogoro. Sasa hatutaki vitu kama hivi, tunataka kila mtu ajitetee mwenyewe, siku yake, ajitetee mwenyewe si ajiingize katika orodha ya kuikia tu pahali fulani kwa sababu wenzake wako pale ndani, kwasababu yule ni mzuri na yule pale ni mzuri na yeye yuko hapa katikati naye anapata kura mara moja. Hatutaki namna hivyo,

kura za madiwani, ziwe siku yake.

Na requirements za mumbuge: Mmbunge basi tunataka awe form four, na mean grade ya D+ and above, na pia awe amepita kingereza D+ na Kiswahili, hizo ni lugha ambazo atatumia kule bungeni. Na moral na ethical qualifications za yule Mbuge pia ziangaliwe, mbuge huyu ana tabia gani katika community yake. Na watu wawe na ruhusa ya kuwaita wabunge wao, wakiwa wamekozea, wakiwa they are not performing, wawe wanaweza kuwaita kupitia referendums yaani, kura ya maoni, watu wauliswe. Ikiwa mbunge hawezi kutengeneza kazi yake vizuri, atolewe na aingie mwingine sio akae paka miaka mitano. Kuwe na uhuru huu wa referendums, kura za maoni. Kusiwe na ubakuzi, wanawake, wanaume wote wana wesapigania hivi viti vya ubunge.

Basi tukifika upande wa Rais, asiwe na power ya ku-dissolve Parliament wakati wowote anataka, iwe ni power ya Parliament waangalie ni siku gani wanaweza ku-dissolve Parliament. Na siku ya kura iweinajuligana, wakati watu wakupiga kura sasa, wajue hata baadaya ya miaka mitano, siku gani watapiga kura tena. Isiwe ni mandate ya mtu mmoja atangaze ni siku gani ya kupiga kura.

Tukienda upande wa Executive yaani mamlaka: Tunaka katika qualifications za President basi siwe zile za kawaida, miaka thelathini na mitano, na yeye awe raia, academic qualifications pia ziwe ni zile zile za D+ and above, form four na awe amepita kingereza D+ na Kiswahili.

Na Presidential Tenure of Office: Muda wa Rais kuka katika madaraka, iwe miaka saba, iwe inatoshana na ile ya Prime Minister ya miaka mitano, kwasababu kule mbele tutaona wakati wa kupokesana uongozi, ikiwa waziri mkuu, wanaenda kwa kura, awe Rais bado yuku pale kwa miaka miwili, ikiwa Rais naye anaenda kupigiwa kura, baadaya ya ile miaka saba amemaliza, kuwe Prime Minister yuko kwenye kiti anaendelea na kutawala. Kisiwe na power vacuum. Sijui mtanielewa basi.

Sasa hapo tunafikia wakati President anaweza kutolewa katika office kwasababu ya misconduct na Provincial Administration bado tunaitaka lakini iwe itapitia kwa kura, Provincial Administrators wachaguliwe kama vile nilivyokuwa nimeshataja.

Katika Judiciary yaani mahakama: Tunakuta kuwa lazima tuendelee na Supreme Court, Constitutional Court na hii sasa Judiciary, mamlaka au mahakama basi tuna academic qualification zao zitakua sikiangaliwa na ile Judicial Commission. Tuna sehemu ya Kadhi, sehemu hii tunataka imalizike kwasababu, kadhi huwa anadumia denomination moja ya wahiislamu pekee yake. Kwa hivyo ikiwa analipwa na pesa za wananchi wote kwa nini ahudumie wahiislamu pekee yake? Ikiwa ni kuudumia wahiislamu pekee yake basi abaki kwa msikiti na alipwe nao, lakini azilipwe na pesa ya umaa. Kwasababu ma-bishop tunaona hawalipwi na pesa ya umaa, wanalipwa na makanisa yao na wanaoza watu, ikiwa kadhi anaoza watu, basi alipiwe na msikiti sio na umaa. Kwa hivyo hizi pesa zote za makadhi wote katika makorti yote Kenya yangezaidia kufanya mambo mengine.

Markoti yote nayo: Kuna ile hali ya kuwa ma-korti yako mbali sana na wananchi, maanake kuna sehemu inayosema haya ma-korti yatamfikia aje mwananchi, wananchi wanafuata haki, hawapati haki kwasababu ma-korti ni kama huko Malindi, kuna wengine hawawezi kwenda paka kule Malindi ni mbali… kwa hivyo basi tunataka korti zote zije paka locational level.

Katika Local Government yaani serikali za wilaya: Tunamtaka Meya na Chairman katika County Council na Meya katika Municipal Council wachaguliwe directily by the wananchi, wapigiwe kura, sio wachaguliwe na ma-Councillor huko. Maanake anaweza kununua ma-councillor kama sita na yeye anakuwa meya mara moja. Tunataka huyu Meya na Chairman achaguliwe na wananchi wenyewe.

Basi funds pia Local Council ziendelee kuweka funds zao na minimum qualifications za ma-Councillor, awe form four, D+ mean grade na D+ in English and Kiswahili, kwasababu tumeona kuwa ma-Councillor ambao wako semi-literate, huwa wanaenda kushikana na yule ambaye ni Clerk kule, naye ni mtu amesoma, kwa hivyo anawapeleka hivi na hivi na pesa nyingi sinapotea katika Councils. Kwa hivyo, tumetaka ma-Councillor ambao wamesoma, siyo ndiyo ma-Councillor ambao ni semi-illiterate.

Minister asiwe na power ya ku-dislove Councils, Councils hizi basi zitategemia ile Regional Government. Hii mambo ya 25% ya President apate katika kila Province, hatutaki namna hivyo, President awe yule amepata kura nyingi, sio lazima awe na 25% from provinces. Hatutaki President pia ana-elect Nominated Members of Parliament, hatutaki, maanake hawa Nominated Members of Parliament ndio wanaaribu kule, siku zote wanakuwa upande wa Government, hata motion fulani ikiwa ni ya kupigiwa kura, wao wanapita upande wa Government. Kwa nini tuwe na Nominated, basi tupaki na wale elected. Hatutaki Nominated Members of Parliament au Councilors. Wabaki wale wale waliochaguliwa

Katika upande wa kupiga kura: Tunataka wakati wa kupiga kura, yale madebe, ballot boxes ziwe transparent, ziwe unaweza kuona mle ndani, hatutaki matebe yale ambayo huoni mle ndani mmewekwa nini. Na tunataka baaadaya kura zimeshapigwa, ziesabiwe pale pale kwa kituo, hatutaki zitolewe hapa paka Malindi sikaesabiwe, tunajua mnatokea nini mle katikati, kwa hivyo sihesabiwe hapa na nambari ihende tu kule. The figure should go to Malindi na figure ya pahali fulani iunganishwe na tujue mtu fulani ameshida. Lakini kura zihesabiwe pale kwa Polling Station.

Tukifika upande wa Basic Rights: Basic Rights ziendelee zile zile customary, traditional believers, waendelee kupata rights zao, property inheritance, fair judgment, economic rights pia ziweko na tunataka hii Coconut Act iwe revoked. Maanake hii Coconut Act ndio mefanya watu hawawezi kugema, kwasababu hii Act hata Bunge likipitisha kule hii act inasimama. Inakatasa mnazi usigemwe, kwa hivyo coconut Act hii katika Katiba ilondolewe, ndio itafanya watu waweze kuendalea na na shughuli zao za mnazi.

WaKenya basi waweze kupata mahitaji kama health care, tunataka matibabu iwekwe bure, pia education iwe bure katika

upande wa primary kusiwe na kutoa chochote katika sehemu hizo, kwasababu kuna wanainchi wengi hawajiwezi na wakati wa health services, tunamuona hawezi kutoa pesa yoyote, kwa hivyo health services siwe bure.

Tukifika upande wa rights for groups: Hizi group za interest of women is not fully grantee in the Constitution. So we want it to be addressed, we want equal rights for women na specific concerns for disabilities kama education, security, employment, shelter, hizo sehemu tunataka ziangaliwe

Land and Property Rights: Individuals should have automatic ownership of land, the Government can acquire a private land but it should be for the betterment of the development of the area. Valuation ifanywe na Private Surveyor. The State Government and the Local Authorities have powers over the use of land. Issues concerning transfer and inheritance, lazima ziendelee, yaani mtu akiwa anataka kuuza kipande cha ardhi, basi lazima family member wawe consulted, watoto, bibi, sio mzee auuze tayari ardhi bila hawa wote kujua. Land Control Board iendelee. Hatutaki Landlords in absentia, hizi sehemu zote ambazo ardhi ziko katika mwambao wa mpwani na wenyewe wako ulaya, zingawanyiwe wanainchi zote. Tunataka zile sehemu zimewekwa lease ya 99 years, ikimalizika lease hii, sehemu zile zote zigawanyiwe wananchi wanaoishi hapo. Hii lease isiwe renewed tena. Kwa mfano hapa Chilore tuna church ambayo iko lease hapa ya 99 years, itamalizika May, zile miaka tisaini na tisa inamalizika May mwaka huu, ikimaliza wale wananchi wote wa Chilore mpaka barabara ya kwenda Sheila hii, upande ule wote, wakawanyiwe mashamba yao.

Kuna zile ardhi zile ambazo kuna wakubwa fulani ambao upewa ardhi huku mwambao wa pwani, hatutaki zawadi kama hizi, ardhi zile ziwachiwe wananchi wenyewe. Mtu aki-retire, asipewe zawadi hapa Coast Province. Hapa kuna wenywe wanakaa, sasa unapewe location nzima ni zawadi yako, hawa wananchi wengine wataenda wapi?

Basi tukitoka hapo kwenye land and Property Rights: Tunataka mila zote siwe sitaweza kuheshimiwa na hata za wamjikenda. Na katika unity ya nchi tunataka we should have one National language, Kiswahili, and two official languages, Kiwahili na Kingereza. Likini tuwe na one national language. Maanake tukiwa na lugha moja, basi tuweza kuungana vizuri zaidi.

Management and use of Natural Resources: Hizi Natural Resources tunataka basi ziwe ni jukumu la Regional Government na ziangaliwe nayo. Serikali ya Majimbo ipewe jukumu hili. Na ikiwa zimetoka katika jimbo fulani, kule katika Central Government kwende only one third, two thirds, sibakie hapa hapa katika jimbo ampako hizo Natural Resources zinatoka, ili iweza kufaidisha sehemu hiyo. Maanake currently tunaona kuwa sehemu kubwa zaidi inaenda kwa Central Government na huko kwenya Majimbo kuna wanjwa hakuna chochote.

Tukifika katika participatory: NGO hatutaki siwe zikuwa na participation in the Governemt, hatutaki NGO, serekali yenyewe iangalie mambo yake na iweze ku-regulate hii minendo ya NGO's.

International Relations: Basi Parliament iweze kutoa Consent. Sio mtu moja aitwe uko nchi za nje na akaweza kuweka sahihi tu kwa niaba ya nchi nzima. Lazima kitu hicho kijadiliwe na Parliament kwanza, ndio kama kuma treaty fulani, agreement fulani, iweze kuwekwa sahihi. Sio watu watatu wameenda nchi za inje, wanaenda kuweka agreement for the benefit of the people. Kwa hivyo hatutaki namna hivyo, tunataka Parliament ihusishwe.

Katika Constitutional Commissions and Offices: Tunataka hizo ziendelee, Human Rights, Anti-Corruption, Land Commission, lakini hizi Commissions zote ambazo zitaundwa baadaya, tunataka zitoe yale majibu yote ya zile Commissions zilizo undwa adharani, wananchi waambiwe Commission ilifanya kazi fulani na matokeo yake ni haya. Maanake tunaona Commission nyingi sinaundwa lakina majibu hayatolewi na zimetumia pesa ya serikali na wananchi. Kwa hivyo Commission ikiundwa itoe uhamusi wake wazi wazi kwa wananchi.

Kuna office moja hapa inaitwa the Office of the Ombudsman: Ambayo ni ile office ya malalamishi, watu huwa hawana pahali pakupeleka malalamishi yao, hii Office ya Ombudsman, tunataka iweko. Watu wakiwa wana malalamishi fulani juu ya serekali, kuwe na office fulani ambayo unaweza kupeleka malalamishi yako. Kwasababu ikiwa utaenda kwa DO, DC na hatakuzikiza, wapi utapeleka malalamishi yako, tuwe na pahali tofauti, office nyingine ambayo ni hii ya Ombudsman, ambaye tutaweza kumpelekea malalamishi yetu yote.

Tukifika upande wa Succession: Basi ni ile ambayo tumesema, kuwa katika Succession and transfer of power, ikiwa Prime Minister ametoka, basi to hand over immediately to the other Prime Minister. Na kiwa ni President ametoka baadaya ya miaka saba, basi to hand over immediately to the new President. Na hakutakuwa na vacuum katika utawala kwasababu ya Prime Minister ni miaka mitano na President ni miaka saba, kwa hivyo basi ikiwa Prime Minister wameenda kupigiwa kura, President ana miaka miwili anendelea. Ikiwa President anapikiwa kura naye baadaya ya miaka saba, Prime Minister naye alijaguliwa miaka miwili iliyopita naye anendelea, ako na miaka mitatu. Kwa hivyo hakuna power vacuum hapo.

Basi kufikia hapo tumefikia mwisho na yale yaliyobakia ni wananchi wenzangu, basi asanteni sana kwa kunisikiliza.

**Com. Riunga Raiji:** Asante sana Bwana Nathaniel kwa maoni haya ambayo labda umezunguzia kuhuzu yale maneno yote, nafikiri tuliandika katika kile kitabu. Na asante sana kwasababu tunaona hiyo si maoni yako ni maoni ya watu wote wa Chilore, Tumesema asante. Sasa wapili ni Raymond K. Thoya, Bwana Thoya karibu.

**Raymond K. Thoya:** Makamishna, Mabibi na mabwana, ninaongezea tu yale ambayo tumesha somewa na Bwana Nathaniel Gandi, kunasehemu ambazo ninataka kutilia mkazo.

Jambo la kwanza, mimi na kijana yule, twaona kwamba tunatofautiana katika umri. Hivi kwamba inaonyesha sisi au mimi ni mmoja wapo katika wale ambao tuliteswa wakati wa ukoloni. Hapa, hapa tulipo, ni mahali ambapo tumeishi kwa miaka mingi,

lakini ni baadaya ya sisi kuteswa na wakoloni wa mara tatu.

Ningelitaka mnifahamu baadaye kamishna, hivi kwamba sisi wa hapa pwani, sisi Wamjikenda wa hapa pwani tunatofautiana na wenzetu wale wa kule baara, kwa vile sisi tulikaliwa na wakoloni wa mara tatu, kulikuwa na mreno, mwarabu na mzungu. Hawa wote walitukalia sisi, sasa ni juzi tuu mwaka wa sitini na tatu, ndio wakoloni wawili hawa, mwarabu na mzungu wakatuachia ushukani.

Lakini katika kupikania uhuru huu, tulikuwa tunapigania land. We were fighting for land. Unfortunateiy, Constitution hii ambayo tunayo ilituadhiri mno, kwasababu sisi hatuna ardhi, ardhi yetu kama mnavyoona ni ardhi ile ambayo haina kitu. Commissioners, mmetoka Malindi kuja upande huu, mmeona namna mvua inavyo endelea kule lakini, nje uko iko mvua? Huku akuna mvua, makosa yalitokea wakati hule wa kugawanywa ule mwambao na best region, zile sehemu ambayo ndiyo nono zaidi. Ikachukuliwa na warabu, sisi tukasukumwa huko ambako hakuna mvua. Na Constitution hii akazidi kutuumiza, kwa hivyo tunataka Constitution hii on land Treaties, Coastal iwe kitu gani, hii Coastal Treaty ifutwe. Na ardhi zile ambazo zilikuwa by rights tusipate sisi. Lakini Constitution haikutupatia. Kwa hivyo ningaliomba Constitution hii iweza kuvumba, kusije sisi nasi ikatulasimu tujukue hatua kama zile zilizo kuwa kule Zimbabwe. Kwasababu, hapa Malindi kuna ng'ombe za grade, mmesiona nyinyi makamishna, ng'ombe za grade zile hasiwezi kuishi hapa, hasiwezi kamwe, kwa hivyo sisi tutaendea kuwa masikini daima daima.

That is not good, that is not good. That is not what we fought for. We fought for land. And it si from the Indian Ocean to lake Victoria. Hapa kuziwe na mtu mkoloni mwingine hapa, ambaye ametufanya sisi tuwe masikini, masikini miaka hiyo yote. These Constitution is the one which as contributed to the squatter problems. So we want hii kitu ifutwe kabisa. Ili nchi ile ambayo ndiyo nono ikwanyiwe sisi ambao ni the indegious people. Bendera hizi mbili ya mwarabu na mzungu zilianguka siku moja. Mzungu yeye akafunga virago akaenda kwao, lakini huyu mwingine alikuwa ametetewa na hii Costitution. Kwasababu tunajua kwamba Sultan wa Zanzibar wakati huo, alipewa nafasi kule London, ndio akaweka vifungu fungu vyake kule kwamba hoo eeeee, nataka Constitution hii iweza kuwalinda watu wangu, ana watu wake huku, na mali zao. Sisi maskini ya Mungu hatukuwekwa pale na hali sisi ndio wenyewe. Tulipigania Uhuru kwa ajili ya ardhi hii, so these Constitution has been very bad to us. Infact we were surpporting one great politician, yule ambaye aliandika kwamba "Not Yet Uhuru". We are were supporting him, because how can we say that were are uko-free and you don't have land. Hata uko tuliko ambako ni baara kavu, kisha no Title Deeds, nothing, nothing, so Constitution hii tafadhali tunataka ifutiliwe mbali pale mahali pakwamba hapa tulikuwa na treaties, treaties za akina nani? Na ile ardhi ambayo nio nzuri kama vile mliovyoona nyinyi Kamishna, there is a great difference between where you come from and here. We are just wondering Tsavo National Park, ikiwa hapa tu. Sasa sisi ni watu wa kuangaika na ni hii Constitution ndiyo walituumiza sisi.

Kijana huyu Nathaniel Gadi amezungumzia habari ya mtu mmoja kuwa na powers, yeye aweze kutoa ardhi, sasa kama mtu yule aliye kuwa na powers, angewapa zawadi wao waliotunukiwa upande huu ambako akuna mvua, sisi tungelishukuru. Lakini yeye

aliwatunukia mahali kule ambako ni kunono. Jamaa zetu walikimbiswa huko. Imagine what type of a Constitution, what type of Government, what type of I don't know. Wewe umeishi hapo na kwa vile you don't have the Title Deed, Title Deed ni karatasi, unakuja kuondolewa hapo, mnatupwa huku na mtu anawekwa huko ambako ni kunono. Sisi tunazungumza kwa uchungu. Tunazungumzia habari ya uchungu, pale polipokoseka, tafadhali Constitution hii iweze kujua ya kwamba kuna kitu and that is why we had tribal clashes here, leave alone about huko juu. Lakini sisi hapa kutoka huko upande wa Digo kwenda hivi paka uko, is the same problem, which was created by these Constitution, so land is the first thing which as to be rectified.

Haya mengine yameshazungumzwa kwa hivyo na hata kama ni ardhi zile ambazo ziko town, kama Mombasa vile, ile Mombasa karibu, karibu three quarters ni ya watu, just a few individuals. Hapa Malindi, the whole town belongs to just afew individuals, how can that be? Kwa hivyo hii Constitution ilikosa pale, kwa hivyo kama ni Malindi, kuna just a few individuals ambao they own, or they were given the ownership, ikatiliwe mbali hiyo na wananchi wenyewe walizumbuka kupigania uhuru waweze kupatiwa hizo. Asanteni makamishna kwa vile nimezungumzia habari ya ardhi pekee yake.

**Com. Runga Raiji:** Asante sana Mzee, nafikiri tutaenda kwa haraka kwasababu nimeona sasa list ya watu niko nayo ni watu hamsini na wawili. Nafikiri sasa tunakubaliana kila mtu tumpatie kama dakika tano hivi tupate nafasi ya kusikiza wengine. Ni hivyo?.

**Wananchi:** Ni hivyo

**Com. Runga Raiji:** Okey asanteni, sasa nitakua nikipiga piga hivi…wakati saa yako imeisha. Okey asanteni. Sasa tuko Mariam Katana Mariam, labda atakuja baadaye. Karibu mama.

**Miriam Katana**: Mimi nitaongea kwa kigiriama kwasababu hawa wakina mama wengine wote ni wa kiriama, hawa wazee hawana neno.

**Miriam Katana:**
**Translator:** Anasema wasichana wana shida sana hapa, baadaya kumaliza masomo, anaenda kutafuta kazi, anapata mkubwa pale yeye ambaye ni boss, kabla hajampatia kazi, anasema mpaka wafanye mapenzi naye ndio apate kazi.

**Miriam Katana:**
**Translator:** Anasema kwamba wakati mwingi pengine unamatatizo na Bwanako, unaenda kwa chief, ambaye anakwambia basi wataka nini? wataka nikuoe ama nifanye nini? Nenda ukasawasishe mambo yako na Bwanako.

**Mariam Katana:**
**Translator:** Kwa hivyo akirudi kwa Bwanake, yeye anafura kichwa anasema umeenda kwa chief na akakuregesha hapa, kwa

hivyo nitakupiga paka nikuue, akuna kuondoka tena hapa.

**Mariam Katana**:

**Translator:** Kwa hivyo, asema kwamba wale wakubwa, wa-boss walakayi ambao wanataka kufanya mapenzi na wasichana, ndio waandike kazi, wakipatika na vitu kama hivyo wafutwe kabisa na wafungwe jela, wasiregelee kosa hilo.

**Miriam Katana:**

**Translator:** Kuna wakati mwingine kwamba msichana anakaidiwa, anafanyiwa mpenzi kwa lazima, akienda apige report, ikiwa ni kwa chief au police, anaambiwa nenda mkasuluishe nyumbani kwa hivyo wale vijana ni kama wanafura vichwa.

**Miriam Katana**:

**Translator:** Kwa hivyo ninaona kwamba wasichana wanazaa watoto ambao hawataki, wanapata mimba ambazo hasisitahili, kwa hivyo wanasorota uchumi wa wasichana, maanake itabidi sasa ampeleke kwa nyanyake yule mtoto na itakuwa ni mzigo tena.

**Miriam Katana:**

**Translator:** Kwa hivyo, anasema kwamba ile punishment, ile adhabu ya mtu amekaidi msichana iwe ni kifungo cha maisha na tena viboko juu yake.

**Miriam Katana:**

**Translator:** Wakati mwingine mahari imejukuliwa kama ni kitu cha lazima, kwa hivyo twaona waesaenda kwa Bwanako, ukaolewa, ukazaa watoto wawili, baadaye anakwambia hana haja nawe tena.

**Miriam Katana:**

**Translator:** Kwa hivyo, maoni yake ni kwamba matatizo kama haya ya kitogea, akuna kuregesha ile mahari kwa Bwana.

**Miriam Katana:**

**Translator:** Kwa hivyo ile mahari yule bibi hatairegesha kwa ule Bwana na tena ile mali waliopata wakiwa bibi na Bwana, igawanywe katikati.

**Miriam Katana**

**Translator:** Kwa hivyo, ikiwa watoto bado ni wadogo, ule Bwana asomeshe wakifika umri ambao wanaweza kujiamlia, wataamua wataenda kwa baba ama kwa mama.

**Miriam Katana**:

**Translator:** Twaona wakati mwingine katika mila zetu Bwana akifa yule bibi itabidi aolewe na kakake yule aliyekufa.

**Miriam Katana:**

**Translator:** Kwa hivyo ile mali yote ambayo imeachwa na yule Bwana yule kakake atachukua pamoja na yule bibi, yote atarithi.

**Miriam Katana:**

**Translator:** Kwa hivyo, ule Bwana ambaye amemrithi huyu, ataangalia wale watoto wake tu, wale watoto wa marehemu watawachwa wapate shida na yule mamake.

**Mariam Katana:**

**Translator:** Kwa hivyo, maoni ni kwamba bwanake akifa, bibi asirithiwe na mtu yeyote na ile mali ibaki kwa yule bibi ili aendeleze maisha ya watoto wake na yeye mwenyewe. Asanteni.

**Com. Riunga Raiji:** Asante sana mama Mariam, ungeona labda utaona baadaye kwa gazeti ya leo korti imeamua kwamba ndoa ikivunjika, mwanamke na mwamme ni lazima wagawanye mali ambayo walipata wakati walikuwa wameoana. Sasa tuko na Renson Gunga. Renson Karibu.

**Renson Gunga:** Basi mengi yameongewa lakini nitaongea kidogo tuu, kuhuzu Rais akishastahafu baadaya ya muda wake wa kuwa ofisini, ningeonelea kuwa, ile Katiba, yule Rais asiweze kupewa pension akiwa ataeendelea kuwa kama mwenyekiti wa chama fulani. Ikiwa ata-retire politics, he can be entitled to ka-pension, lakini ikiwa atakuwa mwenyekiti wa chama fulani, apewe ile pension na chama chake, asiaribu pesa za serikali.

Oni lingine ni Katiba tunayoaandika, lazima ihakikishe ile fair distribution of resources. resilimali igawaywe kisawa, ziyo hapa tuna mmea kama huu mkilifi ambao unatokana na ule mti tunapata dawa ile ya kutibu upele, mashilingi, unakuta ile plant , inajengwa kule bara na mimea inapatika hapa Kenya, hiyo si sawa kabisa. Kwa hivyo pale kunapatikana ile raw mateials, ule mtambo ujengwe pale pale.

Rural access road: Unakuta sana sehemu nyingi za uko, hasa pwani, matunda ya wakulima yanaoza kwasababu bara-bara zimearibika asiangaliwe. Lakini sehemu za upande ule, bara-bara hata zaanikwa mahindi, bara-bara za lami. Kwa hivyo kuwe na ule ukawanyanji wa reselimali kisawa kabisa.

Tourist: Unakuta kuwa Coast Province ina watalii wengi ambao wanaingisa pesa katika Kenya, lakini badala ya kupanua hiki kiwanja tunacho hapa, kumejegwa kiwacha kingine cha kitaifa sehemu ambayo hata akuna watali kabisa. Hii serekali, hii Katiba ihakikishe kuwa, kule ambako kuna sehemu za income, ile plant ama resilimali yoyote ijengwe pale pale ili iweze

kunufaisha wale wakazi wa hiyo sehemu ile. Asanteni sana.

**Com. Riunga Raiji:** Asante sana kwa kuangalia mambo ya saa, sasa tuko na Bwana Ibrahim Unda. Karibu Mzee.

**Ibrahim Uda:**

**Translator:** Mimi nina neno moja tu si mengi maanake kumekuwa na kulaliwa kwa miaka mengi sana.

**Ibrahim Uda:**

**Translator:** Kitu cha kwanza kabisa ni kwamba pwani tumeachwa. Pwani imeachwa kivipi? Watu wengine wana mifirenji paka kwa nyumba zao huku hakuna.

**Ibrahim Uda:**

**Translator:** Kitu kingine ambacho kinatuumiza zaidi ni barabara zetu za mashambani, ziko katika hali mbaya na hatengenezwi.

**Ibrahim Uda**:

**Translator:** Kwa hivyo tunaumia sana kwa sababu ya haya mambo. Kwa hivyo wakati mwingine msaada uletwa huko kwetu unapatiwa tu mkebe mdogo tuu wa chakula, sasa mkebe uleutatosha familia kubwa. kwa hivyo pia hiyo inatuumiza sana.

**Ibrahim Uda:**

**Translator:** Pwani pia imelaliwa sana upande wa mashamba. Sasa zote sisi ni ma-squater tu.

**Ibrahim Uda**:

**Translator:** Mimi nina shamba nilipata nikafukuzwa sababu mimi inasemekana ni sqauter.

**Ibrahim Uda:**

**Translator:** Hiyo shamba inasemekana kwamba ilipatiwa Bwana Mulinge, tukafukuzwa zote. Palikuwa na minazi mingi akaiacha pale pale,

**Ibrahim Uda:**

**Translator:** hekari ishirini na sita za minazi, akapokonywa na Bwana Mulinge.

**Ibrahim Uda**:

**Translator:** Sasa amebaki hivyo, hana chochote.

**Ibrahim Uda:**

**Translator**: Kwa hivyo hii ndio serikali ama serikali iko uko na huko akuna serikali.

**Ibrahim Uda:**

**Translator:** Hii uhuru ulipatikana kule juu ama hata pwani tulipata uhuru.

**Ibrahim Uda:**

**Translator:** Kama uhuru uko kule juu, basi tupelekeni kule na sisi tupate matunda ya uhuru, tule.

**Ibrahim Uda:**

**Translator:** Tatizo kubwa ni mashamba, washihiri wamechukua mashamba makubwa, umepikwa soroveya, yaan survey, ukishika hivi unaapiwa usiende huku, huku si kwako, yeye ana shamba lake amelitetea paka dakika ya mwisho, DC, DO wakasema wajisumbua wewe. Hii mali ni ya warabu, sio yako, na shamba na hilo liko pale Mtangani, hekari saba.

**Ibrahim Uda:**

**Translator:** Asema shamba lake bado liko pale pale, alifukuzwa kitambo lakini yuko pale tu kimapavu. Lakini kila siku ni fujo, kwasababu ya hilo shamba.

**Ibrahim Uda**:

**Translator:** Hiyo shamba alirithi kutoka kwa baba yake, babake alipatiwa na mzee mwingine mshihiri anatwa Abdulahi, sasa watoto, wa Abdulahi ndio wanampatia shida huyu, na ile shamba ilipatiwa babake na akairithi kutoka kwa babake huyu. Kwa hivyo serikali iangalie sana upande wa mashamba, haza upande huu wa pwani. Natitimia sana.

**Ibrahim Uda:**

**Translator:** Kwa hivyo ukishika shamba kidogo unaambiwa haya aachana nayo, hiyo ni mali ya serikali, hiyo ni malali ya serikali siyo ya babako.

**Ibrahim Uda:**

**Translator:** Title Deeds inasemekana zilikuja na hasitolewi kwa watu, hizo ambazo ziko Kilifi, ukienda Kilifi, ukitaka Title Deed yako unaambiwa uleta pesa, je ikiwa mimi sina pesa, ndio nitafanya nini?

**Ibrahim Uda:**

**Translator:** Hiyo shamba ndio nitapata ama ndio litaenda. Tumeajana kwa hivyo hayo ndiyo yangu ni machache lakini yanatuumiza.

**Com. Riunga Raiji:** Asante sana mzee, tuko na Johnson Mtenge, karibu Bwana Johnson? Karibu Bwana Johnson.

**Johnson Mtege:** Asanteni sana wakubwa na wadogo. Mimi sina mengi kwasababu mengi yamezungumzwa isipokuwa nasisitisa habari ya hapa ma-Subchief, Chiefs na DO. Imesemekana kuwa pengine Sub-chief hana kazi yoyote isipokuwa Headman na Chief na huyo Chief awe na muda, alafu akiwa anategeleza mambo mazuri achaguliwe tena. Lakini mimi naomba serikali, au pendekezo langu hawa ma-Chief ambao watabaki na ma-headman, awe sasawa na DO, kwasababu DO, ni mtu ambaye anapata transfar. Chief apate transfer kama DO. Lakini ule uhelegefu unweza kuwa chief yuko hapa hapa saa ingine mziwa lala, basi atakuwa hivyo hivyo paka hiyo miaka hiyo. Lakini akienda kule ambako kuna maendeleo, kadri vile anagwenda, atahakikisha maendelo ya huko ambayo huko ambako nimechaguliwa na huku ni zingine. Paka akirudi kule, anamaoni mengi ambayo atawakilisha upande wake. Hapo hapo nyumbani mbapo amechaguliwa. Asanteni sana.

**Com. Riunga Raiji:** Asante kwa hayo maoni sasa tuko na Kazungu Yaa. Karibu.

**Kazungu Yaa: Spoke in Kigiriama**

**Translator:** Mimi sina mengi nikutoa shukurani kwa nyote mlio kuja, tuwe na moyo mmoja maanake tumetoka mbali, tulitawaliwa na wakoloni baadaya ndiyo tukapata uhuru.

**Kazungu Yaa:**

**Translator:** Kwa hivyo mimi ningetaka hii Katiba ambayo inategenezwa sasa iwe ni Katiba iwekwe mzuri kabisa na tuijue sisi wenyewe.

**Kazungu Yaa:**

**Translator:** Ni kweli tulipata uhuru lakini utaona mambo mengine upande wa juu yako tofauti na mambo ya uko.

**Kazungu Yaa:**

**Translator:** Utaona sisi tuna watoto wetu wanasoma wanapita, wanahitimu vizuri, wanaweza kuwa Ma-DO, PC, lakini ajabu ni kwamba, wale ma-DO tuko nawo ni wageni saa zote hatujapatiwa mtu wetu sisi, na watoto wetu tuko nao.

**Kazungu Yaa:**

**Translator:** Kwa hivyo mji ambao unaongozwa na mgeni uko tofauti huo, hauendelei vizuri.

**Kazungu Yaa:**

**Translator:** Kwa hivyo ni vizuri ikiwa mtu anayetoka huku ndiye anapatiwa cheo kama vile cha DO, maanake yule ndiye anajua matatizo ya huku, ya watu na anajua watu, familia na kila kitu, lakini mgeni analetwa hapa, hajui matatizo wala chochote, yeye ni kuangalia watu tuu, nahajali maanake si kwao, hataleta maeendeleo maanake sio kwao. Ni hayo tu.

**Com. Riunga Raiji:** Asanta sana, Bwana Safari Katenge, karibu.

**Safari Katenge:** Mimi naunga mkono kwa yale yaliyo semwa na wenzangu. Ni hayo tu.

**Com. Riunga Raiji:** Harrison Kahindi, tuko na mtu anayeitwa Harrison Kahindi, labda ametoka kidogo, Charo Yaa, Karisa Yaa, inaonekana labda wametoka kidogo watarudi. Charo Menza, Karibu.

**Charo Menza: Spoke in Kigiriama.**

**Translator:** Ukiwa ni mgonjwa na ukienda kwa daktari, huhakikishe kwamba umepatiwa madawa ya ule ugonjwa ili uwe sasa na wale wazima.

**Charo Menza:**

**Translator**: Kwa hivyo yale tuliyosema yawe yasihishie hapa, yaende huko na yakasikiswe na yafanywe kazi.

**Charo Menza:**

**Translator**: Kwa hivyo ningeomba ni maoni yangu ni kwamba ikiwa ni hospitali, ikiwa ni mashule, yajengwe kila sehemu ya Kenya ili maendeleo yawe sawa sawa Kenya mzima.

**Charo Menza:**

**Traslator:** Ikiwa mnasema kwamba tulipa uhuru, mbona sisi wengine tumekonda na wengine wana matumbo makubwa hapa.

**Charo Menza:**

**Translator:** Kwa hivyo tuhakikishe kwamba serikali iwe ni ya kila mtu, si serikali tu iwe ya watu wachache, ikiwa ni matumbo zote, ikiwa ni kukonda zote.

**Charo Menza:**

**Translator:** Kwa hivyo tunaona kwamba tuna hawa ambao hawafanyi kazi yoyote lakini wao ndio wanopata lile jasho la watu wengine na hawafanyi lolote.

**Charo Mennza:**

**Translator:** Kwa hivyo utaona wakati wa kura mtu anakuja na mfuko mmoja wa unga na fungu la dagaa waliotoka Kisumu, unampatia kura na ndio yuanda kabisa.

**Charo Menza:**

**Translator:** Kwa hivyo tungependa yale maoni ambayo watu wote wametoa yatiliwe mkazo ili Kenye yetu isonge mbele.

**Charo Menza:**

**Translator:** Na hayo yangu tu.

**Com. Riunga Raiji:** Asante sana, Simon Wanje, karibu Simon.

**Simon Wanje:** Mimi sina mengi ya kuzungumza, kwa sababu mengi yamezungumzwa tayari. Ningependa tuchague viongozi wale ambao watatusikiza shida zetu na kusitatua. Ni hayo tu, sina mengi.

**Com. Runga Raiji:** Labda ningetaka kuwajulisha kwamba, wajibu wetu hapa ni kusikisa maoni. Hata kama imesemwa, kama ni maoni yako, usiwe naofu, sema yale tu ambayo unasikia mwenyewe ni lazima tuaandike, hata ukirudia, yale yalisemwa na mngine, kwa sababu kila mtu yuko na haki ya kusema, hata nyinyi nyote mkiwa na jambo moja, kila mtu aseme, kawasababu tunaandika na nyingine tuna tape record, tunachukua yote kama maoni ya watu wa hapa. Sasa ni Alfunzo C. Kazungu.

**Alfunzo C. Kazungu:** Asante sana Kamishna na wengine wote mbao mko hapa, nasema asante sana kupata nafasi ya kuzungumza kuhuzu hii Katiba. Jambo la kwanza ni sikitisho kubwa sana kuona hata ma-hospitali watu wanapata taabu, unaenda hospitalini, dawa zile ambazo ungepata, unaambiwa hapa dawa akuna, lakini ukienda upande wa nyuma huko kuna mashindano, mpaka dawa ile ya maana, unaampiwa songa upande wa bei, hiyo Katiba hapo ichangishe vizuri sana zaidi kwasababu hauwezi kupona na dawa ambazo zile simewekwa maji, na ile ambayo ni ya maana iko.

Pili, serikali tunayoitaji ni ya Majimbo, ili nasi rasilimali za pale kwenye jimbo, wawe wanaweza kusiangalia wao wenyewe. Kwasababu mtu wa mahali pengine akiwa ndiye anakuongoza, hajui shida za pale mahali, kwa mfano, mnazi ni kitu ambacho sisi wenyewe tunakidhamini na hutaona hakitiliwi mgazo kwa upande wa wagemaji, na hali huu ugema huna faida kwa sisi wenyewe wa hapa pwani. Kwa hakika kuna pesa nyingi zinazo potea kwa sababu ya mnazi, kuna mweye mnazi hulipa karo, hulipa ada, wa pili ni mgemaji, atalipa vile vile. Hi ni pesa ambazo zitaingia kwa huo mnazi ambazo zitaingia kwa hii serikali. Tukisema ule ukweli, leseni ya mwenye mnazi, leseni ya mgema, na mjuuzi, zote sinaingia mfuko wa serikali. Hapo inakuwa ni sawa kabisa na hizi pesa sinapotea kabisa kwa serikali lakini singe zaidia.

Mengi yamezungumzwa, ambayo ninayaunga mkono wale waliozungumza kuhuzu jimbo la pwani lina vitu vingi sana ambavyo hata tukiangalia hivi, tungepata faida. Ni muda mrefu sana hakujalimwa barabara huko. Barabara za kutoka hapa Malindi paka Voi huko, ni barabara ambayo kwa hakika ina faida sana kuuzu wa watalii na ingekuwa na lami ingekuwa bora zaidi. Lakini kimia, kama tungekuwa na sauti sisi watu wa pwani, ninahakika ingekuwa sasa hiyo barabara ingekuwa imewekwa lami.

Turudi hapo upande wa mashambani, kusema ukweli hospitali hakuna, na kama hospitali hakuna mtu ni mgonjwa, anapata shida kutoka uko ndani ndani, mama anataka kuzaa ni shida, akuna barabara ya kupeleka wakina mama hospitali mpaka Malindi. Na kutoka huko vile mnavyo kuona nyinyi wenyewe mpaka Malindi ni mbali. Kwa hivyo, tunaamini ya kwamba, kila mmoja akiwe mahali pake anamiliki yeye mwenyewe, hutimiza mambo yake pila matatizo, hata nyinyi mnajua hivyo. Kwa hivyo tafadhali, haya yanayo andikwa hapa, tena vile vile kwenya kuchunguza, wachunguze kwa makini kuona ni mahali gani inatimizwa, yale mnayo andika hapa vile vile yatimizwe, yasiwe yameishia hapa hapa.

Kama vile mnavyo ona, tamupa mfano mmjo, taraja lilikuwa limetolewa pesa ili lijengwe, ikaishia hapo hapo, na iliishia hapo hapo mpaka leo. Je, hiyo ni sawasawa? Nikuonyesha ya kwamba hakuna wenye gujunguza. Kama tungekuwa na wenye kujunguza, ingekuwa hilo barabara, hiyo daraja ingekamilika. Kwa hivyo tafadhalini, kila jimbo, lihakikishe kila mahali pake pana kamilishwa, na tena kila jimbo yoyote ambaye yuko kazini ahakikishe ile kazi inatimiswa. Wale wakubwa wasiwe wenye kuwajia makazi wadogo wao, aende kufanya mambo yake kule kando, hapana, kwasababu yule unamtuma kazi na hata yeye amekuwa bosi pale, badla ya kuwa yeye ameaja ile kazi yake ameingilia ya bosi sasa, wewe bosi waingilia mambo mengine yako pekee yake. Hiyo inafanya serikali mambo yanaaribika, kwa hivyo nitaka muongoze hapo kila jimbo yale yanayo andikwa tena wafanyikazi wale ma-boss wahakikishe kazi zao zinatimiswa. Sina mengi ni hayo machache.

**Com. Riunga Raiji:** Asante sana, huyo alikuwa ni Alfunso na sasa tuko na Bwana Chengo Mumba.

**Chengo Mumba:** Asanteni sasa kwa kunipa nafasi hii. Kwa niaba ya shirika ndogo la jamii kutoka Mgondoni.

Jambo la kwanza, wakati wa kuregebisha Katiba, basi maraia wahuzishwe. Uraia, sitasema mengi sana, ili mtu kuitwa raia wa Kenya, ni awe wazazi wa babu yake wamezaliwa hapa.

Usalama wa nchi: Usalama wa nchi ni haki uorodheshwe katika Katiba, wanajeshi wawe wana athibiwa kuligana na Katiba ya Kenya.

Rais asitaili kuwa amri jeshi mkuu: Hii ni kwasababu Rais anaweza kuwa na makosa fulani na mtu fulani, kwa hivyo ikiwa ni yeye pekee yake, kuamru jambo fulani lifanywe, kwa mara nyingine si vizuri, vizuri ni kuwe na watu ambao wanaweza kujatiliana ili jambo fulani lifanyike, lakini si yeye pekee yake akiseme kitu fulani kifanyike, basi kifanyike. Kwasababu yeye pia ni mwanadamu na inaweza kuwa mara nyingine ana makosa fulani kwenye akili yake, kwa hivyo akiamua kitu hata kama ni kibaya kwasababu yeye amesema, amesema. Hiyo ndio hatutaki, tunasema kitu kikifaywe kiwe kimeshauriwa na watu wengi.

Basi Elimu: Tunataka elimu ya msingi iwe ya bure, kwasababu watu wengi ni masikini wameshindwa kulipia mambo mengi ya shule. Kwa hivyo ikiwa ni mtu kijitayarisha kusomesha mtoto wake, ni kuanzia shule ya upili. Lakini shule ya msingi iwe ya bure.

Alafu muundu wa serikali: Tunataka serikali ya Majimbo, tuwe na Rais kwa jimbo na wa serikali kuu. Kuwe na bunge la jimbo na bunge serikali kuu. Ni hayo sina mengi. Asanteni.

**Com. Riunga Raiji:** Asante sana, sasa tunamwita Bwana Emmanuel Nyache. Nafikiri kwasababu tuko na tape recorder hapa, ukija labda uanze na jina lako, ili liingie kwa tape recorder. Jina lako ndugu.

**Emmanuel Nyache:** Mimi ninaitwa Emannuel Nyache. Mimi sina mengi, kwanza hamjamboni.

**Comm:** Hatujambo.

**Emmanuel Nyache:** Mimi sina mengi, mengi yameelezwa na ule na kama ninaongezea machache kidogo. Sasa langu mimi ni upande wa mnazi, kama yuko Bwana hapa alizungumza maanake mnazi, maanake serikali hii kwa jumla imetuumiza sana upande wa mnazi, haiju kwamba huu mnazi ilikuwa ni mmoja wapo ambayo inafaidi watu wa pwani. Kwa mfano, wakati huu ni wakati wa njaa, au ukame katika sehemu hii yetu ya pwani, haza tujukue hapa Kakoneni, na kama haingekuwa si mnazi nafikiri ungekuja kuona watu wote ni mahiti hapa. Kwa sababu hapa kila mtu akitoka kule kwenye maduka kule sehemu za njini……..
kuna maduka, kuna shule, wote wametegemea mnazi kule njini. Hata hii serikali ya sasa tuliyo nayo, nafikiri, imeona ya kwamba mji wa pwani tunashiriki sana kwa kunywa tuu, la, sisi tunachukua kama ni kitu ambayo ni kama biashara.

Mnazi unatuzaidia kwa upande wa shule, pesa ndogo ndogo kwa upande wa shule, tunasaidiwa na pesa za mnazi. Mnazi inasaidia hata mpaka mahitaji ya nyumbani, kwa mfano kama chakula na mambo mengine mengi, hata upande wa nguo na kila kitu.

Mnazi unasaidia watu wasiyo na minazi kwa watu wasiyo na kazi, kwa upande wa vibarua kazi na mnazi unasaidia kama kwa mfano tajiri mwenye mnazi, nafaidika kutoka na mnazi kwasababu mahitaji yake yote yanatokana na mnazi.

Halafu iko yule mjuuzi naye pia vile vile, naye anafaidika kwa upande wa mnazi, kuna wengine ambao wana watoto shule, wanafaidika kwa upande wa mnazi. Kwa haya kuna munywaji naye, naye ni masikini, hatumdu kunywa beer, beer ni pesa nyingi, hii kitu mnazi ni kutu rahisi, kwa hivyo mtu yeyote ambaye anataka kustarehe, binadamu ni lazima apate sitarehe katika maisha yake, hakuna binadamu asiyekuwa na sitarehe. Ukae siku nyingine uburudike, kwa hivyo unakwenda kwa kitu kidogo, pesa ndogo unapata juba yako ya mnazi, unatosheka, unarudi nyumbani, unakwenda tulia. Lakini beer ni pesa nyingi, sasa tunauliza kitu kimoja ambacho tunauliza, ni kwa nini sasa kitu kama beer, beer ni ulevi, mnazi nao pia ni ulevi lakini sasa kwa nini beer anaruuziwa lakini mnazi inapikwa marufuku. Kwa hivyo sisi watu wa pwani tunalalamika sana, tumelalamika miaka na miaka, ni kama tumeonewa, tumenyanyaswa kwa miaka na miaka na miaka. Kwa hivyo langu mimi ni serekali tunayotaka sisi ni serekali ya Majimbo ili tuwe na uhuru kwa huu mnazi wetu. Asanteni sasa zaisha.

**Com. Ruiga Raiji:** Asante sana, sasa tutamwita Bwana Chege Mucheri.

**Chege Mucheri**: Ni asante sana kwa kufika hapa, kwasababu shida ya hapa, shida ni kubwa si kidogo hapa pwani. Ni kwasababu iko mambo mengi ya hali ya ardhi. Jina yangu mimi naitwa Chege Mucheri. Sisi tuko na shida kubwa hapa. Na shida ile iko ni hali ya hii ardhi, ni kwasababu tulikuwa tunaishi huko Malindi na nikaona mambo makubwa sana ya hali ya ardhi. Na mpaka sisi wenyewe huku tukapikania kwasababu tulikuja kunyanganywa ardhi zetu. Kwasababu watu wanatolewa huko mbali, wanaletwa pale, na huko iko wenyewe wenyenji wa hapa, wamejenga majumba zao huku, wamefanya mambo makubwa huku, wamezaliwa hapo hapo, baba wakazaa watoto, watoto wakazaa tena. Na hapo ni kwao. Sasa kukasemekana wewe uondoke hapo kwasababu hapo sio kwako. Hata watu wengi walisikia hali ya vita ya huko kwa sababu ya ardhi kwasababu ya kuuswe. Na mwenye hapo anafukuswa. Anafukuswa aende wapi? na ni mwenyeji wa hapo.

Pia, ni hali ya hii mnazi: Nitaongea hali ya mnazi, sisi hapa kwetu pwani hakuna kitu kingine tunategemea. Hata tukipanda mahindi hiyo ni yakula, tunakula, lakini hii mnazi inabeba mambo mengi, na hii mnazi moja, hii onaona mti moja inaleta pesa nyingi. Hii inaleta kujenga manyumba, makuti iko, mafuta iko, kila kitu kiko. Haya hata pombe iko hata kama mimi situmii, pombe iko hapo ndani. Na sasa kukasemekana hii pombe ni haramu, na hiyo ndio inasaidia sisi hapa hapa. Sisi hatuna kazi nyingine tunaendelea nayo, tunategemea hiyo, kwa sababu hapa pwani ndiyo kahawa yetu na ndio majani yetu. Pia hata mimi nilizunguga sana huku na huku hata kule bara, mimi ni mtu wa bara, lakini mimi ni mtu wa hapa pwani, mimi nilikaribishwa hapa na nikanunua shamba langu hapa. Na mimi ni mtu wa hapa kwasababu sina makao huko, makao yangu ni hapa pwani kwa sababu mimi ni mtu wa hapa sasa. Na lazima hata mimi nitetee hali ya ardhi na ya kila kitu.

Pia, mimi nimeona mambo mengi sana huku, hali ya hospitali: Ukienda kwa hospitali huko, wewe huna chochote, unaambiwa wewe keti hapo, nikaouna wengine wanakuja wanatia mfukoni, anaongana pale, lakini ule ule mama, au ni mzee ako hapo tuu. Daktari anapita hapo akiwaangalia na anapita tuu. Ni kuonekana yule hana maana, yule anatoa pesa yeye ndiye anamaana. Iyo tunataka iondolewe.

Pia iko shida, ikiwa mtu hawezi kuongosa yule tuna tumemchagua, aongoze kwa njia mbaya, aondolewe tulete mwingeni. Ni kwasababu ni watu wengi wamesoma kabisa, mimi ninazungumza hali ya Kenya nzima, sikusema hapa peeke yake. Tuwe na uhuru kwasababu tunataka sisi tuwe nao. Ni kwasababu wengine wako na uhuru na wengine hawana. Yule hana kitu hana na uhuru. Anakonda tuu, ananyanyaswa, wengine hawana chochote. Ukienda office-ni kwa shida fulani, Kenya nzima mimi nilizunguka na nikajionea. Mpaka unaambiwa wewe unataka nini, leta kitu hapa. Hata checki na mshahara wake, yule mtu masikini anarudi, anaenda kukaa na shida yake. Na sisi ni binadamu wote. Na tumechagua hawa watetee sisi, na wasimamie sisi kwa njia ya amani na mali, masikini, tajiri, tuangaliwe. Lakini zaidi masikini wanaumia.

Pia tunataka hali hii yetu ya ardhi, tupatiwe Title Deed. Kwa sababu unakuja unaulizwa hii shamba ni yako, wapi karatasi, ule

mtu anaonewa, ataenda wapi na ameishi hapo miaka na miaka. Kwa hivyo sisi hatutaki, watu watoka huku kuingilia wenyeji sasa. Ikiwa anakuja aone mwenyeji, si kutolewa huku na kuingiswa huku, wazungumze na mwenyeji, wakielewana, amuuzie lakini hapa iko shida kubwa. Kwa hivyo, iko shida kubwa kisisi na hiyo hatutaki mtu kunyanganywe ardhi yake. Kwasababu tunataka kama ni mtu ameelewana na mwenyewe, muelewane na auziwe na atakuwa mtu wa hapo. Kwa hivyo, tunataka hii masamba yetu tupatiwe Title Deed. Kwasababu Title Deed ndicho kitu mhimu na ndiyo itatuzaidia.

Pia ya pili iko shida, na hiyo tena shida ni kubwa, ndio mimi ninasema nitazungumza bila wasi wasi kwasababu shida ni hiyo kabisa. Utaweza lima shamba lako, ukilima shamba yako, mali yako yote inaharibiwa na ng'ombe na mbuzi. Ukienda basi kwa wale agriculture, hakuna kitu wanakusaidia, ukashindwa utaelekea wapi. Hiyo nayo, iangaliwe hali ya mali kama hiyo kuharibiwa, watu wote wanalia. Unapanda mhogo wako kwa shamba lako, na wale wako na shamba zao, kwa nini arithi kwao anaenda kurithi mali ya wale wengine kwa mashamba yao.

Kama ni mhogo umepanda, hutaipata tena, hata kama ukitoa maelfu. Shida ni nyingi. Shida ni nyingi. Mimi nitamalizia hapo

**Com. Riunga Raiji:** Asante sana Bwana Mucheri, yule mwingine ni Alfred Ngala.

**Alfred Ngala:** Kwa jina naitwa Alfred Ngala, mimi naunga mkono kwanza serikali ya Majimbo. Na ningependa pia serikali izimamie mambo ya elimu, afya na mambo ya maji. Kisha tunataka serikali ambayo haita zungumza uwongo kama vile serikali ya sasa ilisema kuwa, elimu ni bure, halafu wakuleta choki, wakuleta chochote. Sasa hiyo ni uwongo, sisi tunataka serikali ya kuzungumza ukweli, ikisema elimu ni bure, ilete vifaa na kila kitu.

Halafu mambo ya ardhi: Ningependelea wale watu wa kupima, wa survey wakija wakipima ardhi ya mtu, aniambiye baadaya miezi sita niwe nimepata Title Deed, yaani Title Deed siwe na muda kuwa hivi nimekupimia shamba lako, lakini baadaya ya miezi sita utapata Title Deed yako, siyo miaka elfu moja.

Kuhuzu uchaguzi: Watu kama ma-Subchief, ma-Chief, ma-DO na ma-DC, ni watu ambao serikali inatumia pesa mengi sana kuwaelimisha watu kama hawa, kwasababu hupelekwa Colleges, sasa tukisema watu kama hawa wapigiwe kura, itakuwa sasa baadaya miaka mitano serikali inakaramia tena kuelimisha tena mtu mwingine. Kwa hivyo tuwe na transfers ya ma-Chief, kama hafanyi kazi pengine itakuwa ni kwasababu pale ni kwao. Apelekwe mahali mwingine, pengine huenda kapatilika, kuwe na transfers likini sio kura. Tukiwapikia kura serikali yetu itakarimika siku zote, kwasababu ielimishe mtu huyu, baadaya miaka mitano waelimishe mtu mwingine, tutakuwa tunaribu pesa za uma. Ni hayo tu. Asanteni.

**Com. Riunga Raiji:** Asante sana. Sasa tuko na Johnson Gombe, Johnson Karibu.

**Johnson Gombe:** Kwa jina langu naitwa Johnson Gombe. Mimi ya kwanza nasisitiza serikali ya Majimbo. Kitu tunacho

pigania zaidi ni kwa vile askari wale wanatoka bara, hawajali masilahai yetu. Kwasababu wakati mwingine anakushika pengine unakunywa mnazi kidogo, nakuchukua kama mnyama kwasababu hakujui unatoka wapi wala unaenda wapi. Sasa watu kama wale, kama pengine atakuwa mtoto wangu ama atakuwa anachaguliwa hapa ananijua huwa hatanifanyia kitendo kila kwasababu ananijua mimi ni nani, na yeye pia alisomeshwa na ule ule mnazi.

Jambo la pili ni habari hii ya mnazi: Mimi naona ajabu sana, kwamba hata kwenye vitabu vya korani na bibilia havikuhalalisha pombe lakini utakuta kama miraa ni kitu ambacho nacho hali yake ni ile ile lakini kinahalalishwa. Na huko kwetu sisi pombe ile ya mnazi haihalalishwi. Sasa mimi nataka hapa hapo tuone kwamba kile kinachotoka kwa mwenzako kiwe kibaya au kizuri, lakini kule kule kinakotoka, kuliko kujukua kitu cha mwenzako unakidharau kwamba hiyo ni kitu mbaya, na watu wengi sana hata ukiwaona hivi, wengi sana, wale ambao wanaringa, kusema hivi na hivi wote pia wanakunywa mnazi. Mimi naomba serikali hii yetu ya majimbo, kama pengine itakuwa hivyo iwe itaangalia mambo yale kwasababu sisi resources zetu nyingi zinatokana na huo mnazi. Mwanadamu anaishi na kile chake. Serikali tunataka kama Commissioners wote wale ambao wako hapa kwa wakati huu wajaribu kuona kwamba wanachukua haya maoni ya watu wa pwani na vilio vyao wahakikishe kwamba vitafikishwa kule. Kule inavyotakikana. Mimi sana mengi. Asanteni.

**Com. Riunga Raiji:** Asante sana, sasa tuko na Joseph Katenge, yuko? Okey, Gatana Kisau, Joseph Katenge, Okey.

**Joseph Katenge:** Mimi naunga mkono katika haya mwaswali yote yamezungumzwa hapa, jina naitwa Joseph Katenge. Kwa hivyo sina mengi yangu na hayo tu naunga mkono.

**Com. Riunga Raiji:** Asante sana, Kisau yuko karibu? Katana Kisau, hayuko? Karibu.

**Katana Kisau:** Mimi naitwa Katana Kisau, mimi sina mengi, yale yaliyo somwa yawe hayo hayo.

**Com. Riunga Raiji**: Asante sana. Simon Kapombe, Simom Kapombe? Karibu Bwana.

**Simo Kapombe**: Jina langu naitwa Simon Kapombe, nimekuja kwa kuongea neno moja tu. Neno ni kwamba tumepata viongozi wetu ambao wanaendelea kutuongoza lakini hata hivyo malalamishi yangu ni kwamba, upande wa ki-location, tunapata kuona ya kwamba, mtu anaweza kuwa ana maneno yake ambayo yamemkosokea na mwenzake namna ile, hatua haiwezi kuchukulika mpaka pesa zitoke, hata kama ni wewe ambaye umeonewa na mwenziyo. Kwa hivyo tumepata kuona ya kwamba, pesa ndio imeshika ushukani, hatuwesi kuona uongozi mzuri ama uhamusi mzuri mbao ungetufa upande wa ma-Chief. Kwa hivyo, upande wa pesa, tumekaliwa sana. Kwasababu ya kwamba hutaweza kuchukuliwa hatua ambayo ingekuzaidia mpaka uwe una shilingi. Na tunapata kuona wengine hawana pesa, wengine pesa ni kidogo kwao, hawezi, akifika mahali pale, akiambiwa atoe pesa, itabidi arudi na yale mambo ayaache vile vile na yanaendelea kumuumiza. Kwa hivyo tunaona ya kwamba ingelikuwa bora kama serekali ingechukulia hapa mahali pa huyu mtu, hawa watu ambao ni machief wanapata

mishahara yao wakatosheka nayo. Sina zaidi ni hayo tu.

**Com. Riunga Raiji:** Asante sana, Mwaringa Mbia.

**Benson Mwaringa Mbia**: Mimi natoa shukurani zangu kwa kikao hiki. Jina langu naitwa Benson Mwaringa Mbia kutoka Makobeni. Mimi naunga mkono majimbo na utawala wa vyama vingi. Si majimbo tuu, pali utawala wa vyama vingi. Tumechoka kudhulumiwa na serikali na chama kimoja, kuonewa na kutanganywa, kukandamizwa na haki zetu, hasa hapa pwani, hatuna haki kabisa. Chama kimoja kina ukabila, na u-dictator haswa. Maongozi yake ya chama kimoja huwa ni ya ukoo mmoja, haswa kwa mimi pengine nichukue uhadamu wa uongozi saa hii, nitaangalia wale ndugu zangu kwanza, ama watu wangu kwanza, nitasahu wote wale, lakini kukiwa kuna vyama vingi na hii mambo ya majimbo hakutakuwa na hiyo jambo. Ikiwa ni utawala wa chama kimoja, mtu atahakikisha kwanza ile jamii yake ama familia yake ndio imetajirika hivyo kwanza. Iwe ina wikaa ndio wengine baadaye. Na ukijaribu kuongea huo ukweli hata unaweza kutafutwa hata kama ni majambazi lakini umalizwe kusudi hiyo kitu usitoe mkia tena, ukatoa mdomo tena ukazikika unasema nini. Huo sio uhuru bali huo ni utumwa.

Watu wetu hutiwa hata jela bila sababu za maana, utakuta mtu amewekwa korogoroni kwasababu ya pengine ni maneno ama kwasababu ya chama tuu, anawekwe huko ndani na hata funguliwa hata haraka, hata akiwa na familia yake, hawata wajali,hata akifa huko. Zamani ama mwanzoni, tulipokuwa na chama cha KADU, kama hatungezisitiza haya mambo ya kuungana, nafikiri watu wa pwani tungekuwa tumepiga hatuha kubwa sana. Lakini sasa tulipoungana na KANU nafikiri hatujafanyiwa lolote la kusema hii ni la maana la pwani, isipokuwa ni kunyanyazwa tu. Hebu ni faida gani tumeipata kutoka tulipo anza kujinyakulia uhuru mpaka sasa? Tunaweza kuhesabu ni faida gani watu wa pwani tumepata na kujifunia?

Sasa kila jimbo liwe na chama chake. Kwa upanade wangu, mimi ningependa kila jimbo liunge chama chake. Si chama kiwe kimoja. Majimbo yaweko lakini na kila chama chake. Kuwe na serikali kuu. Serikali kuu si iwe ya mtu moja. Huyu atakayeshika serikali kuu awe anafanya kuchaguliwa na haya majimbo. Na ihende kwa zamu. Zamu hii ni atoke pwani, zamu lingine atoke mkoa mwingine.

Upande wa viongozi kama Ma-DC, Ma-DO na hata ma-Chief wetu, kwa upande wetu, maana sio peeke yangu nimeandika hii barua, ni watu wengi, kwa hivyo kwa upande wetu, tunaonelea, wafanye kuchaguliwa kwa kura hawa watu. Kwasababu bila kufanya hivyo na pengine kama huyu mtu ametoka Nairobi na amekuja hapa, huyu mtu hawezi kujua matatizo ya watu wa hapa, mpaka kwanza ashirikiane na watu ndio labda pengine ajielimishe taabu za hapa. Nikichukulia mfano, kama hivi juzi nilisikia kwamba huku DO tutaletwa Lango Mbaya. Hatujamuuona huyo, nasikia tuu alikuja kuangalia hiyo nyumba halafu akaenda zake Malindi. Saa hii anaishi malindi badala ya kuishi lango baya. Hiyo kitu nimeisikia.

Jambo lingine, ni kuhusu mapato ya majimbo: Pengine kama jimbo fulani litakuwa lina mapato zaidi, kwa upande wetu, ingekuwa ni vizuri, izaidie ile majimbo mengine labda pengine itakuwa ni masikini na hayawezi kujiendeleza. Lakini mpaka

muuone nyinyi wenyewe pia memejitosheleza. Tuseme katika mapato yanayo batika yanaweza kutolewa 25% ikapatiwe lile jimbo lingine na hiyo 75% ikabaki ni ya jimbo hilo lao.

Elimu: Elimu ningeomba ziwe sawa, kwasababu hapa kwetu sijue kama nikulaniwa ama ni vipi. Elimu hapa ni shida tuu. Utakuta hapa shule nyingine hata ni udongo ama chini ya mwembe, ukienda baara hata kuna simu hata stima iko, sijui kama serikali ni tofauti kule na hapa ama ni vipi.

Halafu kuna wale ambao husunguka mashule wakiangali kugagua mwenendo wa shule, wale watu naona hatuna hapa. Hapa kwetu pwani hatuna. Kwasababu unaweza kuwa unasafiri, kama mimi ninayefanya kazi kule Malindi, nikisafiri kila siku nikienda, lazima nikutane na mwalimu anaenda huko Malindi, huyu mtu anaenda kufanya nini na sijui wakati hule wa kazi huwa na kazi gani. Kwasababu yeye anaruhusa ya miezi mitatu kila mwaka, kila mwaka nakaa miezi mitatu, off zake yaan leave zake, mimi nitapata mwezi mmoja kwa mwaka, yeye kisha hataenda shule, atakuwa mtu wa njia tuu akienda Malindi kule mara amefanya mambo yake, watoto kule wameenda wamekosa mwalimu, na ukiangalia hata wanashirikiana na huyo headmaster. Na hii saa nyingine nayo inaweza kuleta pia watoto kukosa kupita vizuri somo lake kwasababu hatahudhuria zaidi katika ile shule. Yeye ni mtu wa masafari tuu na kazi zake mwenyewe. Kama kungekuwa kuna hawa wachanguzi wa shule, hii kitu haingeteteka.

Mishahara ya viongozi wetu kama hawa wambunge hivi, kwa upande wangu iko juu zana. Utakuta mtu anafanya kazi la shamba, kama shambaa hizo za kahawa, unakuta mtu hata anapata hata elfu mbili, mbunge anapatia million, labda billion moja, ukichanganya na marupurupu yake, vile ananyang'anya yeye, utaona ameishi mwezi mmoja, miezi miwili, amenunua gari. Sisi unafanya kazi, hata wewe hufe, mtoto wako hapo hapo na hutakuwa ha na basikeli kwa nyumba.

Kwa hivyo kwa upande wetu, tungependa ma-hospitali, haya ma-hospitali makubwa, kila jimbo liwe na hospitali yake kubwa na kama pengine ni upande wa hivi vioo vikuu kuwa na chuo kuu katika kila jimbo. Si viwekwe tu Nairobi ama viwekwe pahali pengine pa watu wa bara na hapa pwani hata moja hakuna, kwa hivyo hiyo kitu nayo ingaliwe. Tujisimamie wenyewe katika kila masomo na kama ni walimu, wawe wanabadilishwa jimbo hili, anawesa akaenda kufanya kazi jimbo lile lingine na tukibadilishana mawazo, tuwe na ile competition ya jimbo hili na jimbo lile ilikusudi watoto wetu waweze kufanya vizuri.

Kwa upande wa mamlaka ya Rais: Hii nimefanya tuu kuambiwa, sasa lakini sijui ameamini nini huyu Bwana, lakini amesema ipunguswe, u-dictator, ni mwingi hapo. Na upande wa ma-squatter, squatter awe ni yule mtu ambaye atatoka hapa kwenda kufanya kazi pengine jimbo lingine. Hatufukuzi watu wa bara no, watu wa bara waweko kwasababu hata kuna nyumba za kupangisha zinataka watu kama hao ni lazima tupate risiki kutoka kwao. Lakini wawe wanajukina kwamba hawa si wakwetu hapa na wasipatiwe hata Title Deeds. Na wakiusiwa kama ni shamba ama ni ardhi, wausiwe tu kwa muda ama wakotishe lakini si kwamba wanausiwa kabisa-kabisa ili kusudi wakati wa kuwa amefinywa hapo ama amechoka hapa, anaweza akaaja hiyo ardhi hapa na akarudi kwao. Vyeti vya kumiliki hizo mashamba vipatiwe tu wale wenye jimbo hilo lakini si katika jimbo

lingine mtu anafanya kuambiwa kuna kipande chako cha ardhi kiko pwani mahali fulani nienda ukajugue hiyo ni ardhi yako. Hiyo ipatiwe tu wale wenye hiyo jimbo lakini si mtu wa kutoka jimbo lingine. Kwasababu ya kuhebusha mambo ya vita vya mbeleni pengine.

Misaada ya kigeni, iliingia: Hii misaada kwa vile kutakuwa na serikali kuu, hawa wanaweza wakaa na wakagawanyia kila jimbo sawasawa.

Watoto wetu pia wapatiwe uhuru, kwasababu wasidharauliwe kwa vile ni watoto. Uhuru si kwamba awachiwe kila kitu, lakini sasa utakuta kuna wakati mwingine mwalimu anaweza kukosana na mtoto akiwa ni kisasi hata pengine hakina maana, wakawa pengine wanatafuta pengine hata msichana, huyu ni mwalimu anaweza kuwa anatafuta msichana hapo, akawa anashindana tuu na mtoto, unaona, mpaka sasa wakawa wana ilekuwindana, ukasikia mtoto amepiga mwalimu ama mwalimu amevamiwa na watoto hiyo nayo nataka pia iangaliwe.

Uwikisaji: Hii kuikisa, kwa upande wangu sioni ni mzuri kwasababu, kama Malindi hapa, mimi nilikuwa na vipanda vyangu vimebomolewa vyote na Mnispa na pale mahali ambapo wameshabomoa, hawakupafanya kitu, wakachukua mabati yangu, wakatoboatoboa wakapeleka huko, sasa nikafikiria kutajengwa kitu ya maana, hapo mahali bado hivyo hata sasa……….

Ulaya huko hata kumejaa, watu wanajenga juu ya wengine. Hapa kwetu bado kuna ardhi kubwa, vibarabara vyenyewe ni vidogo, hata kunaajwa space kubwa ambayo mtu anaweza kuweka kipanda chake, na ukimfunjia basi hata huyu mtu hujui atalala wapi, pengine hata ataibiwa na hata kesho mtoto wake ataenda sukuli hivyo? si hatabaki tu nyumbani kwa sababu hana kazi.

Na kuna mama zetu hapa, ambao wale akina mama wana kazi ya kutoa maboga hapa kwetu wakipeleka Malindi. Utakuta wameweka vitu vinaitwa cherberry pale, mtu analipa pesa pale, halafu tena Malindi pia ana-charge-wa vilevile. Huyu mtu kama ni mnazi wameenda nao kule, na hii pesa amenyan'ganywa hapa na kule nakwo anaeenda kulipishwa kitu ya juu, na ni kila siku, anapata faida gani mpaka ndio asomeshe huyu mtoto? Akichukua mtoto wake wa kike, pengine ameshauriwa na babake mchukue huyu upatie huyu, kwasababu tupate tusomeshe huyu mwingine, huyo mzee hata kama ni kufungwa atafungwa, kwasababu hana jambo la kufanya isipokuwa, amefanya hivi kwasababu asomeshe yule wa kiume, anajua huyu wa kiume ndio labda nitabaki naye hapa nyumbani. Na kama si hivyo, ingalikuwa hawa serikali kuonea hawa watu. Nafikiri hii elimu ingekuwa sawa kwa watu wote. Ni vile tu hatuna uwezo ndio labda utasikia wa-kiriama wana tabia labda pengine ya kuuza watoto wadogo, sio eti kwa kupenda kwetu, ni kwasababu ya umasikini umejaa na tunanyanyaswa na hiyo serikali.

Ndoa zetu, ile ndoa tunafunga, zitumishwe, hizi ndoa na kufatwa kwasababu siku hizi hata hasifatwi tena, lakini sasa siweze kufatwa. Kama kuna hizi mila, mila za unasikia pengine mtu fulani, wanawake labda pengine labda pengine wametairiwa kwa nguvu, hiki kitu inatokana kwa nini? Ni kwasababu labda pengine wale watu wameaja ile mila yao, wameingilia labda mila.

Zamani walikuwa labda wakiishi vizuri na walikuwa hata wakitahiriyana. Leo hii unataka wewe, wahige mfano wako ambao ule mfano wako, wameanza kuuana kwasababu ule mfano wako ambao hawauwezi na itabidi wakufwage wewe, kwa vile wewe ni mkubwa.

Lingine ni kuhusu hii pombe yetu ya mnazi: Mengi yamesemwa sana lakini kuongosea, hata mimi pia ningependa hiyo pombe iruhuziwe kwasababu tunateswa sisi tu huku, lakini hata ukishuka Nairobi pale stage, utakuta hata busa inauswa pale. Na hiyo pia inalewesha. Kwa nini hii yetu ukionekana hata afadhali uvujwe mkuu lakini sasa huhakikishi wewe hutarudia tena hiyo mnazi. Utakula nini? Utasomesa nini? Na hiyo ndio kahawa yetu. Miraa inaruusiwa na hata vitu vingine, hata si pombe ya busa pekee yake. Kuna pombe nyingine sijui inaitwa nini, kule bara, nimeenda hata nikaionja, hiyo pombe inaruhusiwa na inahuswa hivi hivi. Na sijui kwa nini huku kwetu ndio tunakandamiswa peeke yetu. Na tukihuliswa tunaambiwa hatujui kusoma labda, na sasa hata kama hatujui kusoma, kuna wangapi huko juu ambao hawajui kusoma na wamo serikali. Mimi ndugu yangu alikuwa kwa jeshi, na yule ambaye alikuwa akiwaongoza ni mtu ambaye hata kuzungumza kingereza hajui, na yeye ndiye yuko front line. Hii kitu namna ngani?

Kwa hivyo kwa kumalizia, Katiba yetu tunaomba iwe ya majimbo kwa chama, kila jimbo liwe linaweza kuwa na chama chake. Asanteni.

**Com. Riunga Raiji**: Okey asante sana, tafadhali upeane ile memorandum huko. Nafikiri sasa yule mwingene atakuwa Donald Mzomba. Karibu.

**Donald Mzomba:** Kwa jina naitwa Donald Mzomba, nitaanza kuzungumzia kuhusiana na hii pombe. Vile ambayo tumesima kutoka kitambo kuwa mnazi, hapa pwani ni kama cash crop. Ni kama vile kahawa, majani, pareto kutoka kule juu Lakini sasa hapa pwani, tunaumiswa na kitu kimoja kule bunge. Kuna kitu ambacho kinaitwa Coconut Act. Hiyo ikiondolewa, tunajua au tutakuwa na uhakika kuwa mnazi utakuwa unaweza kuhalilishwa. Lakini hiyo kama haitaondolewa, kila Karisa Maitha wamezungumza kule, wengi wemezungumza kuwa wanataka mnazi uhalalishwe, lakini Serikali hajafanya hivyo, tunaomba sana ile Coconut Act, iondolewe ili mnazi huhalalishwe na mpwani, aweze kufaidika kutoka kwa mnazi.

Pili nitazungumzia kuhuziana huwezo wa Rais. Huwezo wa Rais umekuwa mwingi sana, tunaona kuwa kulingana na mambo ya Judiciary, tunaona kuwa Raisi anaowezo wa maisha ya Mkenya, hiyo iondolewe, kwasababu tunaona Rais anauwezo kusema kuwa mtu fulani, baada ya kuwa judge amesema mtu huyo niawe-hanged. Rais akitia kidole ana-kuwa hanged. Hiyo iondolewe mara moja, kwasababu ya kuwa, ni Mungu peeke yake ndiye ambaye nauwezo na watu wake lakini sio bindamu kama mimi.

Kitu kingine ni kuusiana na vyama hivi vya siasa: Kuna ile hali ya kuwa naona kuwa toka kitambo, baadaya ya kura mtu akiwa ameshindwa, ana-defect, anaingia chama kingine, hiyo Katiba ilinde kuwa mtu akiwa ame-defect, asiruhusiwe kusimama kwa

kura. Kwasababu ya kuwa tunaona kuwa yeye ni wale binadamu wale wale, sisi ndizo ambao tumemkataa lakini sasa anoana kuwa pengine chama ambacho kina sifa sana sehemu fulani pengine ni shirikisho, kwa hivyo anaona kuwa nikiingia kwa shirikisho, itapata nguvu zaidi kwasababu ya kuwa, watu wengi kidogo huko, hatujaelimika kivile. Kwa hivyo, tunaona kuwa mtu akiingia kwa shirikisho, kwa sababu ya kuwa yeye ni diwani au yeye anataka ubunge, akiingia pahali kila mmoja atasema shirikisho, shirikisho, shirikisho. Kwa hivyo atapata mara moja. Kwa hivyo, hiyo iondolewe kuwa mtu asiwese ku-defect kuingia chama kingine.

La mwisho ni kuhuziana na hizi Commissions ambazo Rais huwa anasiunda kila mara. Tunaona kuwa zinaundwa, sinatumia pesa za umma, pesa zetu sisi ambazo tunafanya kazi, lakini sasa baadaya ya kuundwa hatupati majibu yote. Mfano mkubwa ni huu wa pompo lulu. Iliundwa hiyo Commission lakini hakuna jibu lolote ambalo Mwananchi alikuwa anatazamia kutoka jibu tuwese kufaida, tujue kuwa kulikuwa kuna nini na kulifanyika nini? Na wale ambao waliusika na ule mkasa, watapata nini? Lakini iliendelea mpaka ilipomalizika, ikawajwa hivyo hivyo.

Mwisho kabisa ni huu umilikaji wa mashamba, tunaona kuwa Rais ana uwezo wa beach plots. Akiwa kule juu anaweza kusema beach plot hii nimempatia mtu fulani, hiyo pia iondolewe. Kwa nini sisi watu wa Malindi tusipatiwe hizo beach plots? Wanapatiwa tuu watu wa kule juu, unaona katika mvuo wa bahari, ma-beach plots mengi yamepatiwa wale watu wakubwa, lakini hakuna hata mpwani yoyote ambaye anayo hata moja. Kuna hii mazuri land na haya mambo ya makanisa, kama tulivyosikia ni kuwa kuna hii kanisa la Angilikani, kuna act ambayo iliaandikwa 1902 na Charles Newton Eliot wakati huo. Hiyo ita-expire May, tunaomba kabisa, kuwa hiyo isiwe re-newed. Kwasababu ya kuwa watu wengi wamekaa kama ma-squatter. Kuna ardhi ambayo ina heka elfu moja mia tano, watu wako hapo lakini hawajapata vibali vya hiyo ardhi kwasababu inasemekana kuwa ni ya mwingereza au ni ya kanisa. Na kanisa haifanyi lolote, haja-develop ile ardhi. Kwa nini wale ambao wameketi pale miaka kumi, miaka ishirini wasipate vile vipali? Langu ni hilo.

**Com. Riunga Raiji:** Saumu Mapipo, huyo mama hayuko? Karibu mama. Okey sawa tu. Asha Omma. Patrisha Karisa, karibu mama.

**Patricia Karisa:** Hamjambo nyote

**Wananchi:** Hatujambo.

**Patricia Karisa:** Jina langu naitwa Patricia Karisa kutoka hapa Chilore. Mimi nilikuwa, kwanza nataka niuunge mkono kama tutapata hii serikali ya majimbo. Kwasababu naona mimi nikiipata hii serikali ya majimbo, nitafaidika, kwa sababu mimi ni mtu mzaliwa wa hapa pwani na tokea nilipozaliwa paka sasa, sijaona manufaa yoyote ya hii serikali yetu ya sasa.

Nikiiangalia kama vile wenzangu walivyo zungumza, kuhusu huu mti wa mnazi, huu mnazi ni mmea ambao wa pwani

walibarikiwa nao na Mungu. Na wenzetu wa bara nao wakabarikiwa na vyao lakini sisi watu watu wa pwani Mungu alitubarikia kweli, lakini sasa kukatokea Mungu mwengine ambaye anatufinya na ule mti wetu tulibarikiwa nao. Kwasababu huu mnazi nikihuangalia, mnazi huna faida nyingi sana. Kuna nazi, tukiuza uko nje tunapata pesa, tunasomesha watoto wetu, tukiangalia pia huu mnazi wenyewe ambao watu wanakunywa, watu wanalewa vibaya kwasababu, serikali hachukui hatua ya kuwa, tunaweka kama kituo, watu wakisema, wapeleke pale, wakauze ili, upelekwe nje watu wapate pesa kama vile watu wanavyo jenga dairy za maziwa. Si watu huku wana dairy za maziwa. Kama mnazi nao ungetengenezewa kama hivyo, tupeleke pale halafu nje, watu wangefaidika na huo mnazi. Lakini kwa vile serikali yetu, haitaki, kuchukulia hatua, na kusema kwamba tunataka watu wa pwani pia wafaidike, ndio maana tunaabiwa mnazi haruziwi saa zote. Ndio watu wanalewa, wanakatana visu, sababu ni hiyo, hakuna pahali pa kuhupeleka. Mimi sina mengi ni hayo tu na ninaomba yafike huko.

**Com. Riunga Raiji:** Asante mama hayo yote yatafika. Sasa Eunice Kahindi.

**Eunice Kahindi:** Mimi kwa majina yangu naitwa Eunice Kahindi, naunga mkono kwa serikali ya majimbo. Kwasababu ni muda mrefu ambao tumenyanyaswa, ukiaangalia hivi hata watoto wetu nao hawana pahali pakusoma, watoto wakipita kama hivi, huko ndiko ambako kuna Ntional Schools, huku tumeajiwa vibanda tu pekee.

Pili, ni upande wa kina mama, sisi tuna vyama, lakini hatujaona manufaa yeyote. Tukisikisa katika maredio, tunasikia wakina mama wamepatiwa mikibo, wamenunua mabasi, sisi tumebaki hivi hivi tu. Sijui kama hawao vingozi wetu ndio hawajui, sijui kama wale watu wa bara ndio ambao wanaelewa zaidi, naomba serikali iaangalie.

La tatu, tunaomba serikali hii ya majimbo akiwa Rais amechaguliwa, azitegemee jimbo moja. Angalau kila jimbo atembelee, ndipo atajuwa huku kuna shida gani.

La nine, tunaomba serikali ikiwa imechagua kama hawa ma-Chief, nimesikia wenzangu wanasema eti ma-chief wapatiwe transfar. Sasa ikiwa hapa amefanya vibaya, akienda huko kwa mwenzake nakwo akafanye hivyo vibaya? Akienda kule kwa mwenzake nagwo akafanye vibaya, akiwa hapa amefanya vibaya ni wajibu wa kuwacha ile kazi kwa maana atakuwa hajui kazi yake. Kwa maana wewe huta kwenda kwa Chief, umeshitaki, basi hawesi kuzungumza na watu, kuna wazee wangine wanasema basi utazungumza na wale. Nani? Nimekuja kwa Chief ama nimekuja kwa wazee? Kwa hivyo ninaomba, hii serikali ikiwa ni ya majimbo, kutafanyika kazi nzuri sana. Yangu ni hayo.

**Com. Riunga Raiji:** Asante sana mama. Douglas Mure, Douglas, nilikuwa nikifikiria nakuja, kama labda ametoka, Douglas yuko? Okey sawa. Charles Mlewa. Charles?

**Charles Mlewa:** Asante sana mimi naitwa Charles Mlewa. Mimi nitazungumzia kuhusu uongozi. Nataka serikali ambayo itakuwa ya Regional Government, ambayo ni ya majimbo na majimbo haya yatakuwa, tunataka serikali ya majimbo hiyo

Regional Government halafu kuwe kuna Prime Minister, katika Central Government, awe na ceremonial President. Hiyo ndiyo tunataka.

Na kuhusu mambo ya parties: Nataka vyama viwili, hatutaki hii vyama hivi ambavyo vimekuwa vikiandikiswa kila mara. Sasa kuna vyama karibu sabini, hatujui vinafanya kazi gani, kwa hivyo hatutaki watu wawe tawalishwa na hivi vyama vingi. Tunataka vyama vichache angalahu viwili, ili ikuwa kuna kile chama kinacho ongoza, kuwe kuna kile chama kingine ambacho ni opposition, ku-check vile wanavyofanya kazi.

Halafu jambo lingine, nataka nizungumze kuhusu hii mambo ya huku ya land: Hasa mashamba. Tumeona kwamba Title Deed sinachukua muda mrefu sana, na sinatolewa Nairobi. Nataka siwe decentralized, yaani siwe sinaweza fika up to Locational level na sichukue muda mfupi kama three months. Kila mtu awe na mpaka Title Deed. Na ile hali ya kwamba Title Deed katika ile degree ya President ya kutoa Title Deed kwa beaches, iwe katika Katiba, itiliwe makazo kwamba hawezi kutoa idhini ya kutoa Title Deed kutoka kule Nairobi, au ya President. Maanake sasa ile front row ya beach plots zote siku hizi inatolewa na President, ambayo sisi watu hata kama ilikuwa shamba lako, la beach plot, lakini huna haki ya kupewa Title Deed. Inapatiwa mtu mwingine aje a-develop. Kwanza wale wengine wanapewa Title Deed kutoka huko, hata hawajui ile plot yenyewe, hajui ile plot ambayo amepewa Title Deed. Ndiyo tunataka Title Deed ipewe katika Locational level kwa wale ambao wanaweza kuona ile shamba kujua ni shamba ya mtu fulani. Ili aweze kumiliki. Sio mtu ambaye yuko Nairobi, anafanya kuaambiwa hapa basi kuna beach, atoe Title Deed, sitolewe huku. Siwe na recommendation kutoka kwa location kwanza ndiyo mtu apatiwe Title Deed.

Kuna hili jambo la mnazi, kuna hiyo Act ambayo imesumbua sana pwani. Hiyo Coconut Act imesumbua muda mrefu sana, natunataka hii Katiba hii hiyo, hiyo Act iwe revoked kabisa. Kwasababu mnazi ni cash crop ya hapa na inamanufa, ina economical value ya hapa, kwa muda mrefu sana tumekuwa tukikosa hizo economic values. Maanake serikali kama inataka tuendelee, inaeza kuhakikisha kwamba mnazi katika mti mwenyewe huna faida, huna mambo mengi ambayo unaweza kutoa katitka mnazi. Siyo mnazi ule wa kunywa pekee yake. Bali mnazi kama mti cash crop, hizo ni products zingine, mnazi kunywa ni kama product tuu, lakini mnazi wenyewe kama mti cash crop una manufa mengi sana kwa mtu wa pwani. Kwa hivyo ikiondolewa ikiwa-revoked ile Act, tutahakikisha kwamba hata kama ni viwanda, tanaweza kuanzishwa hapa kusimamia jambo la mnazi. Kwa hivyo ni hayo machache. Asante

**Com. Riunga Raiji:** Joseph Sharo nafikiri, Joseph Charo Karibu.

**Joseph Charo**: Nina shukuru kwa kupata hii nafasi, mimi naitwa Joseph Charo kutoka Mkondoni na nimepewaa hii nakala ikiwa imechangiwa na watu ishirini na tano hivi. Lakini yote sitayasema hapa kwasababu mengi yametajwa na nikiaanza kusoma, yatachukua muda mrefu. Mimi ningependa hawa wa Mbuge wetu ambao tunawachagua, wabunge na Madiwani wakichaguliwa, wawe wana wahajibika na wale watu ambao wamechaguliwa, sio kuchaguliwa wabaki tuu kwa ma-town.

Wakitwa kwa mkutano wanakataa. Kuwe Katiba hii iwe inawachukulia hatua kali kabisa. Kuwe kuna uwezo fulani ambao tunaweza kuchukua sisi ambao tumemchagua hata kama ni kumchapa viboko ama tumishitaki.

Lingine ningependa hii Katiba iwe itatambua hizi mila ambazo zimepitwa na wakati. Sisi tumeishi na tuko hali ya kuangaziana, elimu imekuja hapa ikiwa imekuta watu wakiwa na tamaduni tofauti tofauti. Lakini hali ya kusoma, tunafikiri kila mahali elimu imeiingia hata kama ni kule mbali kabisa ambapo elimu hapo zamani ilikuwa ni taabu. Kwa hivyo ningependa, hii hali ya kutahiri wanawake, dohara, hizi mila za kuosa watoto wadogo wadogo, siwe sitaondolewa kabisa. Au makabila mengine hii mambo ya kutotahiri, kun'goa meno, siwe pia ni mila ambazo sitaachwa kabisa.

Na lingine la mwisho, labda ni serikali itilie mkazo kwa hawa ma-officer wa nyanjani. Utakuta Officer ameletwa nyanjani akiwa yeye amekuja pale office yake ni pale kwa nyumba yake. Anaandika tu report, monthly report ikiwa anapeleka kule kuwa sehemu fulani ila yeye bado hajafika huko. Kwa hivyo, ningependelea kuwe na wajipikaji wa hawa ma-officers na kuwe kuna hatua fulani ambayo itachukuliwa hawa ma-officer ambao wanakuja na kufanya kazi zao ma-jumbani. Kwa hayo machache hii nakala, inamengi na lakini hata hivyo vyama viwe viwili vya kiwango. Si hivi vyama vingi, maanake, sitapoteza maana. Asanteni.

**Com. Riunga Raiji**: Asante sana Bwana Charo, mwingine ni Nyefu Gitau. Sijui kama ni Njeru ama Nyefu Gitau. Yuko? Imeaandikwa vibaya, Nyefu, Bwana Nyefu yuko, ndiye huyo, karibia. Hayuko? Sorry, sasa tuko na Samuel Mkare, Karibu ni wewe.

**Samueli Mkare:** Kwa jina naitwa Samuel Mkare Mlewa, mimi ninaunga mkono majimbo. Kwasababu kuna mwaka wa milongo mihanda kuna taabu, ninamshukuru Mulungu Were unaishi, soki tukovirisho kalavuki vikikala hata khupate not, uhuru uwe ….

**Translator:** Kwa jina naitwa Samueli Mkare Mulewa na naunga mkono serikali ya majimbo. Najua vituko vyote vilivyo tendekaa kuanzia mwaka wa 1963 mpaka tukaja tukapata uhuru.

**Samueli Mkare**:

**Translator:** Ile kitu kikubwa kabisa ambao tulikuwa tukiteteya wakati wa uhuru ilikuwa ni ardhi. Inaonekana kwamba wakati wa kutetea ardhi, watu wa pwani hatuwa na viongozi wa kutosha kutetea upandi wa ardhi.

**Samueli Mkare:**

**Translator:** Lakini yaonekana kwamba kule juu, kulikuwa na viongozi shupavu wa kuangalia mpango wa ardhi.

**Samuel Mkare**

**Translator**: Kwa hivyo wale viongozi wa kule juu wakajua kabisa kwamba pwani ndio kuna ardhi na wakajua wazi na wapi watakula ule uporu na wapi ni wapi watakula sima ambayo imepikwa sasa hivi.

**Samuel Mkare**

**Translator**: Tuna jua kwamba sima iloyo yani uporu, ni sima ambayo imebaki, imepikwa ikaliwa ikapaki halafu ikaliwa kesho yake.

**Samuel Mkare**

**Translator:** Kwa hivyo sisi huku pwani ule uporu ama ile chakula ya jana iliwekwa na wale jamaa zetu tukale huko juu.

**Samuel Mkare:**

**Translator:** Kwa hivyo wale wengine wetu kule juu, wale mashamba yao yote waliyashika yakamalizika, wakaangali wakaona kwamba ndio sasa kuna nafasi, ndio wakajaa, wakaja kutukandamiza.

**Samuel Mkare:**

**Translator:** Kwa hivyo mimi naomba serikali ya majimbo na mikirudi huku msikae kama vile vya kitambo.

**Samuel Mkare**

**Translator:** Utaona kwamba wakati mwingine kuna kazi zatangazwa watu wakienda wanachua watu wawili tu, watu wa huku pwani.

**Samuel Mkare:**

**Translator:** Kwa hivyo mimi maoni yangu ni kwmaba kuwe na uwazi kabisa, ikiwa watu wanatakikina ni wawili, waseme wazi ili watu wajuee. Si mzazi aende kukopa tikiti apate, watoto wengi waende halafu wachukue wawili tu wengine warudi.

**Samuel Mkare:**

**Translator**: Kitambo nakumbuka kwamba ma-chief na ma-subchief walikuwa wakipigiwa kura, kura ya mlolongo, kwa hivyo kwa nini sasa kuna ugumu wa kufanya kitu kama hicho?

**Samuel Mkare:**

**Translator:** Mengi yamesemwa na yakubali, na nina shukuru kwa yale waliosema machache.

**Com. Riunga Raiji:** Charo kisau, Kanzo Kasungu, Charo Kisau, amezungumza.

**Charo Kisau:** Kwa jina naitwa Charo Kisau mimi nataka serikali ya majimbo kwa sababu kitu ambacho ukifikiria wasiwasi

unaona inalemea upande, ni kama hii, ukichukua chupa ya soda unakuta hata haikujaa, Lakini chupa ya mnazi ama juba yeyote ya samli ama ya mafuta yeyote, kunasemeka mpaka ijae. Ni kunia ya kitu chochote imekuja, haikujaa lakini ukiona gunia ya mkaa au nini inasemeka jazaa kabisa hii gunia ya mahindi mpaka imwagike. Sasa tukiwa na serikali hii ya majimbo, itakuwa kila kitu kina rekebishwa kuwa sawa. Maanake ile kitu huku kuna kunajaa na huko hako hakujai, hapo kuna matatizo lakini serikali ya majimbo kila kitu kiwe watarekebisha wenyewe.

Jambo lingine ninaona nalo katika Commission hii ya Katiba, ni kuwa sawa na wanawake. Katika kazi ama madaraka ni sawa, lakini kimila lazima tuangalie sana, tukisema tuwe sawa tu na wanawake, kweli mimi nitabeba mgongoni mtoto wangu kwa kuwa wamama wanasema tuwe sawa? Kweli hiyo inawezekana hiyo. Tuwe tukichunguza. Ikiwa ni mila, lazima hii Commission iwe itaangalia kimila fulani. Na nikisema hivyo wanazo wanavyoishi, wagiriama nao wanavyoishi. Kwa hivyo tukichanganya kwa kuwa zote tumesoma tumeelimika, tutakuta ni kama tu kufutana futana. Lakini sawa iko tuwe sawa na akina mama, lakini kwamba, ile kimila tuiondoe, hapo tutakuwa tukifutana futana sana. Maanake mimi sitachukua, mtoto ni wangu na amebebwa na mamake, mimi namchekesha chekesha tu hapo halafu nampatia peremente. Lakini si kumpepa mimi. Kwa hivyo tuangalie sana hii kimila. Asanteni sana.

**Com. Runga Raiji:** Sasa tutakuwa na Kadzo Kazungu na baada ya Kadzo Kazungu Tumeombwa na akina mama tuwapatie nafasi wengetaka kuzungumza na sisi wakiwa peeke yao. Nafikiri tutawaheshimu. Kwa hivyo tutaenda break kidogo, watu labda waoche mnazi, au kitu kingine, halafu turidi tuendelee. Kwa hivyo tukimaliza na Bwana Kadzo Kazungu, Kadzo ni mama? Kama angetaka kuzungumza hapa ni sawa lakini baada ya huyu tutawapatia nafasi. Karibu mama.

**Kadzo Kazungu:** Hamjambo wageni

**Comm**. Hatujambo

**Kadzo Kazungu:**

**Translator**: Asema tatizo lake, alifiliwa na bwanake na kawajiwa shamba la hekari kumi nane.

**Kadzo Kazungu:**

**Translator:** Na anasema ana bwanake mdogo ambaye ni Councillor, na bwanake alikufa mwezi wa kumi na moja. Yule Councillor hajaenda mpaka leo.

**Kadzo Kazungu:**

**Translator:** Na alimwajia watot watano, walw watoto watano wanataka kusoma, wanataka kula, nani atawalisha?

**Kadzo Kazungu:**

**Translator:** Je nikishikana na mvulana bado mimi ni mchanga kwasababu bado mimi ni mchanga, akifanya mimba akizaa atakuwa aniongoza, atasema ni wanani?

**Kadzo Kazungu:**

**Translator:** Kwa hivyo anataka kuelewa kwasababu waelewanane. Watoto wanataka nguo za kusomea, hatasipata wapi? Hawana chakula, akizunguka je, watamwambia nini, kwa sababu akisunguka ndio atapata simu. Akikaa hapo nyumbani atapata nini?

**Kadzo Kazungu:**

**Translator:** Hivi sasa wamelala njaa huko nyumbani, amekuja mkutanoni, aende kutafuta vibarua, atunze wanake.

**Kadzo Kazungu**:

**Translator:** Zile heka kumi nane anapokonywa kwasababu yule bwanake alikufa na inaonekana sitakawanywa. Na kwasababu yeye ni mwanamke, yeye hata kwake haendi kumaangalia huyu mama.

**Kadzo Kazungu:**

**Translator:** Kwa hivyo atatumia njia gani?

**Kadzo Kazungu**

**Translator**: Kwa hivyo hana zaidi lakini Mungu wabariki. Lakini mnaelewa haya.

**Com. Riunga Raiji:** Nafikiri tutachukua dakika chache tusikie wakina mama, wazee watupatie nafasi kidogo, tukimaliza halafu tutarudi tuendelee. Asanteni.

**Pastor Peter Pondo:** Tafadhali muwe kando kidogo, ili wakina mama wasidi kuongea. Tafadhali sana.

**Com. Riunga Raiji:** Kuja hapa mbele kidogo au uzungumze ukiwa hapo utuambie jina lako na useme maoni yako, tutaandika na tuko hata tape. Wapi mtu wa kutafusi, Jeffa, we may need translation from either you or Pastor. Can we have somebody so that we can start. Mlikuwa mmejiaandikisha. Okey. Tulikiwa na Eunice Kahindi, huyu aliongea, nafikiri tutauliza tu.

**Jeffa Kingi:** Eunice alizungumza, Nyefu Kisau was not there, Kadzo Kazungu, Josephine Kasosi, this ones, Saumu Mapipo.

**Com. Riunga Raiji:** Endelea Mama

**Saumu Mapipo**

**Translator:** Mimi naitwa Saumu Mapipo, mzaliwa wa hapa Kakoneni na mtu ambaye nimeolewa sehemu za Digo, halafu baada ya kuzaa watoto wawili tukaachana na yule Bwana, yule Bwana tuliishi vizuri mpaka nikamwachia vitu ambayo tulikuwa tumechuma zote, nimemwachia manyumba mengi ya kupangisha, nikarudi kwetu, na nina watoto wawili. Sasa basi Nausukika tena sana.

**Saumu Mapipo**

**Translator:** Kwa nini siwezi kupata chochote katika ile mali na tulipata zote. Wakati tumeoana halukuwa hana kitu, hana kazi, akapata kazi, tukaendelea zote tukapata mali pamoja.

**Saumu Mapipo:**

**Translator**: Alijenga manyumba yenye wapangishaji.

**Saumu Mapipo:**

**Translator:** Lakini mimi ameniacha hivi hivi.

**Saumu Mapipo**:

**Translator:** Maoni yangu kwa Tume ni kwamba mimi kama mzazi pia niwe nina ruhusa ya kupata ile mali, maanake tulipata zote wawili.

**Saumu Mapipo**: Sina mengi na yangu ni hayo.

**Com. Riunga Rainji:** Asha Omari, Asha Omari, ameondoka? Josephine Kazosi.

**Josephine Kazosi:** Jina ni Josephine Kazosi, maoni yangu ni serikali ya majimbo ninaipenda na wamama wameniambia wanaipenda pia. Na ningelipenda sana serikali yetu pia ijunguze wamama hawa walemavu, hasa hawa wamama viwete, kuna wazee wengine hukutana nao njiani, huwabeba wakaenda nao nyumbani kwao, wakawatungisha mimba, basi ikiwa inawesekana, serikali ichukue jukumu kwa wale wazee wanaweza fanya vitendo kama hivyo kwa wale wamama walemavu, wanapowatungisha mimba. Huyo mzee au watu kama hao wahakikishwe na serikali yetu kwamba inachukua jukumu kuwasaidia wale wamama viwete ambao wametungwa mimba kwa njia za kubebwa na wale watoto wanawajiwa wenyewe. Ningalisihi serikali iwasaidie wamama upande huo sana. Maana nimeona kuna kunyanyashwa sana upande huo.

Kitu kingine ambacho wamama tumekaa tukazungumza ni wakati wa wachane. Sisi tukiwa kama wachane, mimi nikiwa ni moja wao. Kuna wamama wengine hata wengine wamebarikiwa wamezaa watoto wa wasichana pekee yake, lakini wakati mzee wake anapokuwa hayuko, ikiwa serikali inaweza kuwasaidia wamama wale wapewe ruhusa, serikali itilie mkazo kwamba

wasichana wao wanapoolewa, wale wamama wawe wanawesa wenyewe kujisimamia na wale watoto wake kwa kuchukua mahari katika moja wa wale wasichana ambao wameolewea.

Nimeona tena katika sehemu nyingi wamama tumenyanyashwa sana upande wa kimatibabu. Kuna jamii zingine ambazo mama anaweza kuwa mgonjwa, tuseme hata kama kwa bahati mbaya labda alisini, hiyo ni kitendo ambacho labda kilimwingia kwa tamaa na binadamu yoyote anaweza kuingiliwa na taama, serikali wacha itusaidie, wamama kama wale wakati mwingine wanapewa purnishment, mtu amegonjeka halafu uonaona jamii haichukui jukumu la kumsaidia huyo mama kwa kumtibu. Serikali tunaomba kama kuna uwesekano, ichukue jukumu la jamii kama hiyo ambayo, mama kama huyo amegojeka. Hata kama ni mama amekozea, lakini kwasababu amekuwa mgonjwa katika ile jamii, kwanza serikali izaidie wamama huyo mwanamke amelengwe kwa matibabu, hata kama ni hiyo dhambi ilitendeka ya washerati. Wacha serikali itusaidie upande huo.

Kitu kingine ambacho nimeona serikali inaweza ituzaidie sana wamama, tunao wasichana wetu wengi ambao wengi wanatungwa mimba bahati baya, labda pengine kwa ukosefu wa chakula, mahitaji ya kimwili, msichana anaona tu ajiingise kwa hiyo ndiyo apate chakula halafu wasichana wana-drop out from school. Ninaomba kama kunauwesekano, serikali, iwazaidie wamama kwa njia kama hiyo, msichana tunapoona amepata bahati baya akapata mimba, kwanza serikali izaidie huyu msichana arudishwe shule na jamii ya huyu msichana ichukue jukumu la kuleea huyu mtoto. Mimi yangu ni hayo na Mungu awabariki.

**Com. Riunga Raiji:** Tatu Katana, karibu mama

**Tatu Katana:**
**Translator**: Ninaitwa Tabu Katana, mimi ni mtu mzima si mtoto niliolewa kitambo hapa Machengo.

**Tatu Katana:**
**Translator:** Ile plot nakaa saahi hata huyu Chief wetu alipokuwa anazaliwa, mimi nilikuwa nakaa pale pale tayari. Na nilizaa watoto kumi nikiishi katika hiyo plot.

**Tatu Katana:**
**Translator:** Saa hii basi sasa naambiwa si kwangu mpaka kuna mzee moja anaitwa Kadenge amesemekana yeye ndiye kwake sasa.

**Tatu Katana:**
**Translator:** Na yeye nakumbuka tuligawanya yeye akashika upande wake mimi nikashika wangu. Ule wake agaugawanya mpaka ukamalizika wote.

**Tatu Katana:**

**Translator:** Sasa ameuza upande wangu , ameuzia Church sasa nyumba zangu itabidi nivunje, niache mgeni ambaye ametoka Malindi kuja kuchukua eneo lile, niondoke na watoto kule.

**Tatu Katana:**

**Translator**: Kwa hivyo mimi, hata hivi leo inasemekana nimehuwawa, itakuwa ni ukweli, maanake mimi sitaki kuotoka pale, pale ndio kwangu sasa.

**Tatu Katana**:

**Translator:** Tuko niko msichana mimi naishi pale, kwa hivyo tafadhali siwezi kuondoka. Hata watoto wengine polisi na wanajuwa kwao ni pale.

**Tatu Katana:**

**Translator**: Kwa hivyo wanasema si kwangu, niende wapi sasa?

**Tatu Katana:**

**Translator**: Yangu ni hayo.

**Com. Riunga Raiji:** Asante mama

**Jeffa Kingi:** Magret Mterengo.

**Magret Mterengo:**

**Translator:** Naitwa Magret Mterengo.

**Magret Mterengo:** Bwanangu alikufa, nimezaa watoto saba nao pia waliondoka duniani wamekufa. Nikabaki pekee yangu sasa. Sina mtu wa kunidutumia, ni mimi tu basi nimebaki. Kwa hivyo yangu ni hayo machache ninaomba serikali ya majimbo.

**Magret Materengo**:

**Translator:** Basi tu hayo.

**Jeffa Kingi:** Furaha Karisa

**Furaha Tatu:**

**Translator**: Mimi naitwa Furaha Karisa, nimeolewa hapa Kakoneni.

**Furaha Tatu**:

**Translator**: Sisi tuliolewa mabibi wane nyumbani. Na zote tulizaa, mimi nina watoto watano, na Bwanangu sasa hawezi kazi tena.

**Furaha Karisa:**

**Translator:** Watoto wangu wananipatia shida sasa.

**Furaha Karisa:**

**Translator:** Nataka kuwasomesha watoto wangu lakini kile cha kuwapelekea watoto wangu shule sina sasa.

**Furaha Karisa:**

**Translator:** Watoto wangu wengine bado ni wadogo, wale bibi wenzangu wana watoto wakubwa, sasa wale wa mabibi wenzangu wengi wanasomeshwa na watoto wao maanake ni wakubwa wale.

**Furaha Karisa:**

**Translator:** Mimi watoto wangu ni wadogo hawaja jua chochote. Na Bwanangu hana kazi.

**Furaha Karisa:**

**Translator:** Sijui nifanye nini?

**Furaha Karisa**:

**Translator:** Magonjwa ni mengi kwa watoto, ni mimi mwenyewe niende huku na huku nipate chochote niwapeleke hospitali.

**Furaha Kanisa**:

**Translator:** Ikiwa sina peni lolote ninalopata niwapeleke hospitali je! shule nitapeleka? Kwa hivyo napata taabu sijui nifanye nini?

**Furaha Karisa:**

**Translator:** Yangu ni hayo.

**Jeffa Kingi:** Mikija mseme maoni, si shida, ikiwa ni shida useme shida yako halafu useme ningependelea itatuliwe hivi. Halua Muramba, maoni yako? Hana. Monicah Mukamaji.

**Monicah Mukamaji:** Kwa majina naitwa Monicah Mukamaji, kwanza ningeanza kuhusu hii pombe. Ingawaje Wanaume wamesema kwamba wanataka pombe iruhusiwe, lakini kwa kweli sisi wanawake tunahumia. Kwasababu hawa wanaume wakiwa wamelewa, saa ingine watakuja na fujo, labda wakupige ama wakutoe nje ndani ya nyumba ukalale nje, kwa hivyo

ningeomba Katiba iaandike, ikiwa wataruhusu hii pombe, lakini wale wanaume wawe na kiasi fulani wakinywa, ama wasiwe wanapiga wale wanawake wao, wawe watachukuliwa hatua.

Lingine ni kuhuzu hivi vitambulisho, kusema ukweli, sisi zote tunaoishi hapa, si wote ambao tunapesa za kuweza kutumia kwa vitambulisho. Na vitambulisho vimekuwa ni pesa, kwa hivyo ningeomba hiyo Katiba pia ingalie hili tatizo la vitambulisho iliwawese kutoa bure. Kwasababu mimi tayari nikiwa na watoto wangu, pengine ni watatu wanataka vitambulisho, na pengine pale sina senti, kwa hivyo hapo wataonekana wale si raia. Kwa hivyo ningeomba pia hivyo vitambulisho viwe ni bure.

Lingine ni kuhusu msitu: Kwa kusema ukiwa sisi tunaoishi hapa, tuko karibu na msitu, tuna mashamba yetu yako karibu na msitu, na sisi wanawake zaidi ndio tunaumia kwasababu sisi ndio tunaolima, tunalima kwa bidii, lakini ule msitu ulio karibu na sisi una ndovu, una wanyama wengi wanao tuaribia mashamba yetu, ambapo hatulipwi na hatupatiwi chochote kwa hivyo vinavyo haribiwa. Mahindi mseme mlilipwa. Kwa hivyo tungeomba hiyo Katiba pia ikiaandikwa, iwe na Sheria za kuwa tukiaribiwa mimea yetu, tutalipwa kiazi gani ama tutafanywa nini?

Lingine ni kuhusu hii Katiba, kwa kusema ukweli hii Katiba, ni wengi hata ukihulisa hawa wakina mama wengine bado hawajasoma na wengine wamesoma. Lakini bado hawajaiona kwa macho hii ni Katiba. Kwa hivyo ningeomba, hii Katiba tukiwa tumeiaandika, ingawaje itaenda huko, iende ikaandikishwe vizuri, lakini tungeomba pia irudi hapa kila mtu apate kuiona na kuijua wale ambo wanajua kusoma. Kwa hivyo yangu ni hayo machache.

**Com. Riunga Raiji:** Asante mama

**Jeffa Kingi:** Rachel Kona

**Rachel Gona:** Mimi yangu ni kusema kwamba, jina langu mimi naitwa Rachel Gona, maoni yangu ni kwamba hii Katiba hii ambayo imeanza sasa, kwangu mimi naona ni nzuri sana, kwasababu ninaonelea kwamba, sisi wanawake tunapata maonevu kwamba, kuna wengine ambao sasa, yaani ni kama Wanaume wanaendelee kuwa ma-chief, ma-DO na kadhalika, lakini sisi, hatujapata ile nafasi ya kuwa ma-Chief ama ma-Sub-chief. Kwa nini sisi sasa tunawachwa nyuma. Kila wakati tutakapo, tunasema tunataka kwenda mbele, tunaambiwa nyinyi hamfahi, mtarudi nyuma. Ni kwa nini sisi tunawachwa nyuma, na sisi tunataka kuendelee mbelee? Tunataka kuwa chief. Hakuna mtu ambaye hataki kuwa mkubwa. Kila mtu anataka kuwa mkubwa. Na ma-chief ni hawa ambao wanabeba ma-briefcase, wamejaa, matumbo yao ni mazuri, wakula chakula na sisi tunabaki hivyo hivyo. Kwa hivyo maoni yangu ninaomba kwamba hii Katiba iandikwe vizuri na sisi pia tuajiriwe kama hao pia. Na wakiwa hawakufanya kazi vizuri, ninaomba Katiba hii ichukulie hatua, kama ni kufutwa kazi, wafutwe kazi, tubaki kama vile vile ambavyo tulikuwa. Ni hayo maoni yangu.

**Com Riunga Raiji:** Usife moyo mama, nilienda ukambani nikakuta Chief na manaibu wake wengi ni wanawake, inawesekana

na inafanyika.

**Jeffa Kingi:** Anjelina Abel.

**Anjelina Abel:** Kwa majina yangu naitwa Anjelina Abel, natoka hapo Chilore. Maoni yangu ni juu ya watoto wetu wa kiume na wakike. Tunafanya bidii kusomesha watoto wetu sana, lakini wanapo faulu na kupita mtihani wa form four, huwa hatuna uwezo wa kuwapeleka juu. Sasa ikiwa kunatoka kazi kama ni ya upolisi au ni ujeshi, watoto wetu hawezi kupata nafasi kabisa huko Malindi. Maana watoto wakitoka hapa wakienda kule, wanakuta tayari watu wametoka Nairobi na barua zao. Tunashindwa, na hapo pia kuna mkubwa moja Kazungu hapa, sijui ni kwa nini anatupagua hasa watu wa Chilore? Pale Chilore hatuna polisi kabisa, na kuna vijana wamemalisa form four, si wasichana siwavulana, sijui wao wanataka kiasi gani kile? Kwa hivyo napendekeza sisi watoto wetu, wapate kuandikwa ikiwa ni jeshi, ikiwa ni polisi na sisi nasi tuweze kupata Maendeleo juu ya watoto wetu. Tupate kula matunda ya watoto wetu maana ma-Bwana pia wengine karibu wata-retire. Ikiwa wame-retire na watoto wetu tunao, kwa nini tusifaidike juu ya watoto wetu. Maoni yangu ni hayo tu.

**Jeffa Kingi:** Sidi Baya, Sidi Baya? Margret Chengo.

**Margret Chengo:**
**Translator:** Mimi naitwa Magret Chengo, nakaa makobeni.

**Margret Chengo:**
T**ranslator:** Naomba serikali ya majimbo.

**Margret Chengo:**
**Translator:** Tatizo langu kubwa ni mashamba.

**Margret Chengo:**
**Translator**: Mashamba tumekuwa nayo kwa muda mrefu, hata inazidi miaka ishirini toka tuchukue haya mashamba.

**Margret Chengo:**
**Translator:** Hatujaona Title Deed wala nini. Hata Officers wa-lands wakija ma-chiefs wanatwambia tutoe pesa mwazo ndio wale ma-officers waje waangalie mashamba yetu.

**Margret Chengo:**
**Translator**: Kwa hivyo maoni yetu ni kwamba Title Deed sipatiwe kila mtu, si yule mwenye pesa ambaye anatoa pesa apate, sisi masikini kama mimi nikose.

**Margaret Chengo:**

**Translator**: Ya pili ni nikuhuzu shule, mwaka huu tuliambiwa kwamba, masomo yatakuwa bure, lakini tunashanga, serikali haijaleta chochote na walimu sasa wanaitisha pesa ya choki.

**Margret Chengo:**

**Translator:** Na wazazi hawana pesa.

**Margret Chengo:**

**Translator:** Sasa watoto wetu wanaenda shule na wanaweza fukuswa sababu hawana chochote, hawana pesa.

**Margret Chengo**:

**Translator:** Kwa hivyo maoni yangu kwa Tume elimu iwe ya bure. Ni hayo tu.

**Com. Riunga Raiji:** Asante mama.

**Jeffa Kingi:** Margret Kazo.

**Margret Kazo:** Kwa majina naitwa Margret Kazo, mzaliwa wa Chilore Sub-location, maoni yangu ni kuhusu elimu. Mimi huwa nina shangaa ninaposikia kuwa walimu wako nina mpango wa kugoma, Sababu tumesiangalia huwa hatuzielewi. Wanao zielewa ni wale wakubwa. Sasa kama sisi wazazi tuko na shida kutafuta pesa ya watoto wetu wasome. Mara hivi twasikia walimu watagoma hata hivyo wana mpango wa kugoma, sijui kama hii serikali yaangalia kivipi huu mpango wa hawawa kugoma. Mimi jambo hili huwa linanisikitisha sana.

Maoni yangu mengine ni haya, ikiwa serikali iko na mpango wa kutuzaidia, watoto wetu wasome bure, basi, iangalie tu masomo kule secondary na kuendelea juu mpaka watoto wetu watakapo pata kazi, lakini elimu ya msingi, tunaweza tukang’a ng’ana sisi wenyewe hata kama ni kuhusa mboga, kwenda kwa kibarua, atamaliza tu standard eight. Lakini kule mbele huwa unashindwa. Mtoto akitaka kwenda Form One, utanunua nguo, mambo mengi, huko shule hakuna, sabuni, kila kitu, mtoto lazima huwe na vile vitu kwanza halafu ndio mwalimu atasema sasa mama vitu vimekamika, leta fee, utashindwa wewe na ile fee, kwasababu vitu umevinunua na tena mtoto utabaki naye. Mwalimu akwambia regea na mtoto wako. Vitu ni sawa lakini twataka chochote hapa. Mtoto wako atakula nini? Sasa nikuwa kule nyumbani sijiwezi, huyu mtoto wangu atasoma? Sitaweza kumsomesha mtoto wangu kwa secondary lakini huku nyuma, tutajikaza kidogo, kidogo.

Na haya mambo ya kuwa mimi nimebeba kikapu ya mboga, huku napeleka Malindi sokoni, tukiwa kule kwenye vipanda, hakuna hata mama moja ambaye yuko na kibanda cha mboka. Waona wale watu wabara watupu, wameapatiwa vile vibanda

vya mboga, na soko ni letu, lakini twashanga sana! Ukifika kule, yule mtu wa bara hata pengine hataki mchicha bali mchunga, yeye zake ni nyama, sukuma hiyo, hata nikipenda huku mtu wa bara hatanunua sukuma yangu. Anasema hii sukuma siyo ya bara. Hasa ni kwa nini yeye alipatiwa kibanda hapa kwetu? Kwa hivyo masoko yetu tupatiwe sisi wenyewe. Hatujakataa watu wa bara, na mtu wa bara ikiwa yeye yuko na hoteli hapa, ahaandike watu wa hapa, siyo kuchukua watoto kutoka bara waje waanjiriwe kazi huko, hatutaki. Na wakiona hiyo ni ngumu wabebane na hizo hoteli zao waende nazo kwao. Hayo ni maoni yangu, sijakata mtu wa bara mimi, kwasababu sikusoma sana lakini najuwa kusoma gari hii inaenda wapi.

Haya maoni yangu mengine huko kwetu, kwa kimila ya Mjikenda, inasemekana kuwa, msichana, yaani mwanamke hana urithi kwa babake, ukuolewa ni basi, unaenda hata ukipata shida kwa Bwanako kwenu kuna vitu lakini hivyo huwezi kuvifaidi. Kwa hivyo mimi huwa nashangaa sana na kusikitika rohoni mwangu. Kwa nini kama mwanamke ameolewa, baba anipatie hata kama ni karombo ka heka, aseme msichana wangu ameolewa lakini uje ukilima hapa. Hata huko kwa bwanako hata huta lima ulime lakini kipande hiki, mkwe wangu ujuwe hiki ni cha mtoto wangu. Lakini kuwa mimi niolewe, kwetu sina uridhi wowote, hiyo ni shida,nilisikia serikali imepitisha hiyo, lakini huku kwetu Mijikenda bado haijafika hiyo Sheria hiyo na kama iko, basi yapanwapanwa huko bara. Si ndiko kuna ambako kuna wale watu ambako wamesoma sana.

Na maoni yangu mengine ni haya, akiwa bwanangu ataona watoto wangu ni wawili wote wako darasa moja, na wataenda hivyo hivyo pamoja pamoja, akili zao ni sawa, ikifika darasa la nane, wote washinde pamoja, sitaki mimi mtoto wangu ule msichana ahuuzwe ati tumsomeshe yule mvulana. Wote wale ni watoto wangu uchungu wao naujuwa mimi mwenyewe. Baba hajui uchungu wa mtoto, watoto wangu wote nawapenda sawa. Kwa hivyo nataka hata kama yeye atataka kuuza msichana na basi yeye ahuuze yule mvulana. Kwa nini anachagua umbo lake ndio hataki amuuze? Kama kuna soko la wavulana wauuzwe. Wasichana wasomeshwe. Kwa hivyo mimi sipendelei. Kuna mzee mwingine amesimama basi mimi nikiuza msichana kwa sababu nimeshindwa na fees. Kama umeshindwa na school fees, wote wabaki. Hakuna mtu atalalamika pale, sio kumuuza msichana. Kama kuna soko la wasichana hata la wanaumme liweko.

Maoni yangu mengine ni hii mambo ya kutoa pesa kwa hospitali: Hospitali siko mbali na Malindi, ukifika uko utaonga poleni wewe, kwasababu hata kupata ile kati unaambiwa leta shilling kumi, kabla ya kuona Daktari, utang'ang'ana uende kwa Daktari utaandikwa madawa vizuri sana. Haya mama nenda uchukue madawa, niunge kwenye lane ya kwenye madawa nikifika kwenye madawa, nahitishwa pesa, kila dawa iko na bei yake. Hakuna nchini ya Shilingi hamsini ya dawa. Hata kama ni ya maji, kama ni ya tembe, zile dawa utapata usingizi tena hizo ni ghali. Mimi nashindwa, hizi hospitali, iondolewe hii mambo ya pesa, kama serikali kweli inatupenda, iondoe hi mambo ya pesa kabisa. Hospitali tukienda twende bure. Unaona kuna private zimejaa, kwasababu mimi naonelea kwanza niende kwa private, nitoa mia tano, lakini mtoto wangu atatibiwa na kesho sitatoa tena pesa. Kuliko huko huku serikalini naambiwa leta hamsini. Mtu wa kufagia pale nimemuandika mimi mweyewe, tena wao Daktari wanataka hamsini wanipatie dawa. Kesho nirudi kule aniambieye leta Shilingi thelathini, ni shidano, ukiandikiwa shidano kumi, no shauri yako hiyo ni mia tatu. Mimi huwanashindwa sana, saa ingine wakina mama wanatoka huko mbali, wanaenda kusalia malindi, akifika huko kama hana pesa, atafanya nini, unakuta wengine wanarudishwa, amezaa na ujauzito

wake. Amekufa na mimba yake kwasababu pesa hakuna.

Maoni yangu mengine ni juu ya barabara, siende mpaka huko ndani kabisa, kule kunaitwa msituni, tena kufike magari. Wale ambao wanapatiwa licences za kupeleka magari si apende tu Kakoneni kwa sababu anaona hapa ni kijiji, kama ni gari yake ni barabara ya Kakoneni, aende kabisa mpaka Chakama. Sio leo aende chakama, kesho ahendi. Vitengeni hakufiki gari. Kama kuna mgonjwa, hakuna hospitali, kwenda hospitali Malindi itakuwaje? Tena hawa wenye magari haya mafuta yateremshwe bei, kama yako mbali, mfanye mpango. Kwasababu mimi sina ticket, niko na mgonjwa, na ninahitaji ticket. Nitafanyanje, siwesi kupeleka mgonjwa peeke yangu, mgonjwa niwe na wenzangu, wanizaidie kumwingiza ndani ya gari. Ikiwa mimi nitoe Shilingi sabini pekee yangu, naenda Malindi, mgonjwa sabini, wale wenzangu wengine? Haya sina pesa mama shauri yako. Yule tun-boi ako na amri juu ya gari kushinda yule mwenye gari. Kwa hivyo mimi naomba hizi barabara siende mpaka kule ndani, na kukiwa na uwezo.

Maoni yangu mengine, akiwa Rais ni mme, kwa nini mimi nisiwe Rais, hivi nimesika kunakuja kura sijui za madiwani mpaka huko kwa Rais, nikasika mpaka uwe umefika form four, sikupenda kwangu kutofika form four. Mzazi wangu alikuwa hana nafasi, sasa wewe huko Sheria zenu mkisema mpaka uwe umefika form four ndiyo utasema ukuwe diwani, huku kutakuwa na madiwani wanawake? Hakutakuwa, Sheria zenu sifike kule kunaotoka haya mambo hayo. Na sisi tunataka huku, hata kama mimi sijui kusoma, lakini najuwa kuongoza, nikiwa nina mji wangu peeke yangu, na ziombi chakula kwa nini nisiwe diwani au nigawa Rais kule, unasema mpaka uwe mpaka umefika form six, form six nitaendaje mimi, hata standard one sikuenda. Asanteni. Maoni yangu ni hayo.

**Com Riunga Raiji:** Asante sana Mama.

**Jeffa Kingi:** Margaret Baya, Rose Mwatela.

**Rose Mwatela:** Jina naitwa Rose Mwatela, nilikuwa nataka kuzungumzia vyama vya kisiasa.. Vyama vya kisiasa saa hii tunasikia ni arobaini na vinane hatujui kama vinaongeseka, na kuna wengine wameanzisha kwasababu wanataka wa-benefit, yaan wanafanya kama ni biashara. Ndiyo tunasema kuwe na kama vyama kumi tu. Kuwe na vyama kumi pekee yake.

Tunazungumza kuhusu President: Akiwa mwanamme, hoyu mke awe makamu kulingana na qualification zake, huyo mwanamke, sisi nazo tupate hiyo nafasi.

Kuhusu urithi: Huyo mtoto mme akipata ardhi huyo mtoto wa kike apate sawa na yule mtoto wa kiume.

Nitazungumzia kuhusu viongozi: Mfano kama DC. Yeye tayari ni DC, alafu anaongesewa na cheo kingine juu, Nominated Councillor. Sasa sisi wenya hatuna kazi iweje? Kwa hivyo hatuvitaki kabisa. Yeye akiwa DC abaki DC, u-Nominated na sisi

pia tupate.

Kuhuzu umasikini: Kufikia saa hii, Kenya tumekuwa masikini kwa sababu ukimwi uko, kuna watu ni masikini sana hata chakula kupata haiezekani, fees, hata madawa, na unakuta serikali inagharamia mambo mazito mazito, mfano kama hiyo msinga hiyo ya magari, kuna ma-pesa yaani tuseme, kwa nini pesa kama zile zisitumeke kwa watu pengine wakonjwa?….

Nitazungumzia kuhusu Wabunge: Mbuge mwenye tumempigia kura sisi anahaki ya kupewa uwaziri. Lakini si Nominated amewe mpaka saa hii yeye amechaguliwa kama ni wasiri na sisi hatukumchagua. Kwa hivyo tunasema ya kuwa yule tulemchakua sisi kupitia kwa kura zetu awe waziri lakini ni Nominated mbunge aende akafanywe ni wasiri na mpaka saa hii amefika kiwangu cha juu, kwa sababu babake pengine alikuwa na cheo ndio kina inakuwa kitu kama hiyo, kwa hivyo hatutaki.

Tunazungumzia kuhusu walemavu: Kuhususu walemavu, kuna badhi ya walemavu wamesoma vizuri sana na unakuta hawezi kufanywa kama headmistress kwasababu anaambiwa hawezi, tunasema kulingana na qualification zake, serikali pia imwangalie kulingana na qualification zake.

National Schools: Tunataka National Schools siwe huku pwani, si mpaka twende Central, huku nasi tupate hizo National Schools hata University pia tuletewe huku sisi watu wa pwani.

Kuhusu Wanyama: Serikali imejali sana wanyama, mfano tu tuko hapa na msitu, kuna msitu unaitwa kaliapapohapo, ndovu wanaharibu mimea, nyati wanaadhiri banadamu kwa hivyo tunasema ya kuwa, ikiwa mnyama ataharibu bidha za mwananchi, ebu kumua eti alipwe pesa nyingi sana, si habari ya kuwa vitu vyangu vimeliwa nachadanganyiwa na kilo mbili za mahindi. Hatutaki tulpwe gharama.

Tunasema kuhusu ardhi: Mu-Kenya, hatugekuenda ya kuwa mu-Kenya atawale popote anapotaka, tusema mfano, kama wewe ni mtu wa pwani, una haki ya kutawala huku, lakini kama wewe ni mtu wa central, unaweza kunua huko juu. Kwa hivyo tunasema ya kuwa mtu atawale kilingana na mahali ametoka. Kwa hivyo twataka serikali ya majimbo. Ni hayo tu.

**Jeffa Kingi:** Next Juma Katana Chengo

**Juma Katana Chengo:**
**Translator:** Jina langu ni Juma Katana Chengo, nakaa Kakoneni, Shela kule juu.

**Juma Katana Chengo:**
**Translator**: Maoni yangu ni kwamba ninakiliyo kikubwa sana, nilifiliwa na Bwana yangu.

**Juma Katana Chengo:**

**Translator:** Akaniachia watoto wakiume watano wote wakawa wako secondary alipokufa. Ikabidi watoke shule wote.

**Juma Katana Chengo**:

**Translator:** Nikawa na shamba langu hekari kumi-nane, likiwalimeja minazi kule Masangoni.

**Juma Katana Chengo:**

**Translator:** Kukatokea mtu alikuwa anataka kuinunua lakini akawa kuna gharama ya laki moja ishirini ilipwe watu walands mwanzo.

**Juma Katana Chengo**:

**Transalator:** Hiyo bei ilipeanwa na watu wa Lands. Kwasababu ya kupima na ku-asses ile value la shamba.

**Juma Katana Chengo;**

**Translator:** Kwa hivyo wakasema kwamba ikiwa nataka kuhuuza niuuze lagi mpili unusu.

**Juma Katana:**

**Translator:** Kwa hivyo huyo mtu akalipa laki moja na akachukua ile form akaenda kabisa. Sasa hivi leo mwezi huu ni watisa huo.

**Juma Katana Chengo:**

**Translator:** Watoto wangu watatu wamemalisa chuo kikuu, sina pa kuwapeleka kabisa. Hata ni wavuvi sasa.

**Juma Katana Chengo:**

**Translator:** Hiyo karatasi ya kuuziana kuandikishana iko kwa wakili, sasa hivi hiyo shamba saa hii ina watu wanakula matunda ya mti yangu, sieziingia pale mimi.

**Juma Katana Chengo:**

**Translator:** Kwa sasa hawawesi kutumia ile pesa pale kusoma ama kuoza wanawake.

**Juma Katana Chengo:**

**Translator:** Maoni yangu ni kuhusu mashamba, ni vipi naweza kumiliki shamba langu mimi?

**Jeffa Kingi**: Una maoni mengine, ya kugeuza Katiba?

**Juma Katana Chengo:** La

**Jeffa Kingi:** Nyefu Katana.

**Nyefu Katana:** Kwa jina naitwa Nyefu Katana, nashukuru kwa wale wenzangu waliosema nataka serikali ya Majimbo ni hayo tu.

**Jeffa Kingi:** Jumwa Charo, Jumwa Charo? Dama Muhammed, Dama Muhammed? Lozi Mwachiru.

**Lozi Mwachiru:**
**Traslator.** Jina langu ni Lozi Mwachiru, mimi nataka majimbo yarudi Kenya.

**Lozi Mwachiru:**
**Translator**: Watoto wetu huku pwani wamekaa, wamesoma na hawapati makazi, tulisema twalilia uhuru, uhuru kukuja kumbe ndio umetutia katika matatizo kabisa.

**Lozi Mwacheru;**
**Translator:** Nilipeleka shule watoto wangu kumi na moja, walio pata kazi ni wawili tu. Wote wamekaa nyumbani.

**Lozi Mwacheru:**
T**ranslator:** Hasa mimi niliwapeleka shule ili waje washike jembe kulima.

**Lozi Mwacheru:**
**Translator:** Nataka waende mezani kama hivi.

**Lazi Mwacheru:**
**Translator:** Uhuru ndio umetupeleka.

**Lozi Mwacheru:**
**Translator:** Kwa hivyo nataka majimbo yarudi watoto wetu waendelee.

**Lozi Mwacheru:**
**Translator:** Kwa hivyo uhuru tupate , kutokea kwa majimbo.

**Jeffa Kingi**: Christian Nyanche

**Christine Nyanche:** Kwa majina naitwa Christine Nyanche. Nitazungumzia kuhusu walemavu, form sikija wanapatia wale ambao sio walemavu na hawajui tabu za walemavu. Wanajukua zile pesa zote wanakula wao. Walemavu wanabaki hivyo, sawa natanganya?

**Audience**: Apana

**Christine Nyache:** Kadeni gati, shilingi kadha uwe member, kuna kitu fulani kimetoka, hutakiona, kitasima sima, hata hutasikia tena chotote. Kutakucha form kutoka huko juu, jaza hii utapatiwa msadaa, sinapatiwa wale ambao si walemavu. Wanachukua yale makaratasi wanajasa wanamaliza na wanayatuma. Kwasababu si walemavu hawajui taabu za walemavu. Kwa nini wanaandikwa hao. Kunakuja forms zingine sinapatiwa ma-Chief, ma-Subchief, tunapatiwa tunaijasa, kisaha hao chief na ma-Sub-chief wanasema tupatieni kitu kidogo ndio tumjaziye. Mlemavu hutapatia nini? Pendekezo yangu ni kwamba kama ni ma-officer wa walemavu wawe walemavu. Kitu ambacho kitatokea kije through walemavu. Lakini sio watu ambao sio walemavu. Ndio pendikezo langu. Na ikiwa mlemavu amesoma, anawesa kuaandikwa pahali popote.

**Jeffa Kingi:** Nyefu Kisau.

**Nyefu Kisau:**
**Translator:** Jina langu naitwa Nyefu Kisau, mimi mwanzo napendekeza majimbo halafu mimi nilifiliwa na bwanangu.

**Nyefu Kisau:**
**Translator:** Huu ni mwaka wa kumi na tano toka bwanangu aniachie, nikaachiwa shamba na ikachukuliwa na kakake yule bwanangu

**Nyefa Kisau**:
**Translator:** Babangu mzazi akaninunulia shamba. Hilo shamba lilitolewa pesa lakini wale waliopatiwa hiyo pesa, sasa wanaanza kunisumbua kutaka ile shamba.

**Nyefu Kisau;**
**Translator:** Sasa nifanye nini mimi na watoto wangu?

**Nyefu Kisau**:
T**ranslator:** Unapendekeza aje, yatatuliwe vipi**?**

**Nyefu Kisau:**

**Translator:** Kwa hivyo ningependa serikali izaidie wachane hasa upande wa mashamba.

**Jeffa Kingi:** Pili Ali.

**Pili Ali:** Mimi naitwa Pili Ali, na maoni yangu kuhuzu Majimbo ni kwamba, kwa mfano upande wa reserve kuna ma-cash crops nyingi sana kama hii pombe ambayo emeleta mambo mengi sana. Sasa watu wengi hawapati faida yake, watu wa huku, lakini watu wa inje tu ndio wanapata faida yake.

Na upande wa urais ni kwamba wanawake pia wanaweza waka-partcipate kwa hiyo mambo kwa sababu hata kwenye urais mwaka uliopita Charity Ngilu akiwa ni mama ndiye alibiganiya. Hata kwa hivyo hata mtu kama mimi ama mwingine anawesa akaingia katika hiyo nafasi.

Na upande mwingine ni kwamba, kwa mfano hawa wamama ambao wanajifungua, kama hakuna kituo mahalumu ambacho kiko karibu, ama nguvu za umeme, hasa hapa Kakoneni, kuna watu wengi sana ambao wanaenda kijifungua kwa wakunga, watu wa nyumbani, na hiyo naona si njia nzuri sababu, sana sana huwa hawapati matibabu mazuri, wanadhirika maisha yao. Sasa kwa hivyo mimi naona ni heri kuwe na kituo mahalumu ambacho kitaweza kuchagua watu na kitakuwa na uwezo wa stima ambazo sitakuwa sawa tu na kule town. Hatakuwa na shida ya wamama ambao wana watoto. Kwa hivyo ni hayo tu Asanteni.

**Com. Riunga Raiji.** Asante mama.

**Kadhu Soya:**
**Translator:** Mimi naitwa Kadhu Soya nimeolewa Mpaloni.

**Kadhu Soya**:
**Translator:** Maoni yangu ni kwamba sisi wanawake nyumbani tunasikitika sana.

**Kadhu Soya:**
**Translator:** Ya kwetu ni hali ya vile ambavyo umeolewa, sasa tu umeingia hapo kwa nyumba tuka msichana ili hakuna chochote nyumbani, sasa mwendelee mpaka mshikane hata mingie hivi na hivi na kufanya kazi ambazo mtaongozana na kufikiria mawazo ya kujijenga. Sasa endelee inje hata ikikuwa hata ndiyo mshakuwa watu wakubwa, mshapata vitu sasa, kule kwa Bwana awe ni mtu ambaye anatodharau ya wewe huna chochote. Huna chako pale kwa nyumba. Ikikuwa ni vitu vya shamba vyote vimemlemea Bwana, kila kitu, sasa wewe huna mamlaka kabisa. Kwa hivyo utakuwa umepanda mnazi, mnazi ushakuwa unagemwa, ni mzuri kwa vile ambavyo una mapato ya kuleta kila aina utakacho kwa mnazi. Lakini kwa nyuma, tuna shida na midomo. Mtu anatoka akija anasema huna chako kabisa. Hapo nyumbani, hata ni heri pesa yeye akishika ni kule nje wale ambao ni walevi wenzake wanawake yeye, anakuwa na hao sasa washakuwa mabibi wengine, ambao wewe atakusahau

kabisa. Sasa unasikitika na watoto. Sasa mawazo yako saa yote una kilio tu. Ikiwa ni nyumba anasema si yako, hapa hata huna chako. Lakini wale ambao analewa nao pamoja, sasa yeye hao mavuno ashakuwa nayatolea inje. Wewe ushakuwa mtu hata kama, ushakuwa mgonjwa, mwenyewe ama mtoto mdogo na wewe ukiangalia ushakuwa mtu mzima Kwa hivyo hayo maoni hayo nilikuwa naonelea ni mpatie.

Na maoni yangu tena ya pili, ni urithi ambao ushazaliwa na mzazi wako sasa mungu amwendelea ameondoka. Sasa vile ambavyo ni mali ambayo mali ile ya babako, sasa ndugu zako wawe wanauza lakini wewe huwe huwesi kupata fungu pale. Na pengine hata walikuwa hawajui. Hata wewe babako alikufa, wakiwa wadogo, sasa vile washakuwa wakubwa, uwaelekeze ndugu zangu hapa mahali fulani ndio mpaka wa baba. Hapa, alikuwa hapa, fulani waliuza, sasa hawa waliouza, lakini mjuwe huku ni kwenu. Sasa pale ni sawa wewe nawe upate fungu pale, wakukatie. Sasa wale ndugu pale nao wawe na njaa wanasema huyu ni mwanamke hawezi kupata fungu lile la baba. Kwa hivyo hapo ndipo ninaonelea kuanzia kitu cha nyumbani basi Bwana akiwa ni mlevi zaidi na kulewa kwake ni wewe ndio hana haja nawe. Vitu na unaangalia, pesa anasipatia wengine kule nje kabisa na wewe unalia na watoto. Kwa hivyo oni hilo, ndio ambalo nilikuwa ninapendelea hiyo ikiwa inaweza kuondolewa, hiyo iondoke. Sisi wanawake nazi tuwe na heshima nzuri ili ndio tanaweza kujijenga.

Hata umasikini tunaona saa nyingi unaingia hapa Kakoneni kwa hivyo, kwa hivyo mtu anapendelea nje zaidi mpaka nyumbani anasahau. Sasa ni lazima ndio naona nyumba iko kinyonge. Kwa hivyo neno hilo naomba msada ambao serekali iweze kutufanyia na sisi tukuwe na kujulikana tuna watu.

Na lingine ni hilo la mashamba, kukiwa ni uridhi, wewe nawe pale uwe unaweza kupata. Na lingine tena mbalo ni latatu ni hali ya mashamba, kule kuna mashamba mengine ina mteremko wa uko njini una wanyama. Wakati mwingine hulima na ukiendelee yashamalisika kuzaa, ukienda ndovu washakula kabisa na hapo huwezi kupata chochote. Hicho ni kilio ambacho kuwa nampatia. Lakini kubwa zaidi likuwa ni hili la kinyumbani. Kwa hivyo hayo ni maoni yangu. Tupate heshima ya kuheshimika sisi wanawake, hayo ndiyo maoni yangu. Kwa hivyo hayo machache, Mungu ayabariki.

**Com. Dr. Nunow**: Mwenye kiti anaendelea kuja nafikiri tunaendelea, na mpaka tulipofika sasa mtu anayefata katika orodha ni Gilbert Safari, Gilbert? Baada ya Gilbert ni Katana Mbaya, Katana Mbaya yuko, anayewafwata wale ni Robert Fondo, Steven Charo.

**Steven Charo:** Basi asanteni sana Ma-Commissioners na ma-officer ambao mmuefika hapa. Mimi nikuongezea hasa ile memorandum ya kwanza kabisa, ambayo imesomwa kutangulia. Na Majina yangu kamili naitwa Steven Charo Silia. Mimi na-suport serikali ya majimbo kwanza.

Pili, ile structure ya majimbo: Kimaoni yangu iwe namna hii, yaani pale juu tuwe na Ceremonial President, halafu chini kuna Prime Minister ambaye ndiye kiongozi wa Serekali, halafu pale njini sasa kuwe na ma-governor, yaani wale Regional Governors

na kuteremka njini. Na labda kwa kuendelee yule Rais, Ceremonial President, au ule uwajipikaji zaidi wa nchi ili asipendelee upande mmoja, awe ni Rais ambaye hatasimaia chama chochote cha kisiasa, achaguliwe tu. Lakini asisimaie masilahi ya chama chochote cha kisiasa. Yawe majimbo ya namna hiyo.

Ya pili ni kuhusu hizi maeneo za uwakilishi bungeni: Yaani zile constituencies, tumeona ya kwamba kuna zingine ni kubwa kubwa mno, hivi kwamba wale wabunge wanao chaguliwa wakati mwingine wanakosa kuajibika na wanalalia upande mmoja. Kwa mfano tukirudi hapa Malindi Constituency, imeanzia kule pwani na imeenda mpaka almost huko na mpaka na Voi kabisa . It is too big. Kwa hivyo kimaoni, labda ninasema ya kwamba, Electoral Commission, ikaweze ku-review, ku-revervive hii, wafanye review, na zile places ambazo huwa zinatumika geographical na population, igawanywe mara mbili, kuwe labda tutapata kitu, pengine Malindi Town Constituency na Malindi Rural, ili kuhakikisha kwamba kuna wambuge hasa ambao watahajibika kutumikia zile constituency zao.

Ya tatu ni kuhusu zile defections, yaani wale wabunge ambao wana mtindo wa kuhama vyama vyao in the course of ile tenure ya miaka mitano. Maoni yangu ni kwamba, ikiwa itakuwa hivyo mbunge inaonelea ahame chama chake, basi asifanye hivyo kule mara moja kabla ya ya ku-consult wale watu wake. Arudi kwa wale watu wake, na awaelezee na wale ndio watakao mpatia ile mandate ya idha ya ku-defect ama kufanya lolote. Otherwise akifanyia hivyo huko, bila wale wananchi wake kujua, basi asiruhusiwe kabisa kusimaia au kugombea hicho kiti.

Na hawa wambuge, wasiowajipiga baada ya kuchaguliwa, wengi tumeona wana mtindo baada ya kuchaguliwa, wanaenda kabisa kule Nairobi na wanakaa kule na wanabaki kule bila kurudia hao watu wao kuja kuaangalia taabu zao. Wanabaki kule kwa ile miaka mitano yote na wale watu wanateseka. Kwa hivyo kimaoni nasema yakwamba, Katiba hii tunayoiunda, iwe na kifungo cha kwamba, wale wananchi wenyewe, wawe wanaweza kumwita mbuge wao na kuja kumwangalia baada ya kipindi kwa mfano miaka miwili. Wamuangalie performance yake. Je ametimiza? ama anategeleza ule wajibu aliopewa ama namna gani? Ikiwa hawajibiki yule mbunge, basi kuwe kuna kifungo ambapo wananchi wenyewe watakuja kusema no, wewe hatukutaki, tunataka mtu mwingine. Lakini ile mambo ya kuja kudanganya danganya, kuonga apate kura, aende, aende kabisa, mpaka ile miaka mitano arudi tena na pesa zake za kuonga, hiyo ni mbaya.

Na ya mwisho ni kuhusu ile mishahara yao hawa wambunge: Tumesikia na tukaona ya kwamba mishahara yao sasa aina haja ni wakae tu dakika kumitano, hike ya five hundred per cent. Hii ni pesa ya umaa. Na kwa hivyo, ikiwa ni kuongezwa, mimi napendekeza Katiba hii, kuwe na Parliamentary Commission ambayo itashughulikia mambo haya. Si wao tu kukaa pale baada ya dakika tano kujadili, na waongeze mshahara wao asilimia mia tano. Hii ni pesa ya umaa na ikiwa ni kuongeza mishahara basi Commission ile, iwe inaweza kukaa na kuaangalia kile kiwangu ambacho ni sawa sawa kinaweza kutosha kwasababu kwanza zile siku wanazo fanya kazi kwa mwezi ni siku kumi na pili, twelve technical days za kufanyia ile kazi, na tukiangalia wengine kwa mfano Matiba, vile alivyo kuwa akihutumu, nikuingia tu na ku-sign na anatoroka. Kwa hivyo baadaya mwezi, ni kama amefanya kazi kwa masaa kidogo. Anapata elfu mia tano na kuendelee kule. Hiyo si haki hata kidogo. Public funds,

kwa hivyo hayo machache Asanteni.

**Com. Riunga Raiji:** Asante sana na yule mwingine ni Faraji M. Mulewa. Bwana Faraji karibu.

**Faraji M. Mulewa:** Asante Bwana Commissioner, kwanza nitashukuru kikao hiki lakini kuna mambo mengi mbayo tumeyakosa. Hasa kwa hawa Wananchi, hawajapata mafundisho ya kutosha ili yale maoni yanapotolewa yawe yana huzani wa kutosha. Wengi wanazungumza lakini ninavyo fahamu mimi, Sheria ni kitu ambacho kesho kinakufunaga lakini hapa ukisema ukisimama unazungumza lakini kesho kinakurudia na kinakufunga. Unarundi tena wewe unaanza kulia kwa hivyo mimi naomba kwamba kwanza kupitia kwenu, mafudisho hayajakuwa ya kisawasawa. Na inahitajika iwe watu wataelimishwa hali ambayo itakuwa ni nzuri kwasababu tunataka kuijenga Kenya kwa hali mpya tena, ukweli ama si ukweli? Na ikiwa tunataka kujenga Kenya yetu, ili yale malalamishi ambayo yako yametokea kutoka hapa na pale, hapo nyuma, iweze kuondoka, je ikiwa itaenda tu hivi hivi kama mchezo mchezo, jiwe hili la msingi tutakuwa tunataka kujijenga kwa njia iliyo bora ama ni ya kupotosha wengine?

Kwa hivyo mimi maombi yangu zaidi ninazizitiza, Wananchi, kwanza watu ni kidogo, kuna wa Lango Baya, hawako, wako hata wa Chakama, wanasitahili nao kwasababu hii ndio Center, iwe serikali imegharamia mafundisho ya civic education katika kila wilaya ili wanainchi waweze kufahamu vyema wanayo yazungumzia.

Wale wanaofanya kazi ya serikali wanaumia sana, na wengi inakuwa hivyo, si walimu, si ma-Officer hata wengine ni ma-Chief hata ma-DO. Wengi wa serikali wanaisha tu hivi kwasababu, kwa sababu hawapati hile haki yao na hawaangaliwe na serikali iko. Ilo ombi Bwana Officer ambaye ni Commissioner nataka lichukuliwa kwa uzani. Na wale wenzangu ambao wametangulia, ile memorandumu ilitolewa na Bwana Gandi, ifatwe vile ilivyo, kwasababu tuliikalia kwa njia ambayo ni nzuri lakini tatizo ni kwamba kuna upande mwingine tumesibiwa, kwasababu Katiba ile ya kwanza kama tungepewa, tungekuwa na ufahamu wa kwamba tungerekebisha zaidi wakati mahali fulani. Tungekata mahali fulani, lakini ni kama upande mmoja tumepewa mwangaza, upande mwingine tuko gisani. Ambao tunaangamia, tuko kwa shimo. Na hivyo hata tunazungumza lakini wengi wetu wafikiria ni ule mchezo, kwasababu mambo mazuri mazuri, kule bara inafanyaywa vizuri, ikifika pwani, inachukuliwa tu kama mchezo, kwa nini? Ambapo ni makosa, kwa sababu Kenya tuko Kenya moja na tunasitahili tuishi tukiwa kama wa-Kakamega atapata kitu fulani, pia wa pwani naye aeze kupata manufa yale yale. Lakini utasikia tu kwa radio, watu fulani wamegawiwa ma-Title Deed, bila hata mtu kulipa lakini Coast inakuwa ni shida. Ndiyo wengi wanalia, uma-squatter.

Mtu anaweza kuuwawa na ndovu hapa, na kuna haki serikali iko na jukumu na ione yule ambaye amepatwa na mziba ule alipewa ridha, lakini siku hizi, hata juzi, walikufa watu watatu hapa, na hata leo hakuna majibu yoyote. Serikali iko lakini hutekeleza ule wajibu wake inakuwa ni shida.

Mimi siamini hii memorandum ama haya maoni tunayatoa hapa kwamba yataenda kuchukuliwa kule. Inaweza kuwa tu kama

mchezo halafu dakika za mwisho, itapitishwa yale ambayo yanafwatwa na wale wakubwa. Maanake wako. Ninavyo zungumza wale masamaki wakubwa wakubwa, ndio wanatumiza sisi watu wa Coast. Kwa hivyo, mimi ninaomba na iwe itatekelezwa. Isipofanyika hivyo mimi nitaondoka lakini, wako watu ambao watakuja wafanye yale ambayo wanataka. Na itakuja iadhiri kwa upande mwingine. Lakini hatutaki hivyo tunataka serikali isiwe na choyo, isiwe na kuficha mambo ambayo ni Wananchi wayapate lakini iwe inaendeshwa tu ka mchezo mchezo. Juzi tulikuwa Kongoni, na hapa tulikuwa tumealikwa pia hivyo hivyo tuje hapa, kila mtu analalamika tu, hatujapata mafundisho ya kisawa sawa. Kwa hiyo tunaomba watu wafundishwe na waelewe. Ndio watoe maoni yao. Kwa hayo mengi ama machache, nitakomea hapo. Asante.

**Com. Riunga Raiji:** Asante sana. Mwingine ni Daniel Ngumbao, kabla ya Bwana Ngumbao kuzungumza, ningetaka kumhakikisha Bwana Lewa kazi ya mafundisho haijaisha. Hii itaendelea mpaka wakati ule kutakuwa na Katiba. Kwa hivyo kila mtu awe uhuru kuzungumzia shida zake. Sisi kama Tume tutajuwa kama vile tutaiaandika Katiba kwasababu nafikiri hata ingawa labda hamjapokea yale mazungumzo alikuwa akisema, kila mtu anajua shida zake. Na hata vile tumesikia asubuhi ya leo na wakina mama, wametoa maoni ambayo ni ya kikatiba ambayo ndiyo tunatafuta. Lakini tutaendesha elimu ya civic education. Karibu Bwana Ngumbao.

**Daniel Ngumbao:** Asanteni hapo nyote. Kwanza nataka nieleze ya kwamba bila majimbo Katiba.., kule nimeandika Ismail Ngumbao lakini yote mawili, Daniel Ngumbao ndiyo iliyoko katika ID number yangu.

Tunahitaji Katiba ya majimbo katika Kenya. Sababu ni moja tu, kwamba kila jimbo lijitegemee lenyewe kwa kila kitu. Ikisiangalia ID numbers zetu tulizo nazo, zimeandikwa, Chilore, Mafungoni Location. Instead of Chilore Matunguni. Kama angelikuwa huyo mhandikishaji wa wakati huo ni wa pwani, hangeandika Chirore Mafungoni location, angeaandika Chirore Matunguni Location. Imefanya confusion kwa kila identity card ya mtu. Mafungoni ni wapi? hakuna Mafungoni huku. Mtu wa pwani anajuwa herufu atakazoziandika kwa jina lolote la kila kitu. Wasumbuka hapa, mara akiita jina hata Magare hawezi kumjuwa, hawezi ku-try kutaja Mgare. Tukiwa na serikali ya majimbo, wabara watajichukua, watakaa, kama ni ma-hospitali, kama ni masukuli, kama nini, watajitengenezea wenyewe.

Rais tuliye naye sasa, mimi jina ni Daniel na yeye ni Daniel, kasoro mimi ni Ngumbao na yeye Arap Moi. Kama tungeweza kukaa pamoja, ningemwambia je Bwana huoni haya. Kutoka Lamu mpaka Vanga siko University ngapi hapa? Angenipa jibu, hangenipa jibu? Hangetoa jibu. Ma-university yote yamejaa huko, je kweli kama kweli kama kungekuwa na majimbo, sisi tuka hapo, mwaka wa thelanini na tisa huu, tukimaliza huu, tukiingia tatu ni miaka arubaini, pengine leo akisikia mayai wanatega huko, akisikia anaweza kabla ya hii December haijafika, apewe pahali fulani na makaende pakajengwe University. Anaweza tu maana yeye ni yeye. Maana kutoka mwenyezi Mungu ni Rais hapa Kenya. Ni kweli si kweli?

**Audience:** Kweli

**Daniel Ngumbao:** Sasa basi tukiwa na majimbo, hile Uatalii College iliyo Nairobi na ikae huko huko. Hiyo pwani ma-hoteli ni mangapi?

**Audience:** Mengi

**Daniel Ngumbao:** Kwa nini utalii College ikasome bara? Tunataka majimbo, majimbo, serikali iwe ya majimbo. Ni Ujaluo jimbo lake, ni ukambani jimbo lake ni huko sijui kwa Kalenjine jimbo lake, hawa katika, hawa wakikuyu jimbo lao, kila watu wapange katika jimbo lao. Kitakacho patikana katika jimbo, ishirini na tano za mia ziende ofisi kubwa, sabwini na tano katika sile mia sibaki katika lile jimbo. Wajifaee wenyewe. Serekali iwe ya nini, andikeni serikali ya majimbo.

Barabara hizi, budget zikitolewa za barabara, ma-bilion ya pesa kila mwaka yanatoka, angalieni. Watali wengi wako pwani barabara haziko. Wanataka kuja wana moyo, wakija wikilala wanalipa, wakilala town huko wanalipa lakini wakienda barabarani, gari laende pole pole kwasababu ya barabara mbovu. Kila jimbo lipange mambo ya barabara zao.

Hapa wengi wamesema mnazi hapa. Mimi nilikuwa Siera-leon vita vya pili vya dunia, Siera-leoni kunagemwa na kuna factory la hile tembo la mnazi, ukienda unaweka na una utapata karatasi, malipo yakifika utalipishwa. Hapa hawezekani. Miaka thelanini na tisa hakuja fanywa factory yoyote ya kutengenesea mnazi. Bado na haitakuweko, hawataki. Hao juu juu mbaka mbinguni. Ilikuwa juu moja sasa ukisikisa ni juu, juu, juu kabisa. Ndio hawataki, tunahitaji serikali ya majimbo sababu ni kila jimbo lipange mambo yake yenyewe. Masukuli, ma-hospitali, kila kitu wapange wenyewe. Nitaanjia hapo. Yatosha hayo.

**Com. Riunga Raiji**: Asante sana mzee Ngumbao, tumeandika, sasa namwita Emmanuel Mwandenge. Ningetaka kuhakikishia Bwana Ngumbao kwamba tuko na makamishna watatu wa pwani na na wanafanya kazi pamoja na sisi katika Constituency zingine. Safari hii hakuna mtu amesaulika. Endelee.

**Emmanuel Mwandenge**: Asante sana Bwana ma-commissioner wageni wale wengine wote ambao wanashughulika katika hii kurekebisha Katiba. Asante sana. Kwa jina mimi naitwa Emmanuel Mwandenge.

Mimi ikwa ninsema hivi, serikali hii ambayo tunatengeneza ama Katiba hii ambayo tunatengeneza naomba iwe ya majimbo. Kwasababu kuuanzia wakati tulipata uhuru mpaka sasa, nafikiria jimbo la pwani limesaulika kabisa zaidi ya majimbo yote. Pengine kama wale ni ndugu zetu ambao mnaona ambao wanaweza kuwa wameumia kama sisi, ni wale wa North Eastern. Wale nafikiri tanaweza kuwa pamoja. Kwasababu hao na sisi hatuko mbali sana. Ni jambo la kusikitisha hata nyinyi ma-Commissioner nafikiri mtakubaliana na mimi na hata wale wageni wengine. Kuwa ukiangalia shule kama hii na ukilinganisha na zile shule ambazo ziko kule juu, tuko wapi sisi? Bado nafikiri tuko kwa Stone Age. Maanake hata nimeona wageni, hata sijui hata wakitoka hapa wakitaka kwenda kujisaidia walikuwa wanaenda wapi. Basi mjihulise, karne hii mbayo tuko saa hii, basi bado mpaka saa hii tuko katika institution ambazo ziko katika hali hii. Na wakati huo serikali ilipochukua uongozi ilikuwa

kila shule inaangaliwa masilahi yake. Je sisi tuliangaliwa upande gani. Kwa hivyo ni kuonyesha kuwa sisi tulisahaulika. Na hiyo ni jambo ambalo linasikitisha sana. Kwa sababu ukitoka hapa ukienda North Eastern shida ambazo siko Kakoneni ndizo ziko huko.

Na anajukua tulichonancho kwenda kutengeneza kwake tu, ni kama ameshika ngombe anasema watu wangu kamueni maziwa. Sasa yule Rais mwingine naya atakayeingia naya, atasema okey watu wangu na nyinyi nimemshikia pembe, kamueni maziwa, sasa wale ambao hawatapata nafasi ya kushika yule ngombe wanaendelee tu kupaki hivyo hivyo . Sijui wanakula mavi yale ya ngombe wamekunya na wale wengine wanakamua maziwa. Ni jambo la kusikitisha sana. Na nafikiria hata saa zingine, sisi kama kuanzia hivi leo, yale ambayo tunasema hayatachukuliwa vile ambavyo tunasema, basi nafikiri history inatuhukumu vibaya sana, kwa sababu mimi ninaona kule mbeleni watoto wetu watakuja kupigana na sisi ndio tutakuwa tumefanya watu wapigane. Na haita kutakuwa vizuri kama sisi ambao leo tunapanga, ikiwe na system ambayo itatuzadia halafu tushindwe kufanya hivyo. Kwa sababu ya kuwa yale ambayo tunayapitisha hapa leo yanaenda yanakaliwa.

Kuna jambo lingine ambalo linasikitisha sana. Maembe yanakushwa hapa pwani, unapata tender ya ku-export hayo maembe yanapatiwa mtu wa kutoka bara aje anunue maembe hapa Shilingi tano anaenda kuhusa embe kule ulaya uko mia mbili. Sasa yule mkulima ndio nazidi kuwa mia masikini. Kwa nini hii tender ya ku-supply ama hii licence ya ku-supply hiyo ya ku -export hiyo vitu isipewe huyo mkaaji au yule mkulima wa kutoka mbale mahali ile kitu nakushwa?

Tuna jambo la kushangasa sana, mnazi tunakatazwa hunaambiwa haufai, miraa inatoka kule Isiolo, inatoka kule huko inakuja mpaka pwani mingine inaenda mpaka Saudi Arabia huko inakuwa exported, na miraa ni ulevi kama mnazi. Lakini kwa sababu sisi ni watu wa pwani, tumeambiwa hawa ni wajinga, hata wakati tunautubiwa, kwa amani mkae hivyo hivyo na ujinga wenu. Yaani mkae hivyo na ule ujinga sisi tutaendelea kunyonya ile rasilimali yenu. Kwasababu ni jambo la kushangasa, unapata hapa pwani, Malindi hii unapata Title Deeds hasipatianwi. Lakini nenda Kenyatta esate, huko Mpegendoni, huko watu walipewa Title Deeds, kutoka masabini huku, inakuwaje serekali ni hii hii moja, lakini mahali pengine, wengine wanapewa Title Deed, wengine hawapewi. Kwa nini wale wa Kenyatta estate walipewa titile deeds. Ni sababu gani, ni sababu wale ni ukoo ya yule mbao alikuwa ameshika ngombe wakati ule anaambiwa sasa wewe nyonya, ndio hivyo sasa. Wakapewa Title Deed, kwa hivyo hizi top standards amazo tunakuwa nazo kwa hii serikali ya unitary imetunyanyaza sana sisi watu wapwani. Isipokuwa majimbo pekee yake ndiyo inaweza kutuokoa.

Na sikusema ati mimi nikisema majimbo eti ikukuwa eti mtu wa bara afukuzwe, apana. Kitu ni kwamba tunataka ile rasilmali inayotoka hapa pwani inufahishe watu wa pwani. Robo moja iende ikasimamie ile serikali kuu. Lakini robo tatu sibaki pale pale kutengeneza masilahi ya pale. Na nanina imani kwamba hata ingawaje mengi yamekuliwa tayari lakini yale kidogo amabayo yamebaki hata sisi nasi angalau tuonje. Maanake, ile keki ya uhuru ilikuja ikagawanywa halafu zile chembe chembe silizo baki, ndizo watu wa pwani na watu wa North Eastern ndio wakaambiwa ndio kuleni hii. Yale makombo, ndio ambayo sisi tumepatiwa. Kwa hivyo mimi siko hapa kutusi mtu yoyote lakini ni kwamba tunataka serikali ile ambayo itaangalia masilahi ya

watu wote bila kujali huwe unatoka wapi, unatoka Central ama North Eastern. Kwa nini kiwanda cha ngo'mbe cha kuchinja ngombe Kenya Meat Commission ijengwe Nairobi, na alafu ngombe zote sinatoka North Eastern. Sasa wewe fikiria ngombe unaitoa Garissa kule kwa gari, unaipeba mpaka kule imechoka masikini. Tena unaenda unaijinja. Hata kwa Mungu ninafikiri kuwa wewe utakuwa umeiumiza sana. Je! kama hicho kiwanda cha Kenya Meat Commission kingekuwa North Eastern si kutoka kwa mfukaji mara moja sinapelekwa pale sinachinjwa, lakini kwasababu kuna watu wako na personal interest, yaani ile hali yaku anataka yeye afaidike ndio unapata kiwanda kinaenda kujengwa Nairobi. Kwa nini maembe inatoka hapa na enaenda kuwa processed Nairobi ama Mombasa na maembe yametoka Malindi. Hayo mambo ndiyo ambayo yametufanya tumekuwa masiki sana. Na hiyo ndio njia ambayo ile serikali ya unitary tunaona kuwa haifai kabisa. Kwa sababu imetunyanyasa mda mrefu sana.

Sasa tunaomba hivi sasa tunavyo peana maoni yetu kwa nyinyi makamishna ambao mmekuja kuwakilisha ile Commission yote, basi mjue kuwa watu wa pwani leo wameamka na wamesema ile Unitary sort of Government hatuitaki tena. Tunataka majimbo na hiyo ndio itatuogoa. Hatutaki kufukusa mtu yeyote lakini kitu ni kwamba ni tushirikiane

Haya kuna jambo lingine la afya: Ni jambo la kusikitisha sana kufikia leo, unaweza kupata mgonjwa anatoka Gosi, anapebwa kwa kitanda, mpaka hapa anakuja kutafuta matibabu ama anapelekwa Malindi. Wakati huo, baada ya uhuru, basi tumesikia mpaka leo tuko miaka mingapi. Mingi sana, halafu watu mpaka leo wangali wanapebwa na kitanda kupelekwa ma-hospitali. Si hilo ni jambo la kusikitika sana. Kama mngekuja makamishena wakati wa El-nino hata nyinyi mngeshangaa sana. Sijui hata kama mngeona hii ni Kenya ama ni mahali pengine. Kwa hivyo kwa nini serikali iwe inaweza kupea madawa kwa hospitali zingine na zingine sinakosa madawa. Kuwa na hiyo hali ya uwazi ya kujua kuwa hii Kenya ni moja na kila watu wanahitaji mahitaji, kama ni hutuma ya afya wapate kama wale Wananchi wengine. Kwa hivyo hapa mpangalie sana Makamishna na muaandike vizuri in black and white na msisaau. Kwa sababu hizi shida ambazo tuko nazo, kesho mtoto wako pia anakuja hapa pwani na anatazipata hizo hizo. Kwa sababu kama mimi mtoto wangu atabebwa na kitanda hata wewe kama tukaa pamoja kule utabebwa na kitanda ukiwa mgonjwa na uletwe hapa hapa. Kwa hivyo hapo muaangalie sana Makamishna. Mwende mpeane vivile ambavyo tunawaeleza.

Hali ya kazi: Upande wa kazi pia iwe ina angaliwa kuwa, ikiwa ni kazi, wale wenye lile jimbo waanze kupatiwa first priority, yaani wawe ni watu wa kwanza kupata hizo kazi halafu wale wangeni pia ndio sasa wachukue. Sio kazi simetokea, ni vacancy ishirini, unapata wale wenyenji wanapata watu watano halafu kumi na tano ni wageni. Hata kama sijasoma, jameni unataka kuniambia, kazi ya rungu, watchman, basi hata kama sijasoma siwezi kujuwa hata kushika rungu jameni? Sasa inakuwa hata ile kazi ya watchman lazima mtu wabara ndio aletwe aje afanye hiyo kazi? Jameni, nafikiri kuna mahali mtu anafika anaambiwa enough is enough. Na hatungetaka kufika hiyo, maanake ikifika hapo ni kuwa sasa tuna-declaire war, na hatungetaka kuwe na war. Unajuwa kitu inayoitwa Civil war in baya sana. Kwa sababu tumeona within Rwanda na nchi zingine zimekuwa na shida kwasababu ya mambo madogo, madogo kama haya ya kunyanyasa watu fulani. Unapata kabila hii inaonekana ni minority ama ni ndogo. Kwa hivyo inachukuliwa ni ndogo kwa hivyo inachukuliwa kidogo, sasa watu wa pwani kama walikuwa wamelala,

hivi basi wameamka, na huu muamko hautarudi nyuma. Kama vile mlivyoona wakati ule wa section 2A kuondolewa ilikuwa shida, watu walipata shida na ikaondolewa, ikaenda, basi hata hivi majimbo is the right time we have majimbo. Not any other time, that is the only way tanaweza kuokoa Wananchi wetu hapa. Kwa hivyo nataka mwende, mwenda na huo ujumbe kuwa hiyo ndio system ambayo itauzaidia. Si kumaliza mwingine lakini ndio system ambayo kila moja atasikia kuwa haki yake imeangaliwa.

Halafu hii mambo ya MP's: Wakati wameenda mbuge, halafu wao wanakuwa na uwezo wa kuwa wanaweza kuaangalia mishara yao wajiongezee, hiyo iwe nje kabisa. MP's kuwe kutawa na Commission ambayo inaweza kuaangalia mishahara yao. Sio wao wanaketi tayari wanasema dakika mbili, wanapitisha five hundred per cent, hawa Wananchi wengine wanapata, mtu ameajiriwa analipwa elfu tano, elfu tano atafanyia nini, na wakati wanaenda kule dukani kununua unga, ule unga ambao yule anaye lipwa elfu tano ndio ule ule yule nalipwa Shilingi mia tano elfu anaenda kununua. Kwa nini sasa kuwe na hiyo hali? Ikiwa ni mishahara iangaliwe, iangaliwe kwa kila mtu, kama ni mwalimu, angaliwe, kwasababu wanaenda kununua vitu madukani, ama kwa soko, wote wanaenda kununua kitu bei moja. Kwa nini wao wawe wengine wanapata mshahara mia elfu miatano mwingine anapata elfu tano. Hiyo tofauti ya mishahara pia iangaliwe. Kwa sababu tunataka tuwe na Kenya ambao Wananchi wote wanaangaliwa hali zao pamoja.

Haya kuana hali nyingine, unapata kuna donors, mtu amejitolea, amesema kuwa anataka kujenga hospitali kwa mfano Malindi. Hiyo hali inakuwa sasa mpaka sijui Rais mpaka akubali, ama anamwapia yule donor, badaala ya kujenga hiyo classic hospital hapa, ipeleke Eldoret, huko ndio nafikiri inaweza kufaa sana. Hiyo hali pia tunaona si nzuri, ikiwa tumekubaliana majimbo, itakuwa wale governors wa lile jimbo, wanaonakuwa ni mahali gani kunahitaji msaada na ndio ule msaada ukikuja unawasaidia.

Kuna kitu ambacho kilitokea hapa Ngomeni. Kuna hospitali kuliwa inatakikana ijengwe na hata donor alitoa pesa nyingi sana, na hiyo ingejengwa na hata ingeshinda ile ya Kenyatta National Hospital, likini imekaliwa mpaka leo, iko kwa records tu kuwa itajengwe na pesa simepaanwa. Hiyo hali inatokana na huyo President. Huyu President awe Ceremonial. Hawe hana uwezo wa kuzuia mambo kama haya. Ndio hii majimbo ndiyo inaweza kutuokoa. Kwa hivyo zingetaka niendelee zaidi kwasababu nasikia nimechemka. Nasikia kuongea sana na wakati kuna wengine wanataka kuongea. Kwa hivyo ni asante sana na ninaimani kuwa ma-Commissioner na wale wengine wote watapeleka ujumbe vile tulivyo upeana. Sio ule unakuwa distorted. Mambo mengine yanabaki.

**Com Riunga Raiji:** Asante sana Emmanuel, nataka kukuhakikishia ya kwamba hii report itapelekwa na hii machine unaona hapa, tume-tape kila kitu umesema. Na tena tukiandika report, Sheria inasema kwamba, lazima tuizambaze katika kila Constituency. Kwa ile report tutaandika, tutaileta hapa, muangalie kama yale mlisema leo yako ndani. Kwa hivyo msiwe na wasi wasi. Mwingine sasa ni Abel Kazungu, hayuko, Harrison, hayuko, Sammy Fondo, Willima Azaa, hayuko, Peter Kumbadha, hayuko, nafikiri mwingine ni Kahingu Katana, Kuna Alfred Mbaya, ni wewe karibu Bwana.

**Alfred Mbaya:** Mimi kwa jina ni Afred Mbaya, mtu wa kutoka Chilore. La kwanza ni kuunga mkono majimbo ambayo ninayotaka.

Kitu kingine ambacho ningeta kuzungumzia ni kwa katika Location yetu ya Chilore, sisi mashamaba yetu yanakaa kwenye ziwa Chilore. Na katika ziwa Chilore, kuna vipoko vinakaa kwa hivyo mimea yetu inaharibiwa na katika ziwa hilo limepakana na msitu wa Arap kazokoke. Ambako kunaishi ndovu, kwa hivyo mimea yetu kila wakati ina matatizo, kuja ikilishwa na ndovu na tunahaitiwa kwamba mimea ikiwa imearibiwa kinamna hile, tunaweza tukalipwa. Na yale malipo ya kuwa tulipwi, hatuyaoni. Kwa hivyo ni kwamba tunanyanyaswa kabisa. Serikali inasema itatupa vya kulipwa kwa kuwa tumearibiwa mimea yetu, halafu hakuna lolote linalo fanywa, serikali hii ni ipi, ambayo tu unaahidiwa kuwa utalipwa kulingana na mimea imeaaribiwa halafu hatupewi. Kwa hivyo huwa tuna kandamishwa zaidi. Kulingana na hata matunda yetu, hatuna soko au hata kule ambao matunda tungeyapata kwenda kusukuma sokoni. Ni yale yale ambayo yanakanyagwa kanyagwa na ndovu na kulishwa na vipoko. Halafu hatupewi chochote, hule aharibifu hatulipwi chochote.

Kwa hivyo tunaonewa, zaidi kabisa. Kwa hivyo ningependa, kama hii serikali ni ya majimbo, pengine tungenufaika pengine mpango ingerekebishwa na pengine hata tukipatiwa matizo kama vile ya mashamba yakiaribiwa, halafu tunapata riziki yetu ile ya kulipwa. Maanake kama tutakuwa sasa tunaambiwa tutalipwa halafu ndovu hata wale watu wa Game, ambao huja wakawafukuza, nao wanasema sisi haturuhusiwi kubiga maaanake manufa ya Watali ambao wanaleta pesa hapa. Sasa zile za watalii, ikiwa sisi hatupewi, si kule mtu atitimia vile vile? Kwa hivyo mimi naona hii serikali ya majimbo ingetufa ikiwa pengine tungepata kurekebishiwa vile ambao pengine vile tutakuwa tukisukoma matunda yetu masokoni na kujinufaisha katika mashamba yetu na sisi wenyewe tunapata manufa pale pale. Sina zaidi ya kusema nitafika hapo hapo. Asante.

**Com. Ruinga Raiji**. Asante sana. Philip Muramba. Muramba yuko? Charo Kahindi, karibu.

**Charo Kahindi:** Nawasalamia nyote Hamjambo

**Audience:** Hatujambo

**Charo Kahindi:** Basi mimi nitajangia juu ya hoja hizi, ile nataka kwanza ni seriklai iwe ya majimbo. Kwasababu mtu akiwa na uhuru katika sehemu yake, yeye yuko na uwezo na nafasi nzuri ya kijifanyia mambo yake mwenyewe yale anayotaka. Si uende uulize mtu mwingine vile mbavyo wewe unataka wakufayie kwasababu, hukienda kama serikali itakuwa hii ya muungano basi ni kwamba mambo mengi huwa yanapitishwa kule halafu kile ambacho wewe unataka basi ni vigumu kufanywa, kwasababu ni wale wafanye mambo yao mpaka waone ya kwamba wametosheka halafu baadaye ndiyo wanakumbuka wewe. Lakini ikiwa ni yamajimbo itakuwa ni rahisi watu kukaa na kuamua mambo yao wenyewe wanayotaka kufanya na wanafanya tu mara moja bila ya kuukiza au hata kuomba msaada kule. Kwasababu kama mapato ya hapa ama rasilimali zote za hapa, mapato yote

yanabaki hapa halafu asili mia ishini na tano pekee yake inaenda n kwa serikali kuu. Zile pesa au yale mabado yote ambayo yatakuwa yamebaki hapa hiyo itazaidia zana kuimarisha na kunufaisha watu wa sehemu ile ambayo wenyewe wanakaa katika jimbo lile.

Kwa mfano tukichukua mfano wa shule kama hii, mtoto anasomea hapa vizuri, anapita vizuri, labda pengine anapata alama kama mia tano hivi, sasa unakuta amesoma hapa katika shule ambayo si nzuri, lakini mtoto akipita vizuri, basi hapa Coast au katika jimbo hili akuna shule ambayo anaweza akasoma. Inambidi sasa anapelekwa mbali ambapo hata yule mzazi ama jamii ile inaweza ikashindwa kumgharimai yule mtoto kwenda kule. Lakini sasa ikiwa mambo yatakuwa ni hapa hapa, itakuwa ni vizuri, watu wanakaa vizuri, wanagharamia hata kama ni malipo ya shule wenyewe, wanafanya vizuri mambo yao, hiyo itakuwa ni sawa. Kuliko ile ya kwamba mtoto atolewe hapa aende huko mbali, halafu hata labda pengine huyo mtoto anaweza kusoma tuu miaka mwili halafu karo inamshinda, anarudi haba, hajapata certificate yoyote, basi elimu ya yule mtoto inakuwa imekuwa mbure kabisa. Kwa hivyo ile ninaomba ni serikali ya majimbo kwasababu mambo yetu tutafanyia hapa haba na itakuwa ni mzuri kabisa.

Kuuziana na elimu, elimu ninaomba katika Katiba hii ambayo tunaitunga leo, elimu kuanzia shule ya msingi mpaka ya Secondary, hii iwe ya bure, serikali igharamia kwa sasbabu mtoto wa darasa kama la nane, ni vigumu sana kupata kazi katika mashirika au katika ma-office zote zile ambazo tunaziona. Kwa hivyo ukifika pale unaulizwa tu kisomo chako? Ni darasa la nane. Sisi tunataka watu wa alama hizi, basi wewe jaribu wakati mwingine. Kwa hivyo unakuta mambo kama hayo huwa yanazidi kusorotesha hali ya hapa pwani. Kwa hivyo mambo ikiwa serikali itashuulikia mambo ya elimu kuanzia darasa la kwanza mpaka kitatu cha nine, mtoto ambaye amemaliza kitatu cha nine, huyu anaweza akajisimia vizuri, na hata kama atakuwa ameaajiriwa mahali, au hata kama ni kujisimamia yeye mwenyewe, anaweza kujisimamia kwasababu tunaona hata wengi ambao wamesoma mpaka kitatu cha nine halafu mtu hata anaweza kujiendeleza mwenyewe kusoma masoma ya inje. Lakini unakuta mtoto wa darasa la nane, huyu akimalisa, akikosa karo ya kwenda shule, basi yule tayari huwa amekosa au ile tumaini limemtoka kabisa. Kwa sababu hajui anziee wapi na ahelekee wapi. Lakini ngalau akimalisa kitatu cha nine huyu huwa amegoma kielimu na huu yuko na njia nyingi za kuweza kujizaidia yeye mwenyewe. Kwa hivyo kile ninomba ni kwamba serikali iwe ya majimbo, na kila jimbo lijisimamie lenyewe na lifanye mambo yake lienyewe na kama ni asili mia ishirini na tano ya mabato ya lile jimbo, basi hiyo iende katika office kuu, lakini sio pesa zote ama mabato yote ya jimbo yanaenda kule halafu tena tunaomba kama msaada tena tuje tufanyie mambo yetu hapa. Hiyo ndiyo imeleta shida kabisa.

Barabara, ma-hospitali na elimu imesorota kwasababu ya mambo kama hayo. Tukichukua mafano nimesoma kwa Nation tusema kama miaka mwili iliyopita hivi, ya kwamba huu uwaja wa Malindi Airport, pesa zake simechukuliwa zikaenda kujengewa Embakasi Internationa Airport. Sasa tukiangalia pesa ambazo zilikuwa zijenge hapa, halafu zimechukuliwa na mtu ambaye alikuwa na uwezo au mamlaka fulani akasema ziende Nairobi mara moja sikajenge huko. Sasa hiyo ndio ni makosa kabisa. Lakini sasa, hata nilisikia tuu Mbuge akijaribu kutetea hiyo mambo lakini sasa kwa sababu pengine ilipitishwa na wakubwa, hata yeye hawezi. Kwa hivyo ikiwa serikali ya majimbo, jambo kama hilo halitakuwa likitendeka kwa sababu watu

watakuwa wanakaa wakifanya mambo yao na wakipitisha. Kwa hivyo kama ni mtu kutoka juu, aje na aseme, nataka jambo fulani, watu wanakaa hata kama ni hali ya msadaa, sasa itakuwa ni watu kwanza wanakaa na wameona hilo jambo ni sawa. Lakini, sio mtu mkubwa kutoka kule juu ahakize mara moja jambo fulani lifanywe na lifanywe, kwa sababu hakuna mwingine kule chini ambaye aliye na uwezo au hali ya kwamba anaweza akazuia. Kwa hivyo mambo kama hayo ndio ambayo yamezidisha kabisa hali ya maendeleo katika jimbo hili.

Ukingalia katika jimbo hili tunazo rasimali nyingi sana. Lakini sasa kuna ukuta fulani ambao umesiba kiasi ya kwamba watu hawana uwezo ule wa kwamba wangeweza kujiamlia mambo fulani na wajifanyie wenyewe. Kwa hivyo unakuta mambo yote yanafanyiwa kule juu halafu sisi imebaki tu ni hadithi, mtafanyiwa hivi, mtafanyiwa hivi na hakuna chochote ambacho kinatendeka. Kwa hivyo kile ninaomba ni serikali ya majimbo na kila jimbo lijizimamie lenyewe. Na wale ambao hawataki majimbo, wabaki kwao. Na hatufukuzi mtu, kwasababu sisi ndio tunataka majimbo na ni katika hili jimbo letu. Kwa hivyo wale ambao, kama mtu hataki, yeye abaki kwao tu, hatumlazimishi. Lakini kitu tunachotaka sisi ni majimbo. Kwa hivyo kwa hayo machache au mengi, basi Mungu awabariki.

**Com. Ruinga Raiji**: Asante sana, sasa tuko na Evans Baya, Evans Baya, Evans ako? Karibu.

**Evans Baya**: Nitazungumza kuhuzu hile hospitali: Tumepoteza watu wengi sana hapa, mtu nimgonjwa, gari ni zile kungojea, mpaka itoke Malindi, huku mgonjwa nazidiwa, ndio ikija, hiyo gari itapata ashakufa. Ni hilo moja tu ndio ninalo.

**Com Riunga Raiji**: Okey asante sana, Ali Omar, Bwana Omar, hayuko? Namwita Charo, Chengo Katembe, Mbaya Omwere, ako? Asanteni, Alfred Ngonyo, karibu.

**Alfred Ngonyo**: Mimi yangu nasema asanteni kwa kuitwa hapa siku ya leo. Jina ni Alfred Ngonyo Kasheru.

La kwanza ni kuhusu kazi kulinga na serikali yetu. Mtu ataajiriwa, afanye kazi kulingana na miaka hamsini na tano amalize. Akishamaliza, amesitaafu, kwasabu ni mkubwa, anawekwa katika cheo kingine. Wako wengi tuna wapata ma-radioni mtu amesitaafu na amekuwa kubwa pahali pengine. Tunao mifano, tuna wakubwa wengine, amekuwa mkubwa kwa idara fulani alipomaliza baadaya akatiwa mkubwa kwa upande wa nyama. Kenya Meat Commssion. Huu ni mfano ambao uko katika wizara nyingi za serikali, tunasisikia.

Lingine ambalo naweza kuchangia hapo ndani ni kuhuzu time kwa upande wa ma-judge. Kwa sababu Judge ni mkubwa ama kulingana na cheo chake cha kazi, anaweza kufika pale kwa siku moja , ajudge kama kesi mbili ama moja, time ya kazi pengine ni sa mbili, aingie kama saa nne. Kulingana na kesi yenyewe ikisha, lunch time ishafika, anaenda, pengine unatoka Longo Baya, Chakama, mtu anaambiwa kesi yako imeairishwa mpaka mwezi uchao darehe fulani.

Tukiaangalia uchumi wa Kenya tunasema umesorota, kwasababu nafasi za kazi hakuna, hiyo pia ni shida ya hapo moja. Sasa mtu kama yule ametoka Chakama ticket yenyewe amefanya ya kukopa, leo hii anaambiwa njoo mwezi wa tano tarehe saba. Malindi hana mtu wake anaweza akalala pale. Imekuwa ni shida tena pengine kukopa kukopa arudi kwao Chakama. Je! pale tutakuwa tume zaidia ama ndio tumeua katika serikali hii yetu?

Lingine ambalo liko hapo ndani ni kuhusu upande wa Tourism

**Com Dr. Nunow**: Alfred, tafadhali baada ya kusema shida, tupatie pendekezo lako, kwani hiyo ni kile ungependa kifanyike.

**Alfred Ngonyo:** Sawa lingine ni upande wa kuhusu tourism. Tunasema wakati huu hatuna wakeni wengi. Kulingana na hali ya uchumi. Hatukatahi, lakini kwa wakati huu shinda kama hiyo iko saa hii, mimi ni moja wao katika tourism, ni mpishi, siwesi kusema ni uzuri lakini ni mpishi. Saa hii ukingia Malindi kuna hoteli fulani pale. Wanalipa mshahara wa three thousand six hundred and no house allowance, no transport, unatoka jikoni saa tano, saa sita, unatoka sehemu za beach mpaka Kisumu Ndogo kwa mguu. Ukiangalia wakubwa, si Ngonyo ni mtu aliyetoka huko juu. Kama vilivyosemwa hapo kwamba chuo kuu kiko Nairobi cha Utalii, mimi pia nimepelekwa huko, lakini mavuno hatuyaoni. Saa hii nina certificate ya kule ma-hotelini na certificate hata ya Utalii. Itanizaidia vipi? Ikiwa nitaenda pahali na nilipwe mshahara ya Shilingi elfu tatu mia sita? Mgeni moja ikiwa asubuhi anakula mia nne, lunch time anakula mia saba, jioni anakula mia saba, elfu moja mia nane usiku, haja lipa, Je tufanyeje?

Sasa maoni yangu napendekeza hivi, kama tungelikuwa na faida ya tourism, tungependekeza ama maoni yangu ningependa shule kama ile ya Utalii ingejengwa pwani. Kwasababu saa hii mimi siwezi kusema ujuzi wangu unafaa, je kama mimi ujuzi ambao ninawo saa hii, ningekuwa ninafanya hapo ndani kama ingelikuwa shule hapa karibu. Tunaweza kufunza hata wengine ambao wanasunguka hawana kazi. Mimi nikiwa nina certificate hiyo na haiwezi kuniokoa, ambaye hana kabisa atafanyaje?

La kuongezea hapo, ni kuhusu upande wa ardhi. Watu wengi wanabishana kwasababu ya makao ni kidogo. Lakini tukiangalia serikali yetu ya Kenya ambayo tunayo, makao mengi yamepewa wanyama wa porini na uwesi songa huko, ukienda kule za ingine wewe ni mwindaji haramu. Lakini miguu mitano mtu anaishi, mkisonga sana mwakosana. Hapo pia naona walifikirie kama jambo hilo. Yangu ni hayo tu asanteni.

**Com. Riunga Raiji:** Asante sana huyu alikuwa ni Alfred Ngonyo. Mr. Kathea

**Mohammed Kathea**: Mimi kwa jina ninaitwa Muhammed Kathea, na niko mbele yenu ma-commissioner kutoa maoni yangu kama ninavyo pendekeza.

Kwanza nataka niunge mkono yale yote ambayo yamezungumzwa kuhusiana na mambo ya pwani. Sitarudia mambo ya pwani

kwasababu yameongewa vya kutosha. Lakini nataka nizungumze mambo ambayo pengine yatanufaisha nchi nzima.

Kitu cha kwanza katika upande wa Urais: Ningeomba kwanza, Rais asiwe Mbuge, hayo ni mapendekezo yangu. Kulingana na uchaguzi wa Urais vilevile maoni yangu yanasema ya kwamba, uchaguzi wa Rais usifanywe sambamba na uchaguzi wa wabunge na madiwani. Ikiwa ni uchaguzi wa Rais ufanywe siku zake na uchaguzi wa mbuge na mwadiwani ufanywe siku zake.

Katika upande wa vyama vya kisiasa: Moani yangu ni kwamba vipunguswe na ikiwesekana viwe viwili tu. Kwasababu hivi vyama vya kisiasa, vimekuwa vingi kusidi na vemeanza kutatanisha watu. La kwanza vimetokesa hali ya kwamba ni vya ukabila, kwamba, maana kila kabila sasa linaunda chama chake. Kwa hivyo watu ambao hatuelewi, tumebaki kutapatapa hatujui twende chama gani. Kwa hivyo pendekezo langu viwe vyama viwili. Nafikiri kile kitakacho unda serikali kitakuwa kiko, lakini kitakacho kuwa cha upinzani kiwe kimoja kiaangalie ile serikali inafanya nini. Hivyo tu.

Pia vile vile upande wa uchaguzi mtu asiruhuziwe kuteuliwa na chama kingine napokataliwa na chama chake, kwasababu hiyo imekuwa ni kawaida. Wakati wa uteuzi wa wa Bunge ama madiwani, Mbuge akiwa chama fulani, na akikosa kura kule za kutokuteuliwa, anakimbia mara moja naenda kuteuliwa chama kingine. Nafikiri kungekuwa na kifungu cha kukataza kabisa ikiwa wewe ni mwana chama wa chama fulani, na ukikosa uteuzi iwe ni shauri yako umepoteza.

Kintu kingine ambacho ningetaka kupendekeza ni upande wa ardhi: Kwa hakika upande wa aridhi, pendekezo langu ni kwamba, ikiwesekana kuwena kiwango fulani cha hekari ambacho Mwananchi momja anasitahili kumiki. Kwasababu utakuta hivu sasa tunazungumza kwamba tuna ukosefu wa ardhi, hatuna mahali pakulima, lakini mtu pengine moja, ana hekari karibu mia tano mia sita na hasifanyi kitu. Ni zake tu katika Title Deed, anaenda anaweka kwa bank, anachukulia mkopo na ardhi inabaki vile vile. Lakini ikiwesekana ikiwa kutakuwa na kiwango fulani cha ardhi, ambacho mtu anasitahili kumiliki, nafikiri hata hili tatizo la ardhi, linaweza likamalizika. Mapendekezo yangu ni kusema mtu binafsi, nasema mtu moja pengine na familia yake, kama ingeliwezekana, kile kiasi kikubwa zaidi, kiwe angalau hekari thelathini. Hekari thelathini mtu na familia yake anatosheka kabisa.

Mwisho, au si mwisho, lakini pendekezo lingine ni kuhusiana na hi gap ya aidha naweza nikasema ni ya mishahara ama ni ya utajiri. Hii gap ya mishahara naona iko tofauti sana. Kama wenzangu walivyo zungumza kuhusiana na ile cap, unakuta hapa mfanya kazi anapata Shilingi elfu tano na pale mwenzake anapata shilingi elfu mia moja kwa mwezi. Hasa ile gap nafikiri ndio hata mara nyingi inaleta ufisadi, kwa maana ni shida kubwa. Kwa sababu kama alivyo zungumza mwenzangu, kile anachoenda kununua anayepata elfu tano kile anachonunua na yule anachonunua kwa shilingi elfu mia moja ni kile kile. Hata tukiaalia kuna mahali kwingine kunatutatiza. Tuaangalie kwa mfano katika malipo ya hospitali, mimi malipo ya hospitali nitalipwa shilingi mia tano kwa mwezi, mwenzangu pale atalipwa shilingi elfu tatu kwa mwezi, malipo ya hospitali ama elfu tano, lakini ugonjwa ukisikwa ni malaria ni ile ile tu. Yule awezi kushikwa na malaria kubwa na huyu akashikwa na malaria ndogo kwasababu ya zile pesa ni ndogo. Kwa hivyo nafikiri kungekuwa na kidogo, balance ya hii mishahara, naona ingetuzaidia sana.

Na mwisho kabisa, ni upande wa Chief's. Pendekezo langu ni kwamba, ikiwa Chief atachukuliwa kama mtumishi wa serikali mwingine, akiwa atachukuliwa kama civil servant, ambaye ameajiriwa na serikali, ile mipango inayo fanyiwa watumishi wengine wa serikali, hasa kwa upande wa transfers, ningependekeza uwe vile vile. Na hata ikiwa haitawesekana Chief kwa sababu inatakikana pengine aongee lugha kulingana na wale watu wake. Pendekezo langu ni kwamba katika transfers zao wakiwa wanaweza kuwa transferred internally katika ile district. Kwasababu tusema kwa mfano Malindi District, hakuna chief anayeweza kwenda katika Malindi District asiwezee kuongea lugha ya pale mahali. Kwa hivyo kama ni transfar's, hata kama haitaruhisiwa Kenya nzima, lakini katika district why? Awe anaweza kuwa transferred ndani ya district ile ili aweze kutofautisha zile huduma katika wale wananchi. Kwa hayo ninasema asante sana, karibuni sana.

**Com. Riunga Raiji**: Asante sana, Robert Chengo, karibu.

**Robert Chengo:** Kwa majina Robert Chengo. Kwanza kabisa nitaongea nikianza na serikali. Kwana napendekeza majimbo, hilo ni jambo la kwanza.

Jambo la pili: Nitaongea kuhusu upande wa Mbunge, ningependekeza ya kwamba, kuwe kutakuwa na yule Mbunge ambaye atakuwa amechaguliwa awe anatoka katika ile sehemu yao. Kiasi ya kwamba, wale watu ambao watakuwa ni wa area wawe wanamjua, na iwapo kutakuwa kuna jambo lolote ambalo si nzuri, wale watu wakule wanaweza wakatambua na wakamtumia yule Mbuge wa kule kwa ajili ya mipango mizuri. Na hiyo ni kwasababu, wakati mwingi tumeona kwamba mtu anatoka sehemu za mbali anakuja kuwa mbuge kama upande wa huko Coast, halafu hata areas zingine hasijui. Kwanza mtu kama huyo je, hii kazi ataifanya vipi ikiwa sehemu zingine hatahasijui hata majina. Kwa hivyo nataka Mbuge awe anatoka katika sehemu ile ile ya kwao.

Lingine, nitataja kuhusu barabara: Barabara kutoka Malindi kuelekea Tsavo, saa hii inajulikana kwamba inalami, lakini hakuna kitu. Sasa ningependekeza hivi, najua kuna pesa ambazo zilitolewa kwa ajili ya barabara hiyo, sasa kwa sababu ambayo imefanya mpaka hii barabara haijamalizika ni kwamba wale ambao walipatiwa ile juhudi ya kutengeneza hiyo barabara hawana mtu maalum wa kuchunguza. Kwa hivyo ikwa ni mradi mwingine hata bali na hiyo barabara, mradi wowote ambao utakuwa uko, mbali na yule ambaye atakuwa amepatiwa ile pesa, au hiyo jugumu, kuwe kutakuwa na mtu mwingine wa kujunguza je hilo jambo lilifanyika au alikufanyika na ikiwa halikufanyika, kuwe katakuwa na Sheria ya hata kushitaki yule ambaye atakuwa amepewa ile jukumu. Bila mtu wa kusimamia kuangali je kuwa jambo fulani limefanywa, basi kama ni corruption kwa serikali itaendelee.

Jambo lingine, kwanza nitaongezea kidogo kabla sijaenda kwa lingine. Kuna mfano ambao nitatoa na ambao pia umechangia kwa ile corruption iwe huo upande wa barabara. Tutatoa mfano mzuri, saa hii kuna watu wanaendelee kujenga hii barabara kutengeneza tengeneza, pesa ziko, na records wanaandika wale wakubwa wakijuwa kwamba pesa kama ni upande wa

mchanga, kama ni kutengeneza daraja, mchanga kiasi fulani, pesa imetumika kununua mchanga ni kiasi fulani, ama pengine ni mawe, pesa ni kiasi fulani. Sasa nataka niongee upande wa mchanga. Badala ya mchanga ununuliwe ili mtu ahaandike kwa record ya kwamba nimenunua mchanga wa pesa kadha, ili kwamba watu wajue zile pesa zinatumika vizuri, mtu anakuja kwa pengine anachukua mchanga kwa njia ama kwa shamba lako na hatakupatia hata kama ndururu. Na kwa sababu hutakuwa hujui, huwezi kuchukua hatua yoyote ile. Na huo ni mfano ambao umeendelea na hata saa hii AIC pale mchanga unachukuliwa na hakuna record ya pesa . Kule wana-record lakini wana- record ya kwamba pesa au mchanga wamenanunu, lakini hawanunui ile pesa inaenda wapi. Hii ni kuchangia hiyo corruption. Kwa hivyo kama kutakuwa na huyo mtu ambaye amechangia kusema atajunguza, jambo hilo halitafanyika. Kama ni mchanga umenunuliwa, hiyo pesa imetumika kweli, hakuna mambo ya kutanganya tena.

Nitaingia upande mwingine wa maji: Tumeona kwamba wakati mwingi mtu ananunu maji, kwa mfano, wakati mwingi huwa napenda sana, hasa upande wa waukulima, lakini huwa wanatumia maji kwa upande wa ununuzi. Ukitaka kunua maji, ya kufanyia irrigation, unakuta hapo, umeona kabisa hakuna ubaya ambao utakuwa umeoufnaya kwasababu hayo maji manayanunua kwa hivyo umeyapata kihalali. Lakini sasa watu wa maji, wakiona kwamba umenunua hayo maji, na umenunua mengi, anajuwa kwamba ile irrigation yako itakufaidisha, wanakataa wanakuzuia wanasema kwamba maji unaharibu. Sasa mimi naharibu vipi ikiwa nitatumia pesa yangu niyanunue yale maji kwa ajili ya irrigation ili nifaidike. Kama ningeyapata ya bure kama ningetumia njia ya kuiba pengine, hiyo ingekuwa pengine wangepata ya kuongea. Lakini sasa kama mimi natoa pesa zangu, kununua hayo maji halafu saa hii unasema maji, hutaki kwasababu utanufaika, sasa hilo jambo je sisi tutafanya nini? Kwa hivyo ikiwa kuna uwezekano kuwa kutakuwa na hiyo mipango ya kwamba Serikali ingie kati, akiwa mtu atakuwa amenunua kitu, hiyo, kitu awe ameipata na kuwe hakuna mtu yeyeote ambaye ataingilia kusema kwamba haifai ama si vizuri, Kwa hivyo jambo hilo kuwe kutakuwa na uwezekano wa kuangaliwa.

Lingine ni upande wa mahari: Tunaona kwamba upande wa mahari ni jambo ambalo saa hii limesumbua watu wengi sana. Kwa sababu mtu akitaka kuoa, mahari imekuwa juu sasa, kiasi ya kwamba si ile ya kawaida. Na ukisikia sababu ni kwamba mtu anasema mwangu mimi nilisomesha mpaka university, kwa hivyo hiyo mahari nitatoa kiwango kulingana na pesa yangu nilitumia. Sasa mimi ambaye nataka kuoa, kama sitakuwa na ule uwezo, hilo jambo litakuwaje? Kwa hivyo ninasema ya kwamba kama nikutakuwa na uwezekano wa serikali kuingia kati, hili jambo kuwe kutatolewa kiwango maalumu kiasi cha kwamba hiyo kitu iwe itazaidia watu. Na hili jambo nasema hivyo kwasababu, kuna mfano mzuri sana ambao nitautoa, kuna mwingine juzi ambaye alikuwa anataka kuoa. Na akambiwa atoe elfu themanini. Pesa hizi alimwambia mkwe wake sasa hii ni pesa nyingi. Akaambia kama ulielewana na mtoto wangu wewe lazima hiyo pesa ni lazima utoe kwasababu ni kiwango ambacho nimetoa na mtoto wangu nimesomesha. Akaambiwa basi kama ni hivyo ni sawa. Sasa yule alitoa pesa yake si kwamba alikuwa hana, akaenda akampatia pesa zote cash, mpaka zingine sikabaki. Likini sasa yule mwenye mtoto akasema basi kwani si vizuri, kwani pesa ya mahari haitolewe cash. Kwa hivyo inaonekana wewe kuna kitu hapo. Hizo zingine chukua nipatie shilingi elfu kumi tu. Je yule mwenye mtoto alipa nini? Tena inachangia kutoshirikiana baina ya yule mgwe na wazazi wa yule msichana. Kwa hivyo kwa ajili ya kuzaidiana hili jambo, serikali ingilie kati. Mara nyingine wasichana wengi wanakaa nyumbani wakizaa

huko kwasababu ya hii. Kwasababu mzazi wake amekata kupunguza hiyo mahari na watu wanakata kabisa kuenda hapo, na mtoto atazaa hapo hapo, si eti hatazaa, hatazaa kwa sababu wako uko nje. Sasa serikali ijaribu kuingilia kati iwapo kutakuwa kuna uwezekano kwa jambo hilo. Sina mengi. Asanteni.

**Com. Riunga Raiji:** Asante sana nafikiri amezungumzia juu ya vijana kwasababu ni lazima tusikize hata kushida ya vijana. Nafikiri wazazi mmesikia. Sasa Eliasi Misathe Kiundu.

**Elias Misathe Kiundu:** Kwa majina naitwa Elias Misathe Kiundu, kwanza ni shukurani hapo nitaitoa kwa Commissioners ambao mko hapa na wote ambao wamefika hapa.

Kwanza kabisa nitazungumzia juu ya serikali: Mimi pendekezo langu ni tuwe na serikali ya majimbo. Na mengi zaidi nafikiri kuhusu serikali ya majimo, wenzangu waliofika hapa wameongea. Kitu ambacho pengine taongezea hasa nitakusa juu ya ndoa. Ni kitu cha kusikitisha sana tukiangalia katika pwani yetu. Tunakuta kuwa kuna wazee ambao wana tabia ya kuoa watoto wadogo. Kwa sababu wana uwezo. Hali hii imeleta mahafa sana kwa watoto wadogo, kwa sababu wazee wengine huja baadaye wakakosana na wale watoto. Kwasababu mtu atakuwa ni kama ameoa mjuku wake. Yule mtoto hampatii hile raha, anaona aibu yule mtoto. Analazimishwa na wazazi wake kwasababu mahari imetolea. Kwa hivyo kitu ambacho ninachoomba naonelea ni vizuri ikiwa katika ndoa zetu serikali itahusika hasa ma-Chief. Kuwe kutakuwa kuna kuaandikiana kwa watu amabao watakuwa wanaoana. Kubunguza ile shida ya watoto ambao wao inawapaza wewe katika shule lakini wanakuwa wanaolewa.

Pili, nitaka kuongea juu ya kitu ambayo imeendelea na hiyo imeumiza vijana wengi. Watu wengi wa pwani. Ni uchawi. Serikali yetu haijatilia sana maanani juu ya kitu hiki uchawi. Tafadhali sana, naomba sana, mjue kwamba pwani imerekea nyuma kiasi kikubwa kwasababu ya kitu uchawi. Kuna viapo, viapo watu hukikisha kwamba huyu mtu ni mchawi. Lakini ni ikiwa ni hali ya kuwa sasa apelekwe mbele court huwa inakata. Na kweli ni kwamba hata katika bibilia zote tunajuwa kuwa uchawi uko. Mfano tumwangili Musa mahajabu ambayo alionesha watu, nyoka moja yule wake akamesa wote wale wa wachawi, huo ulikuwa ni nini, ulikuwa ni uchawi. Tunaomba serikali ione njia ambazo hizo sitakuwa, sita taliwa kwa wale ambao watashikwa na viapo wakiwa wameapa hawa wenyewe kwa viapo, kwamba waliua watu. Maanake wale huwa ni wauaji.

Kitu ambacho bia nitaongezea, ni elimu: Ni kitu cha kusikitisha sana kwasababu watu wengi wa pwani hawana uwezo wa kuelimisha familia zao. Nimeonelea ni vyema sana itakuwa ni njia nzuri serikali, baadaya ya hiyo serikali kufanya kitu kingine, ihakikishe elimu wanaisaidia sana. Hii inamanisha, walimu kwanza walipwe, kwa sababu walimu kama hawatalipwa, mishahara mizuri watakataa.

Pili wazazi wasipatiwe jukumu la kujenga shule. Serikali isimamie. Na ninaona ikiwa kutakuwa na serikali nzuri ya kusimamia elimu, Kenya yetu itaendelea.

Sehemu nyingine ni sehemu ya kazi: Ni kitu cha kusikitisha kwamba kwasababu watu wote wa pwani wengi wamelaliwa, utakuta kuwa kila mahali utakapo ingia, lazima uwe na mtu wako ndio upate kazi. Waweza kwenda kukuta mtu hata hawezi kuongea kizungu, au kingereza lakini ameaandikwa kwasababu ndugu yake ndio mkubwa pale. Tafadhali sana, tunaomba serikali ingalie kitu hiki. Yule ambaye atakuwa hana certificate ya kumuwezesha yeye kuaandikwa mahali asiruusiwe kufanya kazi hapo mahali. Pwani yetu imetegemewa katika Kenya hii. Bahari yote mzima iko pwani. Lakini ni kitu cha kusikitisha sana kuwa mtu wa pwani hanufaiki na bahari hiyo yote. Watu wa uko juu, Province zingine ndio wananufaika. Tafadhali sana tunaomba, ikiwa serikali itaangalia kitu hiki, tuwe na sisi tutanufaika watu wa pwani.

Na kitu ambacho hicho pengine nitaongezea zaidi ni kuusiana na hii misaada ambayo inaletwa katika Kenya yetu. Hapa sizungumzie pwani no, the whole Kenya. Katika huu mda hulio pita tumeshudia kuwa vyakula vinaletwa vya misaada, lakini tutaletewa vyakula vya msaada mpaka lini. Kwa nini kuna Mito na isitumiwe. Nina onelea ni vizuri ikiwa watu wa pwani mito ambayo iko hapa itatumiwa kunyunyuzia mimea. Njaa hiyo yote itaondoka, umasikini tutaupika teke, kuliko kila wakati tuwe tukiomba vyakula. Hii ni aibu.

Nafikiri nikiongezea zaidi kitu cha mwisho, madiwani: Madiwani inapasa wawe ni watu ambao wao wana elimu ya kutosha kwa sababu mtu akiwa ana elimu huwa ndio pia anaweza kusaidia wenzake, lakini ikiwa sasa huyo ndio mtu anaweza kusaidiana na watu halafu yeye hana elimu, inakuwa sasa ni bure. Kwa hivyo najuwa mengi yamezungumzwa na sitajukua muda mwingi. Shukurani naitoa. Asanteni.

**Com Riunga Raiji:** Hata Asante sana, David Kahindi, hakuna, Karisa Mwatete, Edward P. Kingi, karibu.

**Edward P. Kingi:** Asanteni sana kwa kunikaribisha, mimi ninaunga mkono kwa serikali ya majimbo na ninasababu, kwanza nitatoa habari ya ukulima. Hapa, ukulima tumesikia watu wakizungumza habari ya mnazi. Ninaunga mkono ile Coconut Act, kwasababu tangu wakati wa ukoloni tunajuwa kulikuwa kuna act ingine inakatasa Wafrika wasipande kahawa huko up-country, uko bara. Lakini ile ikaondolewa na hata wananchi wa bara wamekuwa matajiri kwa kupanda kahawa. Kabla ya hapo walikuwa ni wazungu peeke yao ndio wanaruhusiwa kupanda kahawa. Hapa kwetu ile Act ingaliko na huu mnazi umerudishwa nyuma. Na kisema mnazi sisemi ile pombe. Kwa wakati huu si tunaojuwa, tuna juwa ya kuwa hata uchunguzi wa Maendeleo ya mambo ya manazi hakuna. Hata ukienda kwa Research Station, utaona hapa Mtwapa wana tengeneza research ya miwa na hakuna mnazi huna tengenezwa research. Kuna mti kama ufuta ambao ni mmea wa mafuta sana hapa kwetu, kutoka Lamu mpaka Vanga. Uko number nane katika mipango ya serikali ya uchunguzi wa kufanya research kupata mbegu nzuri.

Kama ilikuwa ni serikali ya majimbo, kwa sababu hii ufuta ni mmea wa pesa wa jimbo la pwani, ingekuwa inaangaliwa hapa hapa. Na mnazi vile vile. Vile vile hapa kwetu tutaona miwa ilikuwa inapandwa mingi sana huko Ramisi na ikuwa ni utajiri wa

hapa, ukafaa kwa sababu ile Sugar Authority ambayo inasimamia mambo ya kupanda miwa inakuwa huko juu. Sasa wakasema hii sugari ya hapa si nzuri na ilikuwa imekaa miaka mingi sana. Kwa hivyo hapa kunaweza kukushwa sukari, kuna mtambo wa pikisa umekufa, na ni hapa pekee yake hapa pwani ambapo ule mmea unaweza kukuswa na nchi ya Peru huko America ya kusini. Na ulikuwa ni utajiri mkubwa sana kwasababu ile Cereal Board wakubwa wote wanatoka kule bara, basi wakangalia vibaya na pikisa umekufaa. Korosho vile vile imekufa, hii mimea ni cereal boards ambao wale ma-director wote na ma-chairmen ni watu wa bara. Kwa hivyo ingekuwa ni jambo, na tumaini huyu Governor amejaguliwa hapa pwani angejua maana ya mnazi ule mti, angejuwa maana ya pikisa kama vile wale wa juu wanajuwa maana ya pareto, kahawa.

Kitu kingine kule kuna cotton, coffee, tea, coffee and pyrethrium Boards. Hapa kwetu hii mti ya maana haina board. Kwa hivyo hatuwezi kuendelea, ndio tunaamini majimbo yangekuja hapa, tungeweza kuendelea.

Jambo lingine ni utalii. Utalii inaenda shambani na mambo ya ukulima katika kuleta pesa hapa nchi yetu. Lakini kama tumesikia wenzetu wakisema, college ni moja iko huko Nairobi na ukito Vanga mpaka Lamu ma-manager ikiwaona, wamesoma Utalii College na si watu wa pwani. Na kama ni manager anaandika mtu anaandika mtu wake vilevile. Kwa hivyo hapa kwetu ni rahisi kijana wa hapa kwetu kwenda Switzer-land mambo ya utalii kushinda kwenda kusoma Utalii College, Nairobi.

Vile vile tukiangalia ile majimbo tunakuja kwa upande ya elimu. Tulitaka Daktari afike hapa katika hospitali yetu, Clinical Officer, Medical Officer akatwambia mtafute kijana wa hapa anayefanya mahali popote katika Kenya, mkimpata tutampa transfar aje hapa Chilore. Hatuna hata moja na hatuna katika College. Kwasababu gani, kwasababu ile college hata iko Mombasa ya Medical Training College, lakini hata ukifanya application mpaka hufanya application Medical Training College in Nairobi. Na hawapati nafasi ya kusoma hata hapa Mombasa. Na ukienda hapa Mombasa, three quarters ya wale wanafunzi wanatoka kule. Kama ilikuwa ni jimbo la pwani na tuna college yetu hapa, tungewasomesha hapa hapa. Kwa hivyo hospitali zetu zinakosa wafanya kazi hapa hivi hatuna ma-daktari hapa, kwasababu hatunao na hatunao katika college. Na si kwamba watu wakusoma, wana elimu ya kutosha kusoma huko. Kwa hivyo hiyo ni mambo ya ardhi. Sisi watu wa chilore kuna watu kama elfu mbili ni ma-squater katika ardhi ya kanisa. Na ilitogea hivi, mwaka wa elfu moja mia nane tisaini wamishnari wa Church Missionary Society walikuja hapa Chilore wakaanza kanisa. Miaka kumi na mbili baadaya, mwaka wa elfu moja mia tisa na tatu wakanyakua ardhi ya hekari elfu moja mia tano, wakaandikana na Commissioner wa Lands Elliot's wakaandika Title Deed ya miaka tisaini na tisa, hii miaka tisaini na tisa inamalizika mwesi wa mei mwaka huu. Watu wa Chilore wamekuwa wa-squatter. Kuna barua kutoka huko kwa Bishop, kuwa tusipande miti ya kudumu na tusijenge nyumba za kudumu. Kwa hivyo tume kaa hapa hatuna nyumba za mawe, hatuna miembe, hatuna minazi hapa Chilore. Hapa Chilore ukitoka malindi ukiteremka hilo ziwa hutaona mti ya kudumu kwasababu ya ile Sheria ya kanisa. Je watoto wetu watakaa miaka tisaini na tisa mingine kwasababu kanisa inataka kurudia tena hiyo miaka tisaini natisa mingine. Tunasema hii katiba iangalie hizi ardhi ambazo watu walichukua kusinyakua kama hiyo.

Na tena wale walio sign ile karatasi na tumeiona ni Church Missionary Society, Sunsburg Square na Commissioner wa Lands

Kenya. Hakuna Anglican church imeaandikwa hapo. Lakini sasa Angilican Church ndio inatawala hiyo nchi , hatujui iliipata aje. Lakini hiyo inaambatana na zile nchi za Mazrui na zingine zile. Katiba iangalie wale ma-squater wa hizo nchi hizo. Je irudiwe tena wakapewe miaka tisaini na tisa? Sisi tunakata, tunasema Katiba itu-protect ili tuendelee kukaa nchi na tujenge vitu vyetu kama kawaida. Kama watoto wetu watakuwa ma-squater na wajukuu wetu vile vile kama wanapata mia tisaini natisa. Na hakuna maendeleo kanisa imefanya isipokuwa walikuwa wana-charge rent, mzee akilima shamba achukue mahindi apeleke kanisani. Mzee alikuwa nafikiri ya kuwa anapeleka kanisani ni tangizo kwa kanisa, kumbe alikuwa analipa rent. Kwa hivyo hiyo tunataka Katiba itu-protect. Kwa hivyo hiyo tunataka Katiba itu-protect. Asanteni sana.

**Com Ruinga Raiji:** Johnstone Katana. Toya Wachie and Muramba Toya, karibu Bwana.

**Muramba Toya:** Mimi kwa jina naitwa Muramba Toya Slyvester na niko na maoni tatu hivi. Kwanza, sisi wa-Kenya wote kabila mbali mbali, kabila zote ziko na ile tunaitwa mila. Kabila ni Mkamba iko na mila yake, mkikuyu ako na mila yake, mgiriama ako na mila yake. Mimi maoni yangu ni kwamba hizi mila lazima zingaliwe sana. Tukianza kusema kuusu hawa wagiriama wako na mila yao, hasa nataka nikusie kuhuzu uchawi. Uchawi imerekesha sana mandeleo hapa pwani na nikiendelea zaidi uchawi umerekesha nyuma maendeleo ni kwamba, watu wengi wemekufa sana Kenya kwasababu ya Uchawi. Uchawi sasa unaongoza hata kupita ugonjwa wa ukimwi. Kwa sababu hawa wachawi wamekuja wamefanya utafidi wao mpaka mchawi aweza akaroga mtu na akafa kama kwamba yeye alikuwa nahugua na ukimwi na hasa kumbe ni uchawi.

Hivi hapa mtahani wako badhi ya vijana wengi sana walikufa kwasababu ya kurogwa. Mila yetu iko na utafidi wa kuwa mtu anaweza kafwatwa katika mila mpaka akajukana yeye ni mchawi ama si mchawi. Lakini iko hali ya kuhusunisa sana kufikia dakika hii ya kwamba ukifika mtu kama yule ukimfanyia utafidi kumpeleka kwa Chief maanake Chief na Sub-chief katika eneo huwa wanajua zile mila za wale watu ambao wanaishi nao. Lakini tumifika kama hapa tayari Kakoneni, ma-Subchief na ma-Chief hawatili kabisa mkazo kuhusu hawa wachawi. Ukifika kortini kule hawawezi wakendelea zaidi kuchunguza zaidi mambo ya uchawi kwasababu wanasema hawawesi wakaangalia kuundani sana hayo mambo ya uchawi. Jambo ni kwamba hivi uchawi, wagiriama wako na ile kuaangalia kwa ujuzi mpaka mtu ajulikane ni mchawi. Maoni yangu ni kwamba hivi, watu lazima waangalie sana kuhusu huu uchawi. Kwa sababu huu nao unarekesha nyuma sana Maendeleo.

Nitaleta mfano moja ambao ulitokea juzi tu hapa Kakoneni. Hapa, huyu Chief na Sub-Chief wa hapa Kakoneni, walijunguza baadhi ya wachawi ambao waliwashika kabisa kuwa hao ni wachawi. Na wakapelekwa kwa viapo na wakajulikana hao ni wachawi. Wakaregeshwa hapa, walipelekwa mpaka kule ambako ndio watahakikishwa kweli ni wachawi na wakashikwa na ule uchawi wao. Baadala ya wale watu wapatikane na Sheria ya kuwa wamejulikana hao ni wachawi washikwe kwasababu hao ni wauaji. Tujuwa kabisa serikali ilitoa Sheria zake. Sheria ya mtu akiua yeye naye kule kortini anapewa adhabu kulingana na vile ambavyo yeye ameua. Lakini ninashindwa ya kwamba mchawi huku kwetu akishikwa ameua hachukuliwi hatua yoyote. Kwa hivyo ombo langu mimi ni kusizitiza ya kwamba, hizi mila siangaliwe zaidi. Kwa sababu hizi mila ziko na mambo ambao hayo si mazuri kama haya uchawi. Kwa hivyo naomba hizi mila zingaliwe zaidi. Jambo langu ni hilo.

**Com. Riunga Raiji:** Asante sana. Bonface Ruha, Frendia Nyundo, Bwana Nyundo yuko wapi? inaonekana hayuko, Alex Katenge, Charo Toya Karibu.

**Charo Toya:** Mimi jina langu ni Charo Toya Baya. Na maoni yangu ni kusema kwamba, hii mambo ya kura, na hii serikali tulianza zamani sana. Lakini hivi hivi vitambulisho tunauziwa tena tukipigia watu. Hiyo ni maajabu sana hii. Hawa wasimamizi wetu kwamba tumeyafikiria maoni yangu kwamba sasa wanasimamishwa kwa idhini ya pesa tu pekee yake. Mzee yule wetu wa zamani alipigania twaridhi mchanga tu. Sasa mambo ya kisasa ni pesa. Juzi garaji tunaonekana ya kwamba waliwa mfugo wa unga. Tena ukimalizika ule basi upati tena. Utaenda zako na utaumia na njaa yako vile vile.

Basi ndugu zangu, mfikirie sana serikali yetu hii ya majimbo. Tunasema tuna nyanyashwa kweli lakini mambo mengine tunafanya wenyewe. Unakuja tafuta kura hapa kumbe umesimashwa na mtu. Alafu wewe ukifika kule unauza plot zetu kule. Na mimi nimetembea wakati hule wa El-nino, nilikuwa kule upande wa Karashi, lakini nikafukushwa na maji hata pale pale mahali kwangu kulikuwa kama mtoni. Sasa nimeanza hapa mpaka Gongoni kwa mguu, maji hapa, hapa, ninafikiria mtoto moja wa hapa mwanamke, Albert Ngoye, amekuwa marehemu. Sasa nikwenda kule, basi wajomba wakina mzee moja kule Heri, amejaza gari tele warabu. Huku akija anatafuta hapo…… Kwa hivyo hilo ni jambo la kusikitisha sana ndugu zangu. Tujifikirie wenyewe katika nchi yetu hii, tunatafuta sasa, hatuchajua serikali itakuwa ipi. Tunataka majimbo. Pale zamani imekuja KADU, KANU, MWAMBAO zilikuwa vyama vitu kule. Lakini vikaja vikakuwa vipili tu. Haya tangu hapo tunafaidika na nini? Na tulie, kwanza wale wasimamizi hukienda sasa wanataka maoni yangu, mikirudi hapa picha iwe ile ile ya ule mchanga rythm ninayotaka. Si kuwa mnataka kubatilika, mnasema tunataka pwani ni yetu. Sasa tujue kwamba kibali kile, sijui kama huko wanafikiria watu tubadilishia kile kitambulisho, ama tutatumia kile, kile au tutakuwa na mabadiliko. Hiyo ikikafikiriwe. Tusikae hapa na kudanganywa saa zote.

Hatujakuwa na uhakika kwamba tutashika ipi, tukuwe nayo mkononi mwetu. Tunasema lakini wenzetu nao wako vile vile nao kutufikiria sisi. Hivi tunaambiwa kuna hivi. Maoni yangu mimi ni hao na sina zaidi.

**Com. Riunga Raiji**: Asante sana Bwana Charo, Zulubu Mdima, Bwana Zulubu Mdima? Bwana Tatu Kanata, sasa ni Kadho Valone, sijui kama imeandikwa vizuri, Angustus Phondo, Kenneth Misante, Kenneth, Peter Pondo. Okey.

**Pastor Peter Ponda:** Kwa majina yangu mimi ni Pastor Peter Ponda wa Kanisa la African Inland Church hapa. Ningetaka kutoa maoni yangu kwa ufupi sana. Commisioners ambao mmefika hapa, nafikiri tangu tulipoanza mazungumzo yetu, au mazungumzo ya kupokea maoni kutoka kwa wananchi neno moja tu limesimama. Na pengine umefikia wakati ambapo hata mimi naunga mkono neno hilo ya kwamba ile serikali ambao inaweza kutuzaidia katika nchi yetu hii ya Kenya ni Serikali ya majimbo. Mimi naona serikali ya majimbo ni serikali ambayo imetoka kwa Mungu mwenywe. Naona Mungu ndiye ameiruhusu. Kwa sababu ulifikia wakati Mungu akaruhusu serikali ya majimbo wakati wanadamu walipokuwa wamefika

wakati ambapo walikuwa wameanza kwenda kinyume cha mpango wa Mungu. Na ninaona ya kwamba serikali ya mmoja inachangia sana corruption ama hali ya upinafsi. Na huu upinafsi nafikiri ni jambo ambalo ni la kawaida. Kwasababu pakiwa mimi ni Mgiriama na kuna Mkiriama hapa, na aseme ya kwamba unaanza kutoa ile yako kwanza kabla ya mtu mwingine. Yaani iko is natural. Uwesi kuiondoa. Na siwezi kama pengine kuna mtu hapa na apata kazi kubwa mahali na watu wake kule nyuma wanatafuta kazi, it is naturally kwamba atatafuta watu wake aweke pale. Kwa hivyo kile cha kusaidia jambo hilo, ni serikali ya majimbo ili kila jimbo liweze kujiangalia na then kuwe na serikali kuu ambayo italeta ule umoja wa nchi yetu ya Kenya kwa jumla.

Na serikali hii inatakiwe iwe na Ceremonial President. Yaan Rais ambaye atakuwa na abit of Executive powers. Mimi napendekeza awe na a bit of Executive powers ambazo anaweza kua-point Judges, Chief Justice, wale wakubwa wa National Leaders lakini kuwa na Senate karibu na yeye. Ambayo hii Senate si politicians ni watu ambao wanachaguliwa kutoka kila mkoa. Kila jimbo. Kama ni majimbo manane, kila jimbo watu wawili wawili ambo wanenda ku-form ile Senate na President anapo-apoint mtu, lazima iwe confimed by the Senate. Ile kuwa na checks and balances. Si mtu ana-apoint mtu peeke yake na ienaenda hivyo hivyo.

Halafu baadaya ya Ceremonial President kuwe na Prime Minister, ambye huyu Prime Minister anatoka, ama ndiye anaunda serikali. Na Prime anatoka katika kile chama ambacho kimepata Wabunge wengi zaidi. Lakini pia katika Prime Minister, anakuwa pia chini yake kuna Governor ambaye huyu Governor ni Governor wa kila jimbo. Ambaye naye ana mbuge lake ambao wanaunda mambo yao, sheria zao na mambo yakiwa yamezidi, yanaenda kwa Prime Minister lakini pia Prime Minister asiwe na uwezo wa kuamua. Lazima kuwa pia kuna Senate mbayo pia inam-check huyu Prime Minister ili asiunde mambo yake anakapitisha bila watu kukubaliana. Hiyo ni muundo ambaye pengine tukiwa nao katika serikali yetu ya Kenya, tutakuwa na hali ambayo ni inaleta ule ule umoja wa kitaifa.

Na tukiangia upande wa vyama, katika vyama vile ambavyo ni vya kisiasa, mimi maoni yangu ni kwamba kila mkoa ama kila jimbo linaweza tu kujisimaia vizuri ikiwa limeundwa na chama kutoka katika jimbo hilo. Ikiwa ni jimbo la pwani kwa mfano, na limeundwa na serikali ambayo imetoka jimbo la mkoa mwingine, basi itakuwa hakuna tofauti, kwasababu ile faida ambaye inatoka katika jimbo lile kwa njia moja ama nyingine, kwa sababu jimbo litakuwa na mamlaka ya kuhunda Sheria zake. Na kama lina mamlaka ya kuhunda Sheria zake, ikiwa limeundwa, na jimbo ama serikali imeundwa na chama katika jimbo lingine, basi zile faida za jimbo hii, zitaundwa Sheria kiasi cha kwamba hizo faida ziende katika jimbo lingine kwa hivyo kila jimbo liunde serikali yake na chama chake.

Kulingana na mapato, nafikiri ni wazi ya kwamba kisheria serikali inatakiwa ifacilitate, iweze kusaidia Wananchi kutolala na njaa. Na kiwa nime lala njaa, nina haki ya kulaumu serikali kwamba nemelala njaa. Si kwamba kwamba nipatie heshima, aaa, lakini ifacilitate zile resources ambazo ninazo hapa. Niweze kufaidi na niweze kupata mapato ya kuweza kunifanya nisilale na njaa. Lakini ungaangalia hivi ni kwamba, kuna crops kama vile tumeambiwa mnazi, mgorosho, mwembe lakini kwamba serikali

hai-facilitate kuona kwamba inatoa market ama inatoa sehemu ambayo inaweza kuuziwa vyakula hivi ambayo tunatoa, ili tuweze kupata mapato yetu. Kwa hivyo tukiwa na Serikali ya majimbo, it will be automatic. Kwamba lazima lazima tutainua mnazi, mkorosho, mwembe na hivyo tutakuwa na maisha mazuri. Resources ambazo tunapata hapa tumekubaliana katika ule usemi, na mimi nakupaliana hivi ya kwamba, 25% inaweza kwenda serikali kuu. La ile 75% ibaki hapa. Tukichukua barabara vile ambavio tunasiona katika mkoa wa pwani ni mbaya sana.

Tukiangali elimu, ni baya sana. Lakini ukiangali mapato yaani ushuru mkubwa wa Kenya, the biggest percentage comes from Coast region, kama mkoa wa pwani unatoa katika ushuru wa Kenyan nzima kwa mwaka is estimated to be two hundred and nine billion shillings. Na fifty two billion shillings zinatoka mkoa wa pwani peeke yake. Hiyo inaweza kufanya mashule yetu, inaweza kufanya barabara zetu sikawa nzuri. Lakini kwasababu zote zinaenda kwenye Central Government ama zinaenda serikali ya Nairobi, halafu waseme ni wapi pa kupeleka na yule mkubwa pale si wa Coast si atapeka kwao, that is naturall. Kwa hivyo ni vizuri tuwe na serikali ya majimbo, ili tupeleke percentage kule na zingine sibaki hapa kuendeleza maisha ya Wananchi.

Hawa viongozi wetu ambao wanachaguliwa, kweli wasemaji wamesema hapa viongozi wengine wanachaguliwa hapa, halafu wakianguka wanaingia chama kingine. Inaoneka wazi kabisa kwamba, they don't have yaani hawana watu katika miyoni yao. Ni kazi wanatafuta lakini si kuzaidia watu. Kwa hivyo ile Sheria ya kwamba M'buge akikosa katika chama fulani, si alikuwa na lengo la kuwa katika chama hicho kwa sababu kila chama kina malengo yake. Kama ni Shirikisho kina malengo yake, kama ni DP ina malengo yake, sasa ukikosa KANU kufanya nini? Kwa sababu KANU kuna malengo yake pia. Inaonekana huyu mtu ni kazi anatafuta zi kuzaidia watu wake. Kwa hivyo mtu akianguka kule, asi-defect, abaki kule kule ambako ameanguka kama atazaidia atakaa nyumbani basi. Na ikiwa hafanyi kazi, kuna watu sasa tunaona ya kwamba baada ya miaka mitano, mwaka huu wa mwisho, ndio anaenda kuundwa party, wanaenda kwashurukuru watu wao kwasababu wemewachagua. These is a shame. Ni kuonekana huyu mtu amekaa miaka mine amekula, mwaka wa tano sasa anaenda tena kuwabembeleza watu, haya njoni Zoiya zile ambazo nilipwa wakati huo wote basi haya chukueni ngombe mle, mnirudishe tena kule niibe tena. That is the thing. Kwa hivyo mtu amebaki amekaa kule miaka kama miwili mitatu na he is not performing, kutolewe kipengele katika Sheria yetu ya Kenya ya kwamba mtu huyo aweze kutolewa na kura ya wananchi wenywe kwamba hatumtaki na asiingie tena.

Kunao uhuru wa kuabudu: Kenya yetu ina uhuru wa kuaabudu lakini nikiangalia, mimi nikiwa hapa naweza kusema pia kwa niaba ya Kanisa. Nafikiri hakuna uhuru wa kuaabudu kama vile ambavyo inasemekana. Hili jambo liwe very clear in the Constitution ya kwamba uhuru wa kuabudu, dini kama ni Christianity, kama ni Islamic isiwe interfered with wala ukristo usiende kuanza kubagua wengine na kapakua wengine na kuaanza kutukana wengine na kuaanza kutukana. Italeta vita vya kidini katika nchi yetu. Lakini kama ni wakiristo wakisima pale kwa jukwa, waongee bibilia yao mpaka waanguke pale. Kama ni waislam wasome korani yao mpaka waanguke pale. Lakini waslam wasisimame pale wakitukana wakiristo, na wakiristo wakisimama pale wakitukatukana waislam. Kutakuwa na vita vya kidini in these country.

Nasema kama ni uhuru wa kuabudu, kila moja aheshimu dini ya mwenzake. Kwa hivyo uhuru wa kuabudu uangaliwe kabisa katika Sheria zetu. Nasema hivyo kwa sababu it is an evidence katika mkoa wetu wa pwani, ya kwmba wakati mwingine hata last year but one, kuna Wakristo walipigwa mawe hapa Malindi mpaka wakaumia na wakaenda ma-hospitali na wakristo walipo enda kulalamika, hakuna hatua iliyo chukuliwa. Kwa hivyo naona hili jambo hawa viongozi wetu wa kidini, lazima tukubaliane ya kwamba sheria hii iwekwe, ili kila dini ipatiwe respect. Kwa sababu hata wale ambao hawajaokoka, hatuwe kuwatukana. Hao ambao hawajakuwa waislam, those people wa na miungu yao, basi wafwate miungu yao, lakini wakija upande mwingine wajiwe wafwate ile miungu mingine. Kwa hivyo huu uhuru wa kuabudu, uhangaliwe sana. Kwasababu tunataka nchi ambayo ina amani.

Mwisho nataka kusema hivi, ile mambo ya ardhi, ile Mazrui Act iondolewe…..yaan. 89 years whatever, mtu ana Title Deed yuko warabuni ama yuko ama sijui ni wapi, na hapa anamiliki ardhi, hiyo iondolewe kabisa. Na hii sijui ni Presidential sijui wahatever ambayo inasimamia front line ya beach, ni President mwenyewe anaweza kutoa, hiyo ilifanywa makusudi ili wale ambao wako juu wapeane watu wake hapa. Kwa hivyo hiyo iondolewe ili vile ardhi inapeanwa, ipeanwe kwa kila mtu kama kawaida. Na tukifanya hivyo naamini ya kwamba, tunatukuwa tunajenga nchi ambayo ni ya umoja. Kwa sababu majimbo si ya kwamba watu wawe divided, majimbo ni kwamba tuko mbali mbli we are different but we are united. Tuko tofauti kwa sababu tuko mila mbali mbali ama majimbo mbali mbali, lakini pia tumeunganishwa kwasababu zote tuko nchi moja ya Kenye. Kwa hivyo naunga mkono serikali ya majimbo, it's biblical, ni mpango wa Mungu ndiposa tumeupwa tofauti na tukapewa lugha tofauti tofauti, nikazaliwa nikajiona niko hapa pwani, mjaluo akazaliwa, akajiona yuko ujaluoni, mkikuyu akazaliwa akaonekana kumbe yuku kikuyuni that is God's plan. Kwa hivyo twende na mpango wa Mungu na utakuwa na amani Kenya. Mungu awabariki sana.

**Com Riunga Raiji**: Asante sana Pastor, sasa ni Slyvester Katana, ako? Slyvester, Alex Mworo, Alex? Muluma Festus, Kamoyoni Tamaa, ni huyu mzee, karibu mzee.

**Kamoyoni Tamaa:** Mimi sinamengi ya kuongea, hata nikiongea mengi ni ile ambayo imeongelewa tayari. Lakini nina shukuru sana eti nilipata hawa wengine wetu na kufundishana hizi Katiba zetu ambazo zinaendelea.

Mimi, kitu cha kwanza kile ambacho ningetaka hii Kenya tuangalie ni uhuru wetu uwe wa majimbo. Kila mtu akae jimbo lake. Kwa sababu mimi nina miaka hamsini na sita, na wakati tuliaanza kupigania hii uhuru, nilikwa nimesonga mbele, kifua mbele mpaka tulipata huu uhuru, nikasema labda pengine nitavaa nguo nzuri. Eeee! nikataabika kabisa. Nikaangamia, lakini nikiona wale wenzangu ambao wengi wako huko juu, aaa! nahusunika moyoni. Huko iko,aaa ikingia hapa, hata mtu na gari yake. Utaenda ugeti, nilienda Kajiado, nilikuwa na rafiki yangu hapo, nikamwambia je wakati hule naishi sasa, akasema uko kwetu sijui namnakani, kuleni maembe….. ile barabara aliweka lami mpaka nyumbani. Nikajua kweli kuna maendeleo. Na kwetu Maendeleo iko huku kwetu. Lakini tukaona, je ikiwa hii matunda inatoka kule kwetu nikisaliwa huko, sisi ni kuja tu kutembea

na kurudi, tunafaida gani? Nilijikuta, nilona niko tupu. Nikaona basi hazuru lakini jameni nyinyi mlikuja mkavuna mkarudi navyo kwenu, na walivuna, ningeonelea hata huu uhuru ukiwa wa majimbo, pengine na mimi.. sijachoka naweza kuaambiwa mzee hebu njoo hapa, maanaake hata mimi sijachoka.

Nina watoto wangu niwafundisha na wanasoma shule ni hizi Mungu yuko kule. Ukienda shule za uko, jameni sisi tuko na uhuru, na tunao kweli. Na yule mwenye uhuru utapata yuko na uhuru kweli. Lakini sisi hatuna uhuru. Ni kama kunyanyashwa. Maanake miaka hii yote ambayo niko nayo na hata sasa niko na miaka hamsini na sita, nimepika hatua kubwa mimi. Sina chochote, ninafikiria ni kwa nini mambo iko hapa. Hivi sasa nina banda langu nyumbani, lakini naweza kuja tolewa mara moja, ukaambiwa wewe hapa huna tite deed. Mwenye Title Deed ni yule aliye kule. Ni kwa nini hili jambo hilo walikuwa wanalifanya kutu-force sisi? Hiyo Sheria hiyo waliifanya ku-force. Si sharia ambayo kwamba ikuwa iko sawa. Maanake mimi ninakaa nina nasema hapa ni kwangu, kumbe bana mwingine. Ningeonelea kwa sasa ambao kwamba tunaunda hii Katiba mpya, hili jambo liangaliwe vizuri sana.

Kwasababu hii Katiba mpya ikiwa itaenda mpaka uko ambako hivi sasa tunaongea, tutapata kila mtu yuko na Title Deed yake. Maanake area hii iliesabiwa, tuko na ma-area mengi, lakini mtu anakaa nakaa kwasababu ni kwake, lakini si kwako. Hata mule town, moja nasikia vita vilianguka, anaambiwa hii nyumba yako vunja, hapa si kwako, mwarabu alikuja hapo mimi nilikuwa na Title Deed, ikiesabiwa Title Deed, je hatasijasaliwa, titile deed sikisajiwa mimi hata sijazaliwa, tena ulikuja pokonywa yule naye alichukua Title Deed ya babu yake.

Basi si Title Deed litetemea wale walio kule, sisi tuliohapa hakuna kitu. Hata umo town tayari. Hili jambo ni ambalo mkiondoka hapa mlifikirie. Na mkilifikiria na inaoneka wasi tupata sisi wenyewena na makao ya huku utapata mambo yanaendelea vizuri. Maanake hata nikiongea sana yote yameongewa. Kitu ambacho ni cha kufanyiwa hapa ni kutisama Katiba vile ambavyo tunaendelea. Kwa sababu watu wanaishi hapa na mambo yao yaangaliwe vizuri.

Na lakini ikiwa tulibahatika pengine, tukiambiwa huu uhuru uwe wa majimbo, kila mtu atakuwa anaendelea na jimbo lake. Si kwamba pengine, uhuru wa majimbo fulani wewe toka, fulani wewe fanya hivi aaa! Tuwe tuko pamoja lakini tujuwe tunatengeneza nini. Tukiwa tuko pamoja, tutakuwa tunaendelea vizuri. Maanake hiyo italeta mambo mazuri na mafahamikio mazuri. Maanake sasa naweza kuwa nina mgeni wangu, karibu Bwana, nasema tuingie, hapa ndio kwangu hapa, mara kutokee mambo meingine aaa! Hapa ndio kwa fulani, mwenye amekuja mwenye hapa, wewe mgeni wangu utaambiwa hapa sasa likini ni kwako, ni kwangu, nilijenga hii nyumba lakini sasa ni nyumba ndio yangu, ardhi si yangu, si tunaona tofauti. Lakini je ikiwa tulipata Title Deed sata najitengezea kwamba hapa ni kwangu. Kwangu kikamilifu, nitajenga vizuri ni sawa, nijenga vibaya ni sasa. Kwa hivyo ningeonelea kwamba hili jambo la Katiba ambalo tulikuja unda hapa Mungu atubariki nayo, na vile tumeongea hapa kila mtu ayapokee hii maneno haya. Maanake tumeona mengi, mambo mengi kufanya kuaambiwa wewe ukikubali ndio hivi, ukikataa ndio hivi. Maanake hata siku nyingine tuliona tu mambo yanafanywa hapa, kulikuja hata nikujiamrisha Bwana DO hapa. Nikambwambia, vile DO vile ambavyo vinafanywa hapo ni nini, akaniambia kwamba umesemaje, kwangu shambani

wanapewa mabunduki. Hawa ni wakina nani? Hapa tulikuja hapa tunataka tujue ni njia gani baya. Mana esabu sisi ambao hatuna naye. Maana wazee wengine wa kijiji ambao hatuna. Maanake watu wanakufa huku kwetu kwa mambo haya. Maanake mtu, yeye mtu anajikulia tu hanajiekea shambani kwa mtu anafanya hivi, anasema tunatengeneza mipango yetu mizuri hapa, na mtafurahia. Nikija nikiamrisha chief, ambao ni watu walioweka survey hapa na sasa hiyo itakuwa ni nyinyi mliita papato mazuri. Nikayafata na hata nikaambiwa hata zilipwi. Wanataka wafuge nyama, nyinyi muodoke. Hilo jambo liliniuma vizuri sana.

Mimi kwangu shambani niondoke, akae hapa nyama wa msituni, habaki hapa, mimi niondoke. Ni sawa kwasababu nyinyi ndio wakubwa. Hata DO nilimwabia hivi, ni sawa Bwana DO. Maanake nyinyi ndio wakubwa. Hili ni jambo ambalo linafanya ku-forsee wewe fanya hivi. Je kama ilikuwa ni kitu ambacho ni cha haki, singekuwa najuwa hapa ndio ninakaa lakini ilikuwa, ingawaje haijafanywa, lakini ninajua itafanywa. Kwasababu hatuna uwezo. Kwa hivi sasa ambao tunaunda Katiba, na tukielewana hali ya kisawa, utapata dalili pana uhuru. Lakini sasa niko juu juu, wakatikati ambaye yuko na matunda ndiye mwenye uhuru. Na ambaye hana matunda hana uhuru. Sasa sisi tunataka matunda yetu iwe kipali cha mashamba. Iwe ndilo tunda langu……….

**Com. Riunga Raiji**: Ngona Mboro, karibu.

**Ngona Mboro:** Asanteni sana kwa jina naitwa Ngona Mboro. Mimi nikiwa nimesimama mbele yenu, nikiwa nampongeza hiki chama cha majimbo. Kwasababu katika kujiendelesa wenyewe, naona kuna muhimu zaidi kuliko kuongozwa. Tukiangalia hata upande wa Maendeleo katika semu hii yetu, tuko nyuma sana. Tumekuwa nyuma sana kwasababu tukiangalia sehemu kama ya Lango Baya, kwenda mpaka Chakama, hakuna hospitali, hospitali ni Malindi. Kwa hivyo ninaomba kama itawesekana, tupate kituo cha afya karibu..

Pili ni ukaaji wa kule, tumekaa hali ya usi-quatter hivyo hivyo, us-squatter si hapa pekee yake, nimesema umeanzia Malindi town mpaka mashambani. Basi uma-squatter uko kweli. Kwasababu huko tuko na haya mambo ya Weru Ranch, ambayo tuelipishwa shilingi mia tano, mia tano. Mambo ya Weru Ranch yamekuwa zaidi ya miaka thelani nyuma tangu sijazaliwa. Mpaka sasa kodi hiyo bado inaendelea kukantwa.

Lakini tukumbukeni, kama itakuwa vizuri basi watu wa lands wakiwa karibu, muwalete karibu ili waanze kutukawanyia ile sehemu ambayo uko, ugawanyiwe hapo hapo. Hata kama mtu yuko Nairobi, amelipia Title Deed huko, na ni mtu wa bara. Kwasababu tunajua mambo ya Weru Ranch, watu wabara wengi wamejiandikisha. Na tumekuwa kama – squartters. Hakuna hata Title Deed. Tumekuwa zaidi ya miaka thelanini, tangu mababu zetu, na tumeridhi huo usi-quatter mpaka sasa. Na hata wengine vile tunavyo endelea kuzaa, hatujui kama wale watoto mbeleni kutakuwa kivipi. Kwa hivyo ninaomba serikali yetu ifanye hivyo haraka na igawanyie wale wenyeji pale walipo. Yuko na karatasi ile ya Weru Ranch mia tano, hawe hana, apatiwe pale pale mahali pake walipojenga.

Mimi nikiwa sina mengi ni hayo machache. Asanteni.

**Com. Riunga Raiji:** Asante sana. Elias Lewa. Nafikiri tutajaribu kufupisha kwa sababu tuko na watu wengi wamebaki na muda ni mfupi sana. Kwa hivyo ikiweza kufupisha tungeshukuru.

**Elias Lewa:** Wanainchi wenzangu hamjambo. Mimi pia nami nina maoni tofauti ambayo ninataka kuwapatia wapendwa wa tume maana tunashukuru mmetutembelea.

Oni la kwanza hasa, ningependa kuwaeleza ni kwamba, kuna mwenzangu amezungumza jambo ya kwamba kule kule kuwamazisha, Wananchi kuuziana na hii civic education imekuwa kidogo hali ya chini kwa sababu mimi kama facilitator wa uko sehemu za Mlango Baya, kwenda Chakama uko, kuna shida fulani ambazo hasa zinaitajika msijuwe na pia mkienda mkasizungumze. Shida ya kwanza ni kwamba, tumekosa ile njia ya kituinua ili kufanya hii kazi iweze kuwa nzuri. Kwa mfano, inabidii nitumie njia zangu zote na sina , no funds, hakuna kitu ambacho kinaweza kunizaidia.

**Com. Riunga Raiji:** Tafadhali ndugu Lewa leo tulikuja tu kusikiza maoni, mambo hiyo ingine ya civic education tutasikiza. Kwa hivyo sasa ni nafasi ya wananchi wenyewe, halafu watupatie maoni yao. Tunajua shida ya civic education lakini, kikao cha leo ni kusikiza maoni ya Wananchi wenyewe directly shida zao, tunajuwa problem ya hawa walimu wa civic education. Lakini hatukuja leo kwa hiyo kazi, kwa hivyo utaruhusu.

**Elias Lewa:** Asante . Sasa kina maoni ambayo yameaandikwa ki-memorandum kidogo kama ninaweza kupitia. Okey, maoni ya kwanza au oni la kwanza ni kwamba, haya maoni yametoka kwa wanainchi wa Mangongoloni, poleni hamjui Mangongoloni lakini ni sub-location ya Lango Baya.

Oni la kwanza wamesema ya kwamba, mfumo ambao wangeitaji wa serikali wametaka mfumo wa majimbo.

La pili, wakasema ya kwamba haya maoni ambayo tunayatoa, tunatakikana katika Katiba mpya tunayoiunda ijulikane kwamba tunayatoa sisi kama Wananchi wa Kenya, ili niwe na haki au na uwezo wa kutafuta kama hata kama jambo naliona haliendi sawasawa.

Kulingana na Katiba hii ya sasa, ambayo tunataka kuihiunda, basi mamlaka yasiwe kwa Rais zaidi kwasababu ya kiwa kwa Rais zaidi, kuna kuwa na kama upendeleo maana na vile nakavyofanya atakavyotaka anafanya. Na mara nyingi huwa anapendelee sehemu zile za kwao iliaone zinaendeleea. Kwa hivyo hayo mamlaka yawe yakipimo.

Katika Katiba hii ambao sasa tunataka kuifanya Katiba mpya, hasa uwezo mkubwa ama mamliaka makubwa yawe kwa

wananchi wenyewe. Pia kwasababu tumetaka mfumo wa majimbo wameeleza kitu fulani wakasema ya kwamba, kuna sehemu ambazo hasa ni za ardhi na wanainchi hasa wa kawaida hana uwezo wa kupata kimaendeleo. Kwa mfano, mimi nimekaa mahali pale, tangu Jadi, tangu babu yangu na baba na mimi sasa, na hata mashaidi wanaju wa kwamba, pale mahali ninapokaa ni kwetu.

Lakini sasa sifahamiki Kikatiba kwamba ninauwezo hata wa kutafuta kulingana na ile sehemu ninayokaa kimaendeleo. Pengine wenzangu wakiwa wana njia ya kwamba wanaweza kupata hata mikopo. Wanatumia zile Title Deed kuligana na ile aridhi waliyo nayo, lakini mimi, mwananchi wa wakawida ambaye sina Title Deed na nimwana Kenya na nimekaa pale, na hatakuna mashaidi ambao wanajua ya kwmba ile sehemu ni yangu, kwa nini hakuna njia au kuwe kuna njia ya kwamba, ninaweza kutambulika Kikatiba nami niweze kupata manufa kulingana na ile sehemu ninayokaa. Kwa mfano ikiwa kunatoka mikopo, na mimi ninahakika na kuna mashaidi ambao wananiithinisha kwamba pale mahali ni kwangu. Basi niweze kutambulika kikatiba ili niwese kupata nami njia ya kuweza kuniendeleza. Kwa sababu nina watoto nataka kusomesha, ninajamii wanataka kukishwa, na ni mwanakenya, sasa njia ambayo inaweza kunizaidia ni gani hata niweze pia kufanyanya nini kujiendeleza.

**Com. Riunga Raiji:** Tafadhali kawasababu wewe ni mwalimu na najuwa unaelewa, kama ungetupatia tu mapendekezo, kwasababu haya ndio tungetaka ili tuweke. Vile ungetaka tuyatatue hayo maneno. Wengine niwaruhusu wazungumze vile wangetaka. Lakini kwasababu hiyo ndiyo tunataka, ungetaka tufanya nini kwa Katiba ili tutaue hayo matatizo umetueleza.

**Elias Lewa:** Kwa hivyo sasa niendelee au nini?

**Com. Riunga Raiji:** Endelea.

**Elias Lewa:** Okey, kwa hivyo sasa wakataka kwamba maoni yawe kwamba ikiwa inawezekana, itambulike Kikatiba ili mimi pia nami niweze kupa msaada wa kuweza kujiendeleza. Pia wakanipa maoni ya kwamba kilingana na hali zetu za afya, kwasababu tunaishi sehemu ambazo ni za shida, basi maoni yetu katika Katiba yawe kwamba ile serikali iweze kuaangalia kama inaweza kutengeneza hospitali kufikia kiwango cha sub-location. Kila sub-location, ione kwamba ina hospitali ya serikali ambapo Mwananchi wa kawaida anaweza kupata matibabu.

Pia wakanipa maoni ya kwamba, kulingana na elimu, kwasababu ya shida nyingi, basi katika Katiba iweze kuorodheshwa kwamba hata mimi mwananchi wa kawaida nami niweze kutafutiwa njia ya kwamba watoto wangu wanaweza kusoma hata kama sinauwezo. Na Pengine mtayayona kwamba memorandum, kama mlivyosema kwamba mimi ni mwalimu na mengine mtayasoma. Asanteni sana.

**Com. Riunga Raiji.** Asante sana Mwalimu, ni kwasababu tuna watu wamebaki na tunataka kuwapatia nafasi. Safari Hare yuko, Bwana Safari. Kagende Kalama yuko? Kahindi Baya, Moses Mganga, James Ndolo, Katolwa Toya,David Genga,

karibu David, inaonekana wengine wamevutiwa na mpira, wakatoka.

**David Kenga:** Kwa majina yangu naitwa David Kenga. Mimi naunga mkono serikali ya majimbo. Na kwa mapendekezo yangu, nataka, hii Katiba mpya, kwanza kabisa jambo la ufisadi, tungelijaribu tukaona kwamba hii kitu tunamalizana nayo kabisa.

Na lingine ni mwanamke kuwa sawa na mwanamme. Hii ahiwezekani, kwa mapendekezo yangu. Maanake machana hauwezi ukawa usiku. Kwa hivyo mwanamke hawezi kuwa sawa na mwamme. Ni hayo tu.

**Com Riunga Raiji**: Teddy Taito Mazoea.

**Teddy Tito Mazoea:** Kwa jina naitwa**,** Teddy Taito Mazoea, na ninamapendekezo yangu. Kwanza mimi ningalipendelea kuwe na mfumo wa majimbo na katika ile hali ya kuwa na mfumo wa majimbo, kuwe na Rais atachaguliwa moja kwa moja na Wananchi kwa wengi wa kura. Kuwe na Governors Katika kila jimbo. Huyu Governor, yeye atakuwa anasimamia lile jimbo katika ile hali ya kuwa anatekeleza ile kazi yake na Governor awe atachaguliwa kupitia kwa njia ya kura, moja kwa moja na wananchi na awe anawakilisha katika umbuge sehemu yake anayo wakilisha.

Tatu, katika ile hali ya kuteua wale viongozi wa kama Tume, na mkuu wa Sheria, awe ana chaguliwa na Rais. Na wanachini wake wawe wanaweza kuteuliwa na Governors, wawe wana waankilisha majimbo. Kila jimbo liwe na mwanachini wa Mkuu wa Sheria. Upande wa Commission, Rais awe ana uwezo wa kuchagua Commissioner mkuu katika kila tume na wale ma-Commissioner wengine wawe watachaguliwa na Governors, kutoka kila jimbo. Na hapa katika ile hali ya kuchagu. Na hapa katika ile hali ya kuchagua viongozi katika hizi hizi Tume, kuwe kuna utaratibu unao takikana, yaani kuwe una usawa vile viti vikagawanywa njia ya usawa katika kila jimbo.

Katika hali ya kuchagua wenye viti wa Parastatals yaani, wenye viti wachaguliwa na katika kila jimbo, kama kuna Parastatals yoyote iliyoko katika lile jimbo, mwenye kiti, achaguliwe na Governor wa lile jimbo na Director wa lile jimbo.

Tunaingia katika Mbuge: Wambuge wanapochaguliwa na Wananchi, wasiende kukaa huko, wachukue yale mazungumzo yanayo zungumzwa katika Bunge wakishapata yale mazungumzo, warudi, kila mwezi wawe wanakuja ku-report katika zile sehemu wanazo wakilisha katika Bunge. Na wakikosa kwa miezi mitatu, zile nafasi zao, zitangazwe kuwa wazi.

Kwa upande wa matibabu: Unakuta sehemu kama hii yetu hapa Malindi, kuna sehemu zingine hakujaingia matibabu kabisa. Matibabu yako Malindi, mtu anaweza kutoka Mkondoni , hakuna mabarabara, magari ni ya wakati, mtu ni mgonjwa kwa hivyo, mtu anapokuwa mgonjwa inakuwa ni vigumu kitambo aje apate matibabu, kuna kuwa na ule ugumu. Kwa hivyo ningelipendekeza kuwa hizi hospitali hata kama ni dispensary, lakini siwe zinafika katika sehemu ndongo za Sub-Location.

Sifikie kiwango hicho.  Na ifanyike kwa uharaka zaidi.

Tuangalie upande wa ardhi:  Ardhi kila mtu anataka Title Deed, hakuna mtu hapendelei, kwa hivyo tuangalie upande wa ardhi hii, je mwnanchi wa kawaida kule interior, atakuwa na uwezo gani wa kufika mpaka aje afatilie ule mpangilio wa katika ile hali ya kupata umilikaji wa ardhi, mpaka afatilie step kadha mpaka afike Nairobi.  Kwa hivyo kufanya ile hali hiyo iwe katika ufupi zaidi, zile office za aridhi, siletwe karibu na wananchi kufikia kiwangi cha Sub-Location vile vile.

Tuaangalie upande wa passport pia:  Kuna watu kila mtu anaishi maisha ya kivyake.  Kuna  mwingine leo anataka kusafiri, kunakuwa na hali ule ugumu wa mtu kusafiri kutoka nchi yake  kwenda nchi nyingine, labda kimasomo, kikazi, kimatibabu na mambo mengine. Unakuta katika ile hali, mtu yuko interior huku, tuseme Mpondoni huku Sub-Location.  Je yule mtu anapotaka kusaidiwa katika ile hali ya kupata kile cheti cha kusafiri, kama passport hivi, afanye nini?  Inakuwa kwake ni ngumu, kwa hivyo serikali tunaiomba hii, hii serikali itakayo unda hii Katiba mpya itakayo tengenezwa ihakikishe kwamba office ya Immigration siletwe katika kiwango cha Sub-Location.

Tuingi upande wa administrators:  Hawa Administrators wetu tulio nao sasa,  ni sawa kuwa na Administrators wawe waweko kuligana na hali ya kazi.  Kuwe na DC,DO, Chief na Sub-Chief wake.  Na katika hali ya utekelezaji wa kazi zao, Administrators, hawa kwanza tuaanze na DC.  DC awe answerable kwa yule Governor ambaye anawakilisha lile Jimbo. Upande wa ma-sub-Chief, wawe na kiwango cha elimu fulani ambacho kiwango hiki ni kuanzia O-level na kuendelea na katika ile hali ya kuwa wao wanaudumu kama ma-Sub-Chief, na ma-chief na ma- DO, mtu anapochaguliwa.  Mtu anapochaguliwa kama Sub-Chief, asiwe kuwa ataishia pale kama Sub-Chief.  Kunapokuwa kuna DO ameondoka, Chief awe atapandishwa na Chief anapokuwa napandishwa mbele, Sub-Chief apande kama chief.  Kwa hivyo kuwe na ile hali ya mpango ule wa utaratibu. Siyo mtu amechaguliwa sub-chef anakaa pale kama Sub-Chief nazeekea  pale.  Kwa hivyo hiyo hali iangaliwe pia.

Tuangalie upande wa mapeni ya serikali, Finance yaani:  Ile rasilimali inayopatika, pesa zinazopatikana katika jimbo kupelekwe asili mia ishirini na tano katika serikali kuu.

Pesa za retirement:  Mtu anapositahafu, ile yale malipo yake ya kusistafu anapolipwa, yawe yanaongezeka kila mwaka baada ya mwaka.  Kulingana na hali ya uchumi vile inavyo patanda.

Na kimalizia upande wa Tume:  Tume ziweko lakini ziwe njini ya hii Tume ya kurekebisha Katiba, tume zote siwe answerable kwa Tume ambayo irekebisha  Katiba.  Na kuundwe ofisi kuanzia mamlaka ya juu hati ya chini.  Kiwango cha Sub-Location. Katika hii Tume ya urekebishaji wa Katiba na Undaji wa Katiba.  Nafikiri hiyo imetosha.

**Com. Riunga Raji:**  Asante sana, Sammy Phonto, nafikiri tutakupatia dakika tano hivi.

**Sammy Phonto:**  Asante sana Tume ya ujunguzi wa Commission, mimi kwanza nasimama hapa nikisema naunga mkono

serikali ya majimbo. Na nikisema hivyo ni kwamba hapa kwetu pwani tumelalaliwa sana kwa mda mrefu. Tukiangalia saa hii hapa, tuko na Kilifi Institute of Agriculture, ambayo Institute hii inatoa tuu certificates. Hali kule juu wanatoa Diploma. Hasa mtu akitoka Kilifi Institute hapa na mtu ametoka kule juu yuko na Diploma in Agriculture, chapo zote ni Institutes of Agriculture, kazi ikitokea ukienda pale mwenye certificate eti umetoka Kilifi hapa unaanchwa pale, anachukua yule mwenye Diploma kwasababu ametoka kule. Kwa hivyo hapa nafikiri wametulalia kwa sababu tulitanganywa tu kwamba hapa, tunajengewa College hapa ya Agriculture Institute hapa Kilifi lakini haifai chochote kabisa. Una kaa pale ukitoka pale ile karatasi yako na haikusaidie chochote kabisa na urudi nyumbani na huku, ulime shamba yako uko, upande tomato zako na kila kitu lakini kazi uwezi kuandikwa.

Pili tukiangali katika hizi secondary schools, hakuna moja hapa Coast ambayo ni National School. Zote hizo zimeenda kule bara. Na nikisema hivyo ni kwamba mimi mwenyewe nimeishi bara, nimesomea bara huko ukikuyuni, na hali ya kule ya maisha nimeiona miaka ile nimekaa kule. Iko tofauti kabisa na sisi. Hapa pwani sisi ni kama ambaye tulikufa kitambo sana na hata hatujulikani kabisa. Rafiki yangu Amos Kingingi yule pale, tulifanya kazi, kabla hajaenda ku-join University, shule moja hapo malindi. Tulikandamizwa hivi mpaka ikabidi pesa zetu tisiache pale ile kazi tuiache. Kwa sababu hata kuomba ruhusa kwenyewe huende kwenu kwasababu kwenu kuna mahafa, unaambiwa ukienda huku, pesa zako za siku huyo sina kantwa hulipwi. Sasa mambo kama hayo ni yale ya kutungandamisa kabisa sisi.

Tunalalamika zaidi, tukasema kwa nini hapa pwani sisi tusipate chuo kikuu yaani university. Hapo tena sisi tukavikwa tu blanketi kwenye macho hapa. Wakati ukielekea sehemu za Lamu kuna mahali hapo panaitwa Sabaki, kabla hujafika bridge, utaona pale kibao kimeaandikwa Moi University, na kimebakia kile kile kibao pale mpaka ikajengwa, Moi University Eldoret. Na sisi tuko hapa hapa. Kwa hivyo pwani tumelalaliwa sana. Graduates tuko nao, lakini kazi pia hawapati. Wewe utatoka University kule, na degree yako kama Bachelor of Science, tuseme Engineering, ukienda mahali kutafuta kazi, unaambiwa ni lazima uwe na experience ya miaka mitano. Experience hiyo nitaitoa wapi? Wakati kazi zijafanya. Hasa unakuta kazi hiyo hiyo yako, ambayo wewe una degree holder, unainyimwa, inapatiwa form four hapa, hata kama ni form two, kwa sababu yeye anatoka kule juu. Usiposema "chamge" ni "atherere," kazi anapata. Lakini huyu mkiriama hapa kama mimi sasa Katana, kazi hiyo mimi siipati.

Kwa hivyo nafikiri tukiwa serikali ya majimbo, tunaweza kujitawala wenyewe, na tutakuwa tunajijua. Kwa sababu wengine wemeongea hapa, office nyingi ukiingia hapo, usikii lugha ya taifa ama kizungu, aaa, ni kile kikwetu kinakuwa pale ndani. Hasa huko pale huelewe watu wanaongea nini na nini, umeenda pale na vi-certificate vyako pale kutafuta kibarua, hata hakuna mtu anakushughulikia, ama unaampiwa try next time.

Hasa unakuta kuna kule kulalaliana. Kwa hivyo nafikiri tuko na serikali ya majimbo, tutaweza kujitawala wenyewe vizuri sana. Kwa sababu pesa zinazo ingia hapa port kwa siku, ni pesa nyingi sana. Kwani pesa hizo zote zinaenda huko. Tukiangalia hapa kwetu shule yetu ya primary, hii hapo unaiona pale, madawadi yenyewe ni yale yote mmeyaona hapa. Lakini je ukienda

kule bara, namna gani, mambo kule ni tofauti kabisa na mambo ya huku kwetu. Unaambiwa, watu wanaambiwa shule za primary sisifanye mitihani hii ya majaribio, mocks. Hasa huku tunadii tunasema hakuna, tumeambiwa hakuna mocks kabisa. Lakini ukiangalia kule juu, mitihani inaendelea. Mimi nikiwa mwalimu, na nikatoka Government nikaingia Private Sector. Watu wanaambiwa huku hakuna mitihani ya mocks kwa primary schools, pale private nilipokuwa nafundisha, tunatoa mitihani kutoka Koibateki, kwani hao huko si watoto. Ama hawa wetu wa huku si watoto? Kwa hivyo kuna kule kudanganyana kule. Kuvishana blanketi kenye machao. Hiyo ndio tunasema sisi hatutaki watu wa pwani. Tunataka serikali ya majimbo. Asanteni.

**Com. Riunga Raiji:** Nafikiri tutapatiana dakika tano tano ili tumalize. Kwa sababu naone list inaendelee kuwa ndefu, sijui kama watu wako lakini tunafwata list. Bahati Ngumbao yuko, Japheth Ngumbao, Nelson Kunga Chea, Taito Mazoea ameongea, Nathan Mweri, Okey karibu, Nitakupatia five minutes.

**Nathani Mweri:** Kwanza habari zenu, mimi ni Nathani Mweri Manya, Machache nitachangia, kwanza haki za ardhi, iwe ni kwa kila mwana Kenya aliye na umri wa miaka kumi na minane. Aipate kama vile kitambulisho, na pale anapoweza kumiliki kiwango cha juu kiwe akizidi hekari thelathini, maoni yangu. Na tena akimiliki, amiliki juu na huko kusimu pia. Hata kama kutaweza kupatikana mafuta, iwe ni mali yake. Usije upate dhahabu pale uniambie niondoke. Apana, labda tuwe tunaelewana, iyo ni maoni yangu.

Haki za walemavu: Kama vie vipovu, wazimu, viwete na wengineo, serikali yetu ambayo tutakuwa tuko nayo, ambayo itatumia Katiba hii, iwe ikiwatengea bado maalumu la kuwapatia kila mwezi ikiwezekana. Kupitia kwa viongozi wao kama vile ma-DO, ama ma- Chief, ama wowote walio karibu nao. Ili nao wapate manufaa katika mapato ya serikali ile itakayokuweko

Tatu, kwasababu tunakuta kwamba tunafaida nyingi tunazosipata kwa wanyama wa pori na utalii, lakini vile vile, kama wenzangu walio tangulia kusema kwamba wanyama wa pori huwa waaribu mmea ya watu ama wakati mngine hudhuru watu kabisa. Maoni yangu kuhusu hao, ama kuhusu rasilimali hizo, kama sisi ambao tuko na msitu hapa karibu, kuwa kuna kama ndovu, kiboko, na wanyama wengine. Wale wanyama kimaoni ni kwamba, lilo bado linalo patikana pale, sabini na tano za mia, ziutumie wale wanaokaa kando kando ya ule msitu. Ama eneo hili hasa, ama eneo lile la umbuge ambao ule mstitu unakaa. Rasimali zozote kuanzia ile mti, wale wanyama, 75% iwe itautumia wale, na hile sehemu iliyo bakia iende katika ile serekali kuu. Na wale wanyama kwa sababu lile pori haliongezeki, wale wanyama wawe wanafanyiwa culling kila mwaka mara moja. Kama vile ndovu, wanaendelea kusaana na kusaana na pori ni lile, kwa hivyo wanafikia mahali ya kwamba hata wale askari wenyewe kulinda, hawezi kuwahakimu na wanatoka, wakati mwingine hata wale askari wanasema sasa tufanye nini?

Kwa hivyo wale ndovu wawe wakipunguzwa ama wanyama wengine wale wa bori. Ingawaje tunawapiga picha lakini wafikie kiwango cha kuweza kudhuru maisha ya watu. Kuwe kunafanyiwa culling, wanapunguswa mwaka kwa mwaka.

Kama vile tulivyosikia vilio vya wenzetu wengine, kwamba tunsema upande mwingine memea yetu inalemewa, tumeona ni

kwamba serikali, ile itakayo kuweko, ambayo mimi naunga mkono wale wenzangu wote walio sema serikali ile ambao wamesema kutoka hapa, majimbo, kwanza kabisa watenge pesa zitakazo kuwa sikinunua mazao ya eneo lile la uwakilishi mbugeni. Mmea wowote ule ambao uko pale, serikali ihakikishe kwamba inaununua. Ili kwapatia kipato wale raia wa pale. Na kama si mmea, kama ni ufukaji, hata kama wanafuga punda, serikali ingalie kutatokea soko wapi la kwauza wale punda ili kwamba yule raia anayekaa pale aweze kupata pato lake kwa kile kitu ambacho yuko nacho.

Kwa mfano wenzetu wa North Eastern, kama wao ni wafugaji na ikiwa serikali haitaangalia kwa kupeleka ng'ombe ama ngozi ama maziwa, watakula nini? Itabidi kuwaletea msaada. Kwa nini na wana kitu wanaweza kukifanya na kikatoa bato. Kwa hivi iwe ni jukumu la serikali kutafuta ni wapi itaipeleka ile rasilimali inayotoka pale mahali. Hata kama ulioko pale ni mchanga, serikali iangalie itafanya nini na ule mchanga wao ndio wale watu wapate kipato ili wasiwe masikini.

Oni lingine, kunazo Sheria ambazo sinazimamia rasilimali za maji, sisi hatujui sana, lakini tunasikia, kunazo sheria ambazo sinasimia kama mito na wakati mwingine huwa inazuia watu kufanya shughuli zao za kimaendeleo. Maomi yangu ni kwamba, zile Sheria zichunguzwe tena katika Katiba hii ili kwamba raia wa kawaida, awe anaruhuza ya kuweza kuyatumia maji yale kwa kufanya kama unyunyizaji wa mashamba, na maendeleo mengine muhimu. Kama ni maji ya mito ama ya ziwa lile lililoko karibu naye. Na pia serikali yenyewe ihakikishe kama wale raia wa pale wa hawana uwezo wa kufanya mradi wa kuyatumia yale maji, ibunishe mradi kwa manufa ya wale wananchi wa pale ili waweze kupata mapato kulingana na ule mto ama ziwa.

Mwisho serikali iwe ikitoa mbengu kila msimu kwa raia wa kila eneo la uwakilishi mbungeni kulingana na mmea ule unaoweza kumea pale na ukafanya vizuri. Asanteni sana.

**Com. Riunga Rasiji:** Sammy Karama, Galu Mwago, Wilson Baya, Karibu.

**Wilson Baya:** Asanteni sana, kwanza nashukuru sana kwamba Kakoneni kumekuwa kikao cha kuweza kutoa maoni. Nilikuwa zitegemeei. Sikuwa na matumaini, sikujua kama tutaweza kuzungumza kutoka hapa hapa. Kwa hivyo ninatoa shukurani.

Mimi sitazungumza mengi, kwa sababu yale ambayo ninataka kuyazungumza yako katika ile memorandum ambayo ilipeanwa hapa. Sasa nikuweka tu makazo kidogo. Serikali ambayo mimi kwa maoni yangu ninahiitaji ni ile serikali ya majimbo. Na hii serikali ya majimbo ninayo hitaji mimi, ninataka ifahamike wazi ya kwamba huo mwaka wa sitini na tatu, kulikuweko na majimbo. Sio yale majimbo yale ambayo tunayataka sasa. Tunataka majimbo yale ambayo yana uwezo kamili. Yale hayakuwa na uwezo. Majimbo ambayo tulikuwa nayo mwaka wa sitini na tatu, ilikuwa yanaendeshwa na ile serikali kuu. Serikali kuu inaendesha majimbo chini. Na kwa hivyo kulipotokea maadui, wale wa yale majimbo huko juu, ambao wana uwezo mwingi kuliko wengine, wakayaua yale majimbo.

Maoni yangu ni kwa katika Katiba, idhipitike wazi ya kwamba tunataka majimbo ambayo yana uwezo na yana nguvu na ndio ambayo yataendesha ile serikali kuu. Kusema hivyo ni kwamba mapato ya kila jimbo, jimbo lenyewe liwe na uhuru wa kutumia 75%, na 25% ndio ambayo itapeanwa kwa serikali kuu ili iweza kuendesha mambo yake ya kiserikali kuu. Kwa sababu ni kutokana na kunyimwa pesa za kuweza kujiendesha ndiposa majimbo yakafaa. Kwasababu ilikuwa pesa zinatolewa zote, zipelekwe kwa serikali kuu ndio halafu jimbo liombe. Pesa za kuweza kujimdu. Halafu maadui ambao hawakutaka majimbo wakajua njia ya kufanya ni kuikataza pesa na yatakufa yenyewe automatically. Na yakafaa automatically.

Serikali ya majimbo hapa kumetolewa list ndefu sana, ya malalamishi, lakini serikali ya majimbo ikiingia, hiyo list itakuwa fupi. Ni kama wale wasomaji wa bibilia wanajua. Wakati wa Musa sheria zilikuwa kumi, halafu Yesu Kristo alipokuja anafundisha wanafunzi wake akasiweka zikawa mbili. Akasema mpende mwenzio na upende Mungu na upende jirani yako. Alipokuwa akiondoka anapaa kurudi juu akaivuja akawa moja. Akasema, pendaneni kama vile nilivyo wapenda nyinyi. Hivi ni kwamba serikali ikiwa ya majimbo matatizo yote ya ardhi ambayo yametolewa, ilivunjwavunjwa, matatizo yote ya ma-hospitalini, matatizo yote ya mashuleni, yote yatarudi kwa jimbo. Kwa hivyo jimbo lenyewe litaangalia shule zake, mashamba yao, bahari yake na kila jimbo huku litaangalia vitu vyake. Sasa matatizo kutakuwa hakuna.

Tunataka yule Commissioner of Lands awe hapa kwa jimbo, na kila jimbo liwe na wake. Na tunataka Lands Act iwe moja. Sisi hapa pwani zote tuko katika Kenya hii, Kenya uhuru, kwa nini pwani hapa sisi tunatawaliwa na Act’s tatu za Land na huko mahali kwingine ni Act moja. Hapa kuna Presidential Act, wanaiita nini, Presidential decree along the sea shore, kuna, what do they call it, kuna ile Mazrui Land Act, halafu kuna ile Act ya kawaida. Kwa nini sisi hapa pwani tuwe na watu watatu ambao lazima ukitaka ardhi, aidha huende kwa huyu, au uende kwa yule na hii sababu mas-squatter umebakia hapa pwani. Ni kwasababu huna mahali pa kwenda. Ukienda kwa Commisioner of lands, unaambiwa hii ni mambo ya Mazrui land. Ukitaka kwenda baharini, unaambiwa hii ni lazima tumulize Rais. Hiyo kitu hatutaki. Katika Katiba tunataka ipandishwe Lands Act iwe moja na tena ikawaliwe katika jimbo. Na maneno itakuwa imeisha.

Hata nafikiri nimemalisa maanake hiyo ndiyo muhimu. Kwa sababu ikiwa katika jimbo ukulima tutasimamia wenyewe kama ni kuakugizia matinga tuyagizia katika jimbo level. Hakuna mtu tutafanya reference kwake. Na asante. Nafikiri nimechukua chini ya dakika tano.

**Com Riunga Raiji:** Asante sana sasa Dismas Thoya, na huyo ndiye atakuwa wa mwisho kulingana na list yetu.

**Dismas Thoya:** Basi Asanteni sana kwa ajili ya kupata wakati huu ambao nitaenda kuzungumza machache sana pengine kiwezekana ninachukua chini ya dakika tano.

Mimi kwa upande wangu ningelipendelea serikali ya majimbo. Na nikisema serikali ya majimbo simaanishi ya kwamba wale

ambao si wa hapa pwani, wauawe ama wapekwe kwao. La, lakini kila jimbo liwe na nafasi ya kujitawala.

Jambo lingine ambalo nafikiria ikiwa serikali itatawala ya majimbo, shida hizo sitaondoka ni upande wa passport ama hati ya kusafiria. Unaona ya kwamba mara nyingine unaweza kuona mtu amepata nafasi ya kwenda ulaya, amepata barua ama mambo yale ambayo alikuwa anayangojea yamefika. Na yeye anasitahili apate passport ili asafiri. Lakini ukifika katika office ya uhamiaji, unaona mtu huyo napelekwa huku, na kule na kule anaambiwa atoe pesa ambazo hata si halali yeye atoe unaona. Na mara nyingine unaona ya kwamba hata ile siku yake ya kufika, ya kusafiri ama kuondoka katika ile nchi ahame imefika, na passport hajaipata. Mimi mwenyewe nina passport na nilipata shida sana nikiitafuta. Nili-apply hiyo passport, nikaenda kwa Immagiration Office nikaambiwa ngoja mpaka pengine wiki ijayo, nikifika ile wiki ijayo, nikaambiwa ile application yako imechukuliwa na askari wa Special Branch, kwa hivyo nenda Malindi. Nikifika Malindi, nikaiona kweli ni file yangu, nikasema sasa hii inakuwa namna gani? Kuna mtu mwingine akitatafuta passport ni siku moja amepata hiyo passport. Lakini mimi ninambiwa kwamba niende kwa office ya Special Branch huko pengine nitapata mambo yangu huku nizungumze na wao. Nikifika pale niliambiwa lete lunch, Shilingi ngapi, nikaambiwa hata kama huna pesa nyingi, toa angalau Shilingi mia tano. Hizo mia tano mimi sina. Kwa hivyo nafikiria kwa hivyo hata si mtu ambaye anaenda ulaya pekee yake. Lakini kila Mkenya anayo kabisa haki ya kuwa na passport. Na basi mtu ambaye anatafuta passport na mtu ambaye anatafuta kitambulisho, huyu wa kutafuta kitambulisho ndiye ambaye anaweza kuchukua pengine muda marefu. Lakini passport, ni kitabu ambacho kiko tayari na hii picha tu na jina lako linaandikwa na unapewa, the very day. Kwa hivyo wapendwa mkifika uko katika mambo ya Katiba huko, na haya mambo ambayo manaandika hapa kama ni kweli yatafika uko, tafadhali sana, mambo ya passport, na mambo ya Birth Certificate.

Naona si halili mtu kuonga ili apewe birth certificate. Birth certicate ni kitu ambacho ni cha siku na hiyo na mtu apewe mara moja na aende zake. Lakini Birth Certificate unaona mtu anaambiwa, wewe ngoja kidogo, sijui nenda ukajukue kitambulisho cha mama yako, pengine yule mama alikufa, mpaka hiyo kitambulisho cha mama. Mimi siku ya kutafuta hii kitu, niwaambia ya kwamba apana, mimi baba alikuwa mlevi na hana kitambulisho na wakati huo alikipoteza. Nikawaambia wazi. Wakasema haya basi, lete tutatengeneza. Kwa hivyo mambo ya passport na Birth Certificate, tafadhali haya ni mambo madogo sana. Na ikiwa mtu ametaoa zile qualifications, zile requirement, apewe Birth Certificate ama passport aende zake kama ataenda ulaya maataenda wapi, hatakama atakaa hapa Kenya ataenda, wacheni naye wacha apewe.

Jambo lingine ni kuhusu recruitment: Recruitment wapendwa hivi tumeona mambo ambayo si ya justice kabisa. Mtu mmoja anawo uwezo wa kuaandika squad nzima na mtu mwingine hana. Haya mambo haya ya education, at least poleni sana ma-Secretary wa Commissioners, unaona ya kwamba mtu anaambiwa uwe umefika form four ama pengine form six ndio uaandikwa police. Likini mimi ninao ushuhuda kwamba kuna asikari GSU ambao hawajui kabisa hata kuandika jina lake mtu hajui. Anaandikwa anamaliza training anaenda tu, anachukua mbunduki awaweka mgongoni anaenda kuchunga ng'ombe. Anaandikiwa barua pengine kutoka nyumbani, akifika hapa kwa College ama katika Station hiyo ambayo anafanyia, anachukua ile barua anapatia mtu nisomee hii barua kwasababu he does't know how to read. Tafadhali hiyo serikali ya majimbo itaua

hayo mambo yote. Kwasababu si halali mtu hawehajasoma kabisa, aandikwe Askari na mtu ambaye amesoma, pengine amefika form six ama form amekuja anaangaliwe wewe sijui mguu wako sijui uko namna gani. Kwasababu hana mkubwa ambaye anamjua.

Siku moja niliona aibu sana Kilifi. Kijana alifika form six, mwili wake ni salama kabisa. Akendeshwa mbio na wenzake, ikifika upande wa medical check up, upande wa ile urine, anaambiwa hapana wewe tumeona sasa wewe ni mgonjwa. Akasema hapana, mimi ni mgonjwa? Yeye amejipima huko amaeona ni sawa, hapa yule sijui yule Recruiting Officer anasema wewe sasa ni mgonjwa. Siku hiyo mimi niliona kabisa, kijana anasukumana na mtu ambaye ana mapeke hapa. Kwa sababu anaanchwa na hali ambaoyo si nzuri. Anaanchwa na sababu ambayo hakuna. Kwa hivyo nafikira majimbo yatamaliza hayo. Sizungumzi habari ya ukabila lakini unajuwa tusifanya watu wakauana. Kwasababu hapa mtu akiwa haki yake inachukuliwa, na pengine uhuru walipigania pamoja, na yeye ananyang'anywa, hao watu watauna na hao wakubwa ndio watafanya hawa watu wauane. So take care. Asanteni sana

**Com. Riunga Raiji:** Haya asanteni sana, Wananchi wale wamevumilia kutoka asubuhi mpaka saa hii. Sasa tumefika mwisho wa kikao hiki cha leo. Tuko tu katika Malindi, tunaenda pahali pengine na kwa sasa tutamuliza Reverend kama yuko, Pastor Peter Ponda, aje tumshukuru Mungu kwa kuwa na sisi tangu asubuhi. Karibu.

**Pastor Peter Ponda:** Basi na natuombe. Tunakushukuru Mungu wetu kwa wakati mwema ambao tumekuwa mahali hapa, wakati wa amani, wakati ambapo Baba umetupa nafasi ya kuongea yale ambayo umetuwesha kuongea, tunaomba Bwana, ukapate kuwa pomoja na kila moja wetu na hata mwana uakazidi kutabariki kama Wananchi wa Kenya ili Bwana katika kurekebisha Katiba yetu, umoja wetu baba kama taifa ukapate kuendelea kuonekana.

Na Bwana ukabariki ma-Cmmissioners wetu katika kazu ngumu hii, Bwana ukawape hekima ambayo mwana inatoka juu, ili kuwa mapenzi wakatengeze yote kwa ajili ya utukufu wa jina lako.

Tunapoachana hapa na hata tunakumbuka mkutano wa kesho Malindi, Bwana pia ukaendelee uhubariki. Uwe pamoja nasi zote na ni katika jina la Yesu aliye ni Bwana na Mkozi tumeomba.

AMEN.
Meeting ended at 5.30 p.m.

&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&.